# KISWAHILI

## Michepuo Mingine

## Kidato cha 6

## Kitabu cha Mwanafunzi

***© 2022 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi***

*Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi . Haki zote zimehifadhiwa. Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi  wakati yaliyomo yamenukuliwa.*

# DIBAJI

**Mwanafunzi mpendwa**

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kwa kutoa kitabu hiki cha Somo la Kiswahili, Michepuo mingine, kidato cha nne kitabu cha mwanafunzi. Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo katika kila ngazi ya elimu kuweza kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa w a ujifunzaji. Mambo mengi yanaathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo. Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unakuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi kwa msaada wa walimu ambao majukumu yao ni kufanikisha ufundishaji. Utapata stadi zinazofaa kukuwezesha kutumia yale uliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, utaonyesha tofauti siyo tu katika maisha yako bali hata kwa taifa.

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na w anafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika ufahamu huu, Ili kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako litakuwa :

- Kuendeleza maarifa na stadi kwa kufanya kazi na mazoezi yanayolenga kwenye mada. Kuwasiliana na kupeana taarifa sahihi pamoja na wanafunzi wengine kwa kupitia wasilisho, mijadala, kazi katika makundi na mbinu

nyingine za ufundishaji kama: michezo ya kuigiza, utafiti, uchunguzi na utafiti katika maktaba, katika mitandao na nje ya shule.

- Kushiriki na kuwajibika kuhusu ujifunzaji wako na kufanya utafiti, uchunguzi kwenye maandishi yaliyochapishwa /mtandaoni, wataalam na kuwasilisha matokeo ya utafiti.
- Kuhakikisha ufanisi mzuri wa mchango wa kila mwanakundi katika kazi sahihi uliyopewa kupitia maelezo na majadiliano unapoongea hadharani.
- Kutoa hitimisho sahihi kuhusu matokeo ya utafiti uliotokana na mazoezi ya ujifunzaji.

Napenda kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki kutoa mchango wa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (CTLR-REB) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza.

Pongezi muhimu ziwaendee walimu wa Chuo Kikuu cha Rwanda kwa msaada wao wa kutoa wataalamu ambao ni wahadhiri na wachoraji waliosaidia kusimamia, kuendeleza na kufanikisha uboreshaji wa kazi hii kuhusu picha na michoro sahihi. Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata .

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB**

# SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki. Kitabu hiki kisingeliwezekana kufanikiwa bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki, jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu ziendee vyuo vikuu na shule mbalimbali kwa kuwaruhusu wafanyakazi wao kufanya kazi na Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi katika mradi wa utoaji wa kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa wahadhiri na walimu ambao juhudi zao na uandikaji wa kitabu hiki ulikuwa wa thamani.

Mwishowe, neno la mwisho la shukrani liwaendee wafanyakazi wote wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (CTLR-REB) walioshiriki katika mchakato wa kufanikisha uandikaji wa Kitabu hiki.

**Joan Murungi**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana ( CTLR)**

# YOLIYOMO


**DIBAJI** ........ iii

**SHUKRANI** ........ v

**UTANGULIZI** ........ 1

**MADA KUU 1: MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI** ........ 6

**MADA NDOGO: MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA BENKI** ........ 6

**SOMO LA 1: BENKI NA SHUGHULI ZAKE** ........ 7

1.1. Kusoma na Ufahamu: Penye Nia Pana Njia ........ 7
1.2. Msamiati kuhusu Benki ........ 10
1.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi ........ 10
1.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Benki ........ 13
1.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ........ 14
1.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu cha Habari ........ 14

**SOMO LA 2: MANUFAA YA BENKI** ........ 15

2.1. Kusoma na Ufahamu: Manufaa ya Benki ........ 15
2.2. Msamiati kuhusu Manufaa ya Benki ........ 18
2.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi ........ 20
2.4. Matumizi ya lugha: Manufaa ya benki ........ 20
2.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ........ 21
2.6. Utungaji: Utungaji wa Kifungu cha Habari ........ 21

**SOMO LA 3: AINA ZA BENKI** ........ 22

3.1. Kusoma na Ufahamu: Benki Nchini Rwanda ........ 22
3.2. Msamiati wa Msingi ........ 24
3.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi ........ 24
3.4. Matumizi ya Lugha: Aina za Benki ........ 24
3.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ........ 26
3.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu cha Habri ........ 26

**SOMO LA 4: WATUMISHI WA BENKI NA MAJUKUMU YAO** ........ 27

4.1. Kusoma na Ufahamu: Watumishi wa Benki na Majukumu yao ........ 27
4.2. Msamiati kuhusu Watumishi wa Benki na Majukumu Yao ........ 29
4.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi ........ 30
4.4. Matumizi ya lugha: Wafanyakazi Mbalimbali na Shughuli zao ........ 32
4.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Mazungumzo kati ya Afisa wa Mikopo na Mteja ........ 33
4.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu cha Habari ........ 33

**SOMO LA 5: KARATASI MAALUM ZINAZOTUMIWA KATIKA BENKI** ........ 33

5.1. Kusoma na ufahamu: Mazungumzo kati ya Meneja wa Benki na mteja. ........ 33
5.2. Msamiati kuhusu Kifungu cha Habari ........ 36
5.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi ........ 36
5.4. Matumizi ya Lugha: Katarasi Maalum Zinazotumika katika Benki. ........ 37
5.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ........ 38
5.6. Kuandika : Utungaji wa Kifungu cha Habari ........ 38

MADA KUU YA 2: FASIHI KATIKA KISWAHILI .......................................40
MADA NDOGO: TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI.........................40
SOMO LA 6: HADITHI FUPI .......................................................41
6.1 Kusoma na Ufahamu: Majuto ni mjukuu ........................................41
6.2. Msamiati kuhusu Hadithi Fupi ..............................................46
6.3. Sarufi:Virai Nomino........................................................47
6.4. Matumizi ya Lugha: Fani na Maudhui katika Hadithi Fupi ....................49
6.5 Kusikiliza na Kuzungumza ...................................................54
6.6 Kuandika: Utungaji .........................................................54
SOMO LA 7: USHAIRI KATIKA KISWAHILI ...........................................54
7.1. Kusoma na Ufahamu: Vaa vazi la Heshima.....................................55
7.2. Msamiati kuhusu Shairi.....................................................57
7.3 Sarufi : Virai Vitenzi.......................................................58
7.4. Matumizi ya Lugha: Ushairi.................................................59
7.5. Kuzungumza na kusikiliza: Majadiliano ......................................62
7.6 Utungaji: Utunzi wa Shairi ..................................................62
SOMO LA 8: UFAFANUZI WA RIWAYA.................................................63
8.1. Kusoma na Ufahamu : Muhtasari wa Riwaya ya Adili na Nduguze .................63
8.2. Msamiati kuhusu Riwaya .....................................................65
8.3. Sarufi : Vishazi.............................................................66
8.4. Matumizi ya Lugha: Sifa za Riwaya ...........................................68
8.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano .......................................70
8.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu ...............................................70
SOMO LA 9: UFAFANUZI WA TAMTHILIA .............................................70
9.1. Kusoma na Ufahamu: Sura Moja ya Tamthilia ...................................71
9.2. Msamiati kuhusu Sura Moja ya Tamthilia ......................................77
9.3. Sarufi: Vishazi Tegemezi .....................................................78
9.4. Matumizi ya Lugha: Fani na maudhui katika Tamthilia ..........................80
9.5. Kusikiliza na Kuzungumza : Majadiliano........................................83
9.6. Kuandika : Uandishi wa Muhtasari wa Tamthilia ................................83
MADA KUU YA 3 : UBUNAJI .......................................................86
MADA NDOGO: HOTUBA NA UFUPISHO .................................................86
SOMO LA 10: MAANA YA HOTUBA.....................................................87
10.1. Kusoma na Ufahamu: Hotuba ya Meya baada ya Kazi za Umuganda .................87
10.2. Msamiati kuhusu Hotuba ya Meya...............................................89
10.3. Sarufi: Uambishaji wa Vitenzi ................................................91
10.4. Matumizi ya Lugha: Mambo Muhimu katika Hotuba ................................93
10.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano .........................................94
10.6. Kuandika: Utungaji wa Hotuba .................................................94
SOMO LA 11: MUUNDO WA HOTUBA....................................................95
11.1. Kusoma na ufahamu: Hotuba ya Mkuu wa Kamisheni ya Umoja na Maridhiano
11.2. Msamiati kuhusu Hotuba.......................................................97
11.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi Awali Utendewa na Mzizi .......................98

11.4. Matumizi ya Lugha: Sifa za Hotuba ... 100
11.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ... 101
11.6. Kuandika: Ufupishaji wa Hotuba ... 101
**SOMO LA 12: UFUPISHO ... 102**
12.1. Kusoma na Ufahamu: Hotuba ya Daktari Mkuu ... 102
12.2. Msamiati kuhusu Hotuba ... 103
12.3. Sarufi :Uambishaji wa Vitenzi:Viambishi katika Vitenzi na Viambishi tamati . 105
12.4. Matumizi ya Lugha: Ufupisho ... 108
12.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ... 111
12.6. Kuandika : Ufupishaji wa Hotuba ... 112
**MADA KUU YA 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO ... 114**
**MADA NDOGO: MIDAHALO NA MIJADALA ... 114**
**SOMO LA 13: MDAHALO ... 115**
13.1. Kusoma na ufahamu : Mdahalo ... 115
13.2. Msamiati ... 125
13.3 Sarufi: Uambishaji wa maneno ... 127
13.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Mdahalo ... 129
13.5. Kusikiliza na Kuzungumza : Mazungumzo na Majadiliano ... 130
13.6. Kuandika: Utungaji wa Mdahalo ... 130
**SOMO LA 14: MJADALA ... 130**
14.1. Kusoma na Ufahamu: Mjadala ... 130
14.2. Msamiati kuhusu mjadala ... 136
14.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno kuhusu Vivumishi na Vitenzi ... 136
14.4. Matumizi ya Lugha: Sifa za Mjadala ... 139
14.5. Kusikiliza na Kuzungumza : Majadiliano ... 141
14.6. Utungaji: Utungaji wa insha ya mjadala ... 142
**SOMO LA 15: UHUSIANO NA TOFAUTI KATI YA MIDAHALO NA MIJADALA ... 142**
15.1. Kusoma na Ufahamu: Midahalo na mijadala ... 142
15.2. Msamiati kuhusu Kifungu ... 144
15.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno ... 146
15.4. Matumizi ya Lugha : Mdahalo na Mjadala ... 148
15.5. Kusikiliza na kuzungumza : Majadiliano ... 149
15.6. Kuandika: Utungaji wa mjadala ... 149
**MAREJELEO: ... 150**

# UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha yenye asili ya kibantu ambayo hadi sasa imepiga hatua kimatumizi, kisarufi, kimsamiati na yenye kutumiwa na jamii mbalimbali barani Afrika na ulimwengu kwa ujumla. Jamii ya Wanyarwanda imezungukwa na jamii nyingine zinazozungumza lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, inahitajika kufanya mawasiliano katika nyanja mbalimbali hususan kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kitabu hiki kimeandaliwa kuwasaidia wanafunzi wa kidato cha sita michepuo mingine kuzoea kutumia lugha hii kwa ufasaha.

Masomo katika kitabu hiki yameandaliwa kwa kuzingatia matakwa na mahitaji ya nchi ya Rwanda katika kumjenga mwanafunzi aliye na uwezo wa kuisaidia jamii nzima katika kukabiliana na matatizo mbalimbali kama vile kujilinda na magonjwa ya zinaa pamoja na UKIMWI, kushughulikia masuala ya mazingira, usawa wa jinsia, kwa uchache. Lugha hii itamsaidia mwanafunzi kupanua mawazo yake katika kuwasiliana na watu wengine kutoka maeneo mbalimbali wanaotumia lugha ya Kiswahili. Aidha itawasaidia kuelewa maisha na utamaduni wa watu hao kwa ujumla. Pamoja na hayo, kitabu hiki kitamsaidia mwanafunzi kujenga tabia ya kuwa na heshima, uvumilivu, upendo, amani, haki, umoja na ushikamano, demokrasia na desturi ya kujitegemea. Vilevile, mwanafunzi ataweza kujenga tabia ya kujiamini na kuwa huru kwa kutoa mawazo yake binafsi na kuwasikiliza watu wengine huku akijenga uwezo wa kutimiza wajibu wake kwa kuheshimu haki za binadamu na kuzingatia utu bora. Mwanafunzi mwenye uwezo unaotarajiwa kupitia masomo yaliyoandaliwa katika kitabu hiki, atafanikiwa kukuza kipaji cha ubunifu wenye lengo la kuweza kutumia maarifa, stadi na mwenendo mwema alionao ili kushirikiana na wengine kulijenga taifa lake na kupambana na matatizo ya aina mbalimbali na hivyo kufanikiwa kujiendeleza yeye binafsi na hata jamii nzima kwa ujumla.

Lugha ya Kiswahili imepewa hadhi zaidi hasa tukizingatia kuwa wanafunzi hufundishwa lugha hii katika shule za sekondari na hata vyuo vikuu. Tukizingatia pia kuwa Serikali ya Rwanda imefanya juhudi nyingi kuipa nguvu lugha ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali, ni sharti vitabu vya kufundishia viandaliwe ili kufakinisha ujifunzaji na ufundishaji wake katika shule mbalimbali nchini. Kitabu hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia vipengele muhimu vyenye kumpa mwanafunzi maarifa, stadi na mwenendo mwema kupitia vipengele vifuatavyo:

1. **Kusoma na Ufahamu**

Kusoma na ufahamu ni vipengele muhimu katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Vifungu vya habari vilivyotumiwa kufunzia vimebeba stadi muhimu kwa kumwezesha mwanafunzi kuelewa miundo tofauti ya lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, wanafunzi wanatakiwa kuichunguza michoro iliyotumiwa na kutafakari kuhusu uhusiano kati ya michoro hiyo na vifungu vilivyotumiwa ili kuchochea na kukuza uwezo wake wa tafakuri tunduizi, utafiti na ugunduzi.

Wanafunzi wanatakiwa wasome kwa makini na kwa ufasaha vifungu vilivyopendekezwa ili waweze kukuza uwezo wao katika stadi ya usomaji na pia wajibu maswali yote waliyoyapewa chini ya kila kifungu.

### 2. Msamiati wa Msingi

Kila kifungu kilichopendekezwa katika kitabu hiki huambatana na ujifunzaji wa msamiati mpya ambao husaidia kumwezesha mwanafunzi kuitumia lugha ya Kiswahili bila pingamizi lolote. Kila mwanafunzi anatakiwa kuchunguza msamiati uliotumiwa kwa kuzingatia matumizi yake katika vifungu vya habari ili kujizoeza kuutumia pia katika miktadha mbalimbali. Ili kufanikisha ujifunzaji wa msamiati katika kitabu hiki, ni vyema kila mwanafunzi atumie kamusi ili kupata maana tofauti za kila neno na kulitumia katika miktadha inayofaa.

### 3. Sarufi

Kipengele cha sarufi nacho ni muhimu sana katika ujifunzaji wa lugha yoyote. Sarufi huihusu miundo sahihi ya lugha na mwanafunzi hawezi kufikia umilisi unaotarajiwa bila kuzingatia kanuni za kisarufi. Maneno yanatakiwa kupangwa vizuri katika sentensi kwa kuzingatia upatanishi wa kisarufi unaofaa kulingana na aina za maneno yaliyotumiwa. Ni vyema mwanafunzi atamke vizuri miundo ya lugha ya Kiswahili na afanye mazoezi mengi ya kumwezesha kutumia aina za maneno kwa ufasaha: nomino, vivumishi, viwakilishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, vihisishi. Maneno haya huchukua nafasi zake katika sentensi na kila mwanafunzi hutakiwa kuzingatia miundo yake tofauti katika miktadha ambapo hutumiwa.

### 4. Matumizi ya Lugha

Katika kitabu hiki, kipengele hiki cha matumizi ya lugha kimepewa kipaumbele ili kumjenga mwanafunzi aliye na uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili kwa njia mwafaka. Sehemu hii imegusia mambo kadhaa ambayo yanamtaka mwanafunzi atafakari kwa kina kuhusu masuala muhimu yanayoikabili jamii yake na ambayo anakutana nayo katika maisha yake ya kila siku. Isitoshe, matumizi ya lugha humtaka mwanafunzi aweze kujiongezea maarifa na stadi za aina tofauti katika vipengele ya lugha kama vile ufupisho na muhtasari, fasihi, midahalo na mijadala, hotuba, insha, nk. Ni kipengele ambacho hudhamiria kumsaidia mwanafunzi kuweza kujiamini kwa kuyafafanua vyema mambo mengi atakayokutana nayo maishani mwake kwa kuitumia lugha ya Kiswahili kwa njia sahihi.

### 5. Kusikiliza na Kuzungumza

Vipengele hivi vya kusikiliza na kuzungumza ni vipengele muhimu sana katika ujifunzaji wa lugha yoyote ile. Ifahamike kuwa, lengo kuu la lugha ni kuwasiliana na sehemu kubwa ya mawasiliano hujikita katika uwezo wa kusikiliza na kuzungumza. Kila mwanafunzi ajitahidi kuwasikiliza wengine darasani na hata nje ya darasa ili kujiongezea uwezo wake katika usikilizaji.

Watu wengine hujifunza lugha kutokana na hali kwamba hupenda kuwasikiliza watu wengine wakiongea. Kwa hivyo, wanafunzi waigize michezo yao katika makundi yao mbalimbali na wawasilishe kazi za makundi darasani. Midahalo na mijadala iliyopendekezwa itiliwe mkazo ili kila mwanafunzi aweze kuizungumza vizuri lugha ya Kiswahili na kusikiliza hoja na maoni ya wengine.

### 6. Kuandika

Kipengele cha kuandika ni kipengele muhimu sana katika kumjenga mwanafunzi mwenye uwezo wa kuitumia lugha ya Kiswahili kwa njia mwafaka. Ni vyema kila mwanafunzi ashiriki mwenyewe katika mazoezi mengi yaliyopendekezwa ili kukuza uwezo wake wa kuandika. Uakifishaji uzingatiwe katika mazoezi hayo kuhusu uandishi wa insha, mijadala, midahalo, mashairi, n.k.

# MADA KUU YA 1:

## MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

# MADA KUU 1: MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

## MADA NDOGO: MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA BENKI

**Uwezo Upatikanao katika Mada:** Kusikiliza kwa makini, kusoma vifungu vya habari na kutumia msamiati muhimu katika mazingira ya benki.


**Malengo ya Ujifunzaji:** Mwanafunzi amalizapo mada hii atakuwa na uwezo wa: kuchagua maneno au msamiati wa kutumia katika shughuli zihusianazo na benki, kulinganisha na kutofautisha aina za benki kwa kuzingatia huduma zinazotolewa kwa umma, kujaza vyema karatasi maalum zinazotumika katika benki na kujiunga na benki kwa ajili ya kupata huduma zilizopo.

**Kidokezo**

1. Uliwahi kuingia katika benki?
2. Kama uliwahi kuingia katika benki fulani, ulikuwa na shida gani?
3. Benki ina manufaa gani kwa jamii?
4. Elezea kuhusu wafanyakazi wa benki na majukumu yao.
5. Kuna aina gani za benki unazozifahamu?

## SOMO LA 1: BENKI NA SHUGHULI ZAKE

Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali hapo chini.




***Zoezi la 1: Jibu maswali haya kulingana na yale yaliyopo kwenye mchoro hapo juu.***

1. Ni watu gani unaowaona kwenye mchoro?
2. Eleza kile wanachofanya watu unaowaona kwenye mchoro huo.

### 1.1. Kusoma na Ufahamu: Penye Nia Pana Njia

*Soma kifungu kifuatacho ili uweze kujibu maswali yanayofuatia hapo chini.*

Katika kijiji kimoja, palikuwepo na familia moja iliyoishi kwa ufukara. Mume aliitwa Migambi na mkewe Shirubute. Watu hawa hawakuwa na nyumba ya kuishi. Kwao kupata pesa ya kupanga nyumba, lilikuwa tatizo kubwa. Waliishi bila shamba, bila mifugo na hata hawakuweza kupata bima ya afya na karo za watoto wao kwa urahisi.

Shirubute alipokuwa mjamzito, mume wake aliwazia mengi kuhusu afya ya mkewe na mtoto mtarajiwa.

Siku ya kujifungua ilipofika, Migambi aliamua kuwaendea marafiki zake ili wamkopeshe fedha za kumpeleka mkewe zahanatini. Alipomfikia rafikiye wa kwanza na kumuelezea shida yake, alimjibu kuwa hana sarafu hata moja na kumwelekeza kwa jirani yake. Migambi aliendelea na safari kwenda kwa jirani huyo ambaye naye alikuwa rafiki yake pia. Alipofika nyumbani kwake, alimkuta amelala kitandani akiwa mgonjwa. Yeye alikuwa anatarajia kwenda zahanati kupata matibabu. Hapo Migambi hakusema lolote aliamua kuendelea na safari yake kwa rafikiye wa tatu ili amsaidie kupata uwezo wa kumpeleka mkewe zahanatini. Rafiki yake huyu wa tatu, alikuwa hana pesa kwa sababu alikuwa amezitumia kwa kulipa bima ya afya na kununulia watoto wake vifaa vya shule na kuwalipia karo.

Mara hii, Migambi alirudi nyumbani kwa huzuni na kujiuliza kitu ambacho angeweza kufanya ili kuyaokoa maisha ya mkewe na mtoto wake. Alikuwa na mawazo kadhaa. Kwa bahati njema, alikutana na mwalimu mwema mmojawapo wa walimu wanaofundisha watoto wake. Mwalimu huyo alimuuliza habari zake. Muda mrefu ulikuwa umepita bila kuonana. Migambi alimuelezea tatizo alilokuwa nalo nyumbani kwake. Mwalimu huyu alikuwa mtu mwema, mwenye huruma na upendo. Kwa hiyo, aliposikia uzito wa tatizo aliloelezewa, bila kusitasita alimsaidia na kumpa pesa alizokuwa anahitaji kwa kutatua shida yake. Kweli, Migambi alikiona kitendo hicho kama jambo jema ambalo haliwezi kusahaulika maishani mwake. Alifurahi sana na kumshukuru kwa wema wake, kisha akarudi nyumbani kwake.

Baada ya kujifungua na kutoka zahanati, Shirubute na Migambi walikaa nyumbani na kuongea kuhusu yaliyowafikia kutokana na ufukara wao na namna wanavyoweza kufanya kwa ajili ya kuepukana na tabia ya kuombaomba tena misaada kutoka kwa majirani zao. Waliamua kufanya kila liwezekanalo ili waweze kujitegemea wao wenyewe. Shirubute alitoa hoja kwa mumewe Migambi kwa kumwambia kuwa aliwahi kusikia kuwa watu wengine hutajirika kwa kutumia mikopo kutoka benki. Mke huyu aliendelea kusema kuwa wanawake, vijana, wanaume na watu wote wenye miradi mizuri huipeleka benki ili kuomba mkopo na kupewa fedha watakazozitumia katika kuanzisha na kuendeleza miradi hiyo. Yeye alipendekeza wafikirie mradi mmoja ambao ungeweza kuwasaidia kuinua maisha yao wakatoka katika hali ya umaskini na kuwa matajiri kama watu wengine. Hapo waliamua kununua shamba kubwa na kuanzisha shughuli za ukulima na ufugaji wa mifugo midogo midogo. Wao walipanga kulipa fedha hizo kutokana na pato lao kutoka kwa mifugo na shamba lao. Waliamua kupanda mahindi na kuyauza katika viwanda mbalimbali vilivyotengeneza unga wa mahindi katika kijiji chao.

Bila kukawia, Migambi alienda kwenye benki ya wananchi iliyopatikana katika kijiji chao cha Mwiza na kupeleka ombi lake kwa meneja wa benki hiyo. Alipofika kwenye benki, aliangalia wateja waliokuwa wakikaa kwenye ukumbi mkubwa wa benki na kuona kuwa alikuwa akiishi katika dunia isiyo na mwelekeo. Alishangaa kuona watu wengine wakisimama mbele ya madirisha ya makeshia wakihesabu noti walizopewa.

Hapo afisa wa kuelekeza wateja alimsogelea na kumuuliza alichokihitaji ili aweze kuhudumiwa. Alipomuonyesha karatasi zilizoandikwa mradi wake, aliombwa kwanza afungue akaunti ili naye awe mteja wa benki yao. Wakati huo, Afisa mwenyewe alichukua fursa ya kumwelezea Migambi kuhusu huduma zote zilizotolewa na benki yao na Migambi alifurahi.

Afisa alipozungumza na Migambi alitambua vizuri matatizo yake na kufurahia namna Migambi alivyofanya uamuzi wa kushirikiana na benki yao ili aweze kuinua maisha ya familia yake. Hivyo aliamua kumpeleka kwa Meneja wa benki hiyo ili amuelezee hali halisi ya maisha yake. Hapo ndipo Meneja alimsaidia kupata kazi ya usafi katika kampuni moja iliyojishughulisha na kusafisha mazingira katika mashirika mbalimbali. Migambi alifungua akaunti yake katika benki hiyo na kuanza kuhifadhi pesa zake huko. Baada ya miaka mitatu, Migambi alikuwa ameisha pata fedha za kujinunulia shamba lake na kujijengea nyumba nzuri huko kijijini. Mke wake alianza kupanda mimea ya aina tofauti na kuuza mavuno katika masoko mbalimbali yaliyowazunguka. Yeye alipohitaji fedha nyingi zaidi kuliko walizozipata, walikuwa wanaomba mikopo kutoka benki yao na kuipata bila wasiwasi kwa sababu walijulikana kwa uwezo wao wa kulipa kwa muda uliopangwa bila kushurutishwa.

Kwa sasa, Migambi na mkewe wanafahamu vizuri umuhimu wa benki na wao huichukua kama taasisi au shirika la fedha linalohifadhi pesa za watu ili zisitumiwe ovyo ovyo na ambalo husaidia watu kwa kuwapatia mikopo ya fedha ambayo hulipwa kwa muda uliopangwa. Mara nyingi wao huwaelezea watoto wao na watu wengine kuhusu huduma za benki yao na jinsi inavyoweza kuwasaidia kuboresha maisha yao.

**Maswali ya Ufahamu**

1. Familia inayozungumziwa katika kifungu hiki ni ya nani na nani?
2. Mwanamke Shirubute alikuwa na tatizo gani?
3. Migambi aliwatembelea marafiki zake kwa lengo gani?
4. Baada ya kujifungua na kutoka zahanati, walipanga kufanya nini?
5. Walipomaliza kukubaliana kuhusu hoja ya Shirubute, Migambi aliamua kufanya nini?
6. Migambi alielezewa nini na afisa wa huduma kwa wateja wa benki kuhusu maana ya benki?
7. Eleza msimamo wa Migambi baada ya maelezo aliyopewa kuhusu benki.
8. Eleza namna afisa wa huduma kwa wateja anavyowapokea wageni.
9. Jadili jinsi benki inavyoboresha maisha ya wateja wake.
10. Baada ya kusoma kifungu hapo juu, umepata somo gani?

11. "Penye nia pana njia." Eleza uhusiano uliopo kati ya maana ya methali hii na kifungu cha habari ulichosoma.

## 1.2 Msamiati kuhusu Benki

***Zoezi la 2: Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na matumizi yake katika kifungu hapo juu:***

1. Benki
2. Mteja
3. Mkopo
4. Fedha
5. Bima ya afya
6. Keshia
7. Mwelekezaji
8. Taasisi
9. Mradi
10. Riba
11. Wananchi
12. Kampuni

***Zoezi la 3: Tunga sentensi zenye maana kamili kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. Akaunti
2. Kutoa pesa
3. Kuhifadhi pesa
4. Kukopesha pesa
5. Kulipa karo
6. Mtu mwema
7. Tatizo
8. Zahanati
9. Uwezo
10. Keshia

## 1.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi

***Chunguza kwa makini sentensi zifuatazo ili utambue kauli ya tendo:***

1. Meneja alifunga akaunti ya mteja: Kauli /hali ya kutenda
   - Katika sentensi hii, kiima anatenda tendo.
   - Kiima: Mtu au kitu kinachotenda tendo katika sentensi.
   - Kiima: Meneja.

Ni nani alifunga akaunti ya mteja?

***Zoezi la 4: Jaza nafasi kwa kutumia vitenzi ulivyopewa: lilitendwa, alimkopesha, analimisha, alipata, alipelekwa.***

1. Mwalimu …………………pesa bila riba.
2. Mumewe …………………uamuzi.
3. Mzee yule………….........…kwa kutumia jembe jipya.
4. Shirubute………….......…. zahanati.
5. Jambo jema…………....…na mwalimu.

***Zoezi la 5: Tunga sentensi moja moja katika nafsi ya tatu umoja, zenye kauli ya kutenda, kutendwa, kutendesha kwa kutumia vitenzi ulivyopewa: kutenda, kupanga.***

**Maelezo muhimu**

- Mnyambuliko ni tendo linalofanyika kwa kuzalisha neno au maneno mapya kwa msingi wa neno jingine.
- Mnyambuliko wa vitenzi ni hali ya kuongeza viambishi kwenye mizizi ya vitenzi ili kupata kitenzi chenye maana nyingine.

**Kwa mfano :**

- Kazi ya kunyambua vitenzi inajitokeza katika kauli au hali mbalimbali kama vile kutenda, kutendea, kutendesha, kutendewa, kutendeka, n.k.

Hali /kauli ya kutendea : Hapa tendo linatendeka kwa manufaa au faida ya mtu au kitu kingine.

Mfano: Mama anawapik**i**a chakula watoto wake.

Hali /kauli ya kutendewa: Hapa kauli huonyesha kutenda tendo kwa niaba ya mtu fulani.

Mfano: Nyanya alilim**iw**a shamba lake.

Hali /kauli ya kutendeka: Hali hii huonyesha uwezekano wa tendo kutendeka.

Mfano: Mti umevunj**ik**a.

***Zoezi la 6: Nyambua vitenzi vifuatavyo kwa kuonyesha hali mbalimbali za mnyambuliko kwa kufuata mfano huu.***

| Hali ya Kutenda | Hali ya kutendea | Hali ya Kutendesha | Hali ya kutendwa | Hali ya kutendana | Hali ya kutendewa | Hali ya kutendeana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kusoma | Kusomea | Kusomesha | Kusomwa | Kusomana | Kusomewa | **Kusomeana** |
| ------- | ----------- | -------------- | Kuchezwa | ---------- | ------------ | -------------- |
| Kupiga | -------- | -------------- | ----------- | -------------- | ------------- | --------------- |
| ------ | ---------- | ------------- | ---------- | ------------ | kujengewa | ------------ |
| ------- | ---------- | ------------- | ------------ | Kupendana | | --------------- |
| ------- | ---------- | Kuimbisha | ----------- | ------------- | ------------ | -------------- |

***Zoezi la 7: Soma kwa makini sentensi zifuatazo kisha uzisahihishe.***

1. Mwanafunzi yule anasomeka kwenye shule yetu.
2. Mwalimu alitendana Migambi jambo jema.
3. Benki inakopeshwa pesa wateja wake.
4. Mkulima alinufaisha na mkopo wa benki.
5. Kiswahili kinafundisha nchini Rwanda.
6. Akaunti inafungulikiwa kwenye benki.
7. Migambi alifunguka akaunti ya hundi.

***Zoezi la 8: Chagua jibu sahihi kutoka parandesi kisha ukamilishe sentensi zifuatazo:***

1. Watu wasiojiweza nao wana haki ya………..akaunti kwenye benki. (kufunguka, kufungua, kufungia)
2. Kwa kuwa mradi wake umepangwa vizuri……mkopo. (amekubalina, amekubalika, amekubaliwa)
3. Bwana Migambi………………. nyumba nzuri. (alijijengeka, alijijengea, alijijengewa)
4. Kiswahili ………..katika shule za sekondari. (kinafundika, kinafundisha, kinafundishwa)
5. Watoto wale …………..sana. (wanapendeka, wanapendeshwa, wanapendana)
6. Watumishi wa benki …....... huduma wateja wao. (wanawapatiaa, wanawapatia, wanawapatiana)
7. Wanajamii ……………………. kwa kujiunga na benki. (walijitajirisha, walitajirisha, walijitajirishia)

## 1.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Benki

***Zoezi la 9: Soma maelezo yafuatayo kuhusu maana ya benki kisha ujibu maswali yafuatayo.***

**Maelezo muhimu**

- Benki ni taasisi au shirika la fedha linalohifadhi na kukopesha fedha kwa wateja wake wanaotaka kuendesha miradi yao mbalimbali.
- Miradi hiyo huweza kuwa ya kuzalisha mali kama vile kufanya biashara, kushughulikia kilimo na ufugaji, ufinyanzi, kufyatua matofali, kununua magari ya abiria na kubeba mizigo, kujenga nyumba za kupangisha, n.k.
- Benki ina lengo la kuimarisha uchumi na maendeleo ya wananchi.
- Benki inaweza kuwa njia moja ya kujitajirisha kwa kupewa mkopo na kuutumia ifaavyo.
- Ukipewa mkopo wa benki unaurudisha pamoja na riba.
- Benki hushauri watu wote kuipelekea pesa zao ili izihifadhi kwa usalama.
- Benki inamtoa mtu katika hatari ya kubeba fedha chungu nzima kila mahali alipo.

- Kulingana na maendeleo ya teknolojia, huduma za benki kwa wateja zimerahisishwa sana hata kuunganishwa na mitandao ya simu za mkononi.

***Maswali:***

1. Eleza namna benki inavyoweza kuchunga usalama wa fedha za mwekaji.
2. Taja mifano miwili ya faida mteja anazoweza kupata kutoka benki.
3. Toa mfano wa miradi mitano inayoweza kupelekwa kwenye benki na kupewa mkopo.
4. Jadili jinsi benki inavyoimarisha uchumi na maendeleo ya wananchi.
5. Jadili kuhusu manufaa ya kuunganisha huduma za benki na mitandao ya simu ya mkono.

***Zoezi la 10: Andika maneno kumi yanayohusiana na benki.***

## 1.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

***Zoezi la 11: Jadili kuhusu mambo yafuatayo:***

1. Huduma zinazotolewa na benki kwa wateja wake.
2. Benki ni njia nzuri ya kusaidia watu kujitajirisha.

## 1.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu cha Habari

***Zoezi la 12: Tunga kifungu cha habari chenye aya nne kuhusu mada ifuatayo:***

"Benki ni Taasisi Muhimu katika Kuinua Uchumi wa Wananchi"

## SOMO LA 2: MANUFAA YA BENKI

***Zoezi la 1:***
***Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali ya hapo chini***




***Maswali***

1. Elezea kuhusu wahusika unaowatazama kwenye mchoro hapo juu.
2. Kwa maoni yako, watu hao wanaenda wapi?
3. Unafikiri kuwa wanatarajia mambo gani katika safari yao?

### 2.1. Kusoma na Ufahamu: Manufaa ya Benki

*Soma kifungu cha habari kuhusu Manufaa ya benki, kisha jibu maswali yaliyopendekezwa hapo chini.*

Kila mtu hulenga kufanya shughuli zinazomwezesha kupata faida kwa ajili ya kuboresha maisha yake.

Wale ambao hawana uwezo wa kutosha hufanya juu chini ili waweze kupata fursa ya kuongeza pato lao, wengine huamua kuendea matawi ya benki na kupeleka maombi yao ya mikopo ili waweze kutatua shida zao baada ya kuwa wamepanga mipango ya miradi ya maendeleo.

Bwana Gakire na jirani yake Izere, ni wanachama wa ushirika mdogo unaohusika na kila mwanachama kuchangia fedha kidogo kila wiki. Kutokana na fedha hizi walizochanga, kila mshiriki anayetaka pesa huruhusiwa kuomba mkopo wa faranga chache anazohitaji na kuzirudisha kidogo kidogo kila wiki pamoja na riba ndogo sana. Baada ya miezi sita, washiriki wote hugawana pesa na kila mshiriki akapata mgawo wake pamoja na faida yake kulingana na akiba aliyokuwa nayo.

Siku moja washiriki walikutana kama kawaida kwa kuendesha shughuli zao. Bwana Gakire alikuwepo pamoja na jirani yake Izere. Walipokuwa wakiendesha shughuli za ushirika wao, bwana Gakire alitambua kuwa migawo iliyokuwa ikitolewa ilikuwa haiwezi kumsaidia kuyatatua matatizo ya kifedha aliyokuwa nayo nyumbani kwake. Yeye aliamua kwenda benki ili aweze kuomba pesa zinazoweza kutosha kumsaidia kutatua matatizo yake. Wazo hili alilifikiria wakati ambapo jirani yake Izere naye alikuwa na wazo hilo hilo. Walifikiria kuwa benki inaweza kuwapa mkopo wenye fedha nyingi na kuanzisha miradi mbalimbali ya kuleta faida.

Njiani, Gakire aliangalia nyuma yake kidogo akamuona Izere akitembea kwa mwendo wa haraka haraka. Gakire alipunguza hatua ili mwanamke huyo amfikie. Baada ya kusalimiana, walikaza mwendo na kuongea kuhusu mambo mbalimbali. Lakini, kila mmoja aliendelea kuwaza kuhusu miradi yake ambayo angeifanya baada ya kubahatika kupata mkopo kutoka benki yao. Walipofika benki, walipokelewa vyema, walipewa nafasi ya kukaa katika ukumbi wanapokaa wateja wengine kwa kungoja huduma mbalimbali. Waliwakuta wateja wa marika mbalimbali wakiwemo wakubwa kwa wadogo. Wakati uliwadia Gakire na Izere kupatiwa huduma. Waliingia mmoja baada ya mwingine katika ofisi ya mikopo ambapo kila mmoja alielezea jambo lililomfanya kwenda hapo kuomba mkopo. Afisa wa mikopo aliwatolea maelezo Zaidi kuhusu utoaji mikopo kama vile kuwa mteja wa benki husika, kuwa na akaunti hai, kuwa na dhamana ya mkopo unaoombwa, nakala za vitambulisho vya mwombaji, pamoja na barua ya maombi ya mkopo iliyoandikwa kwenda kwa meneja wa benki husika. Barua hiyo inapaswa pia kuambatanishwa pamoja na pendekezo la mradi unaokusudiwa kutekelezwa kutokana na mkopo huo. Aidha walielekezwa pia kuhusu muda wa kungojea kupewa mkopo toka baada ya kukamilisha maombi. Kwa kuzingatia maelezo hayo, Gakire na Izere walitambua kuwa nao wangetimiza vigezo vya kupewa mikopo yao. Lililobaki lilikuwa kumuandikia Meneja wa benki kwa minajili ya kupata pesa kisha kwenda kuanzisha miradi yao. Wao walikuwa wakitumia akaunti zao vizuri tangu miezi kumi iliyopita baada ya kufungua akaunti zao za hundi. Kila mara walipokuwa wakipokea faranga kutoka kwenye ushirika wao walikuwa wakizipeleka kwenye akaunti yao ya akiba katika benki hiyo. Kwa hivyo, walihesabiwa miongoni mwa wateja walioweza kuaminika na kupewa mikopo yao bila wasiwasi wowote. Hapo waliandika barua za kuomba mikopo.

Baada ya muda mfupi, benki ilikuwa imeisha tathmini faili zao na kuwaita ili kuwapa mikopo yao. Wao walitumia vyema pesa hizo na kufanikisha miradi yao wakapata faida kubwa. Gakire alijenga nyumba nzuri na kununua pikipiki aliyoipeleka mjini Kigali kwa ajili ya biashara ya kubeba abiria. Aliajiri dereva wa kuendesha pikikipi hiyo ambayo kila mwezi iliweza kuingiza pato la faranga laki moja. Izere naye alifungua duka la biashara la kuuza nguo zilizotengenezewa nchini na ambazo zilipendwa na wananchi wengi. Yeye alipata faida kubwa kiasi kwamba miezi mitano baadaye aliweza kujinunulia gari la kumsaidia kupeleka bidhaa zake katika sehemu mbalimbali nchini. Watu hawa walikuwa na tajiriba kubwa ya kupanga na kutekeleza miradi, wakatimiza ahadi zao za benki kwa kulipa vizuri mikopo waliyokuwa wameomba.

Miradi yao ilizaa matunda sana, wakaanza kuhesabiwa miongoni mwa matajiri wa hali ya juu. Hivyo wakawa mifano ya kuigwa katika nchi nzima. Siku hizi kila mwananchi ameisha kuelewa manufaa ya benki na nafasi ya ushirika mdogo mdogo unaosaidia jamii katika kuinua maisha na kutatua shida ndogo ndogo zinazojitokeza katika maisha yao. Kila mtu aliye na nia ya kubadilisha maisha kuwa mazuri, sharti ajiunge na benki na aanze kuhifadhi pesa zozote anazoweza kupata kutokana na shughuli zake ndogo ndogo. Hii itampatia uzoefu wa kutumia vizuri pesa alizonazo.

**Maswali ya Ufahamu**

1. Nini kilichosababisha Gakire na Izere kwenda benki?
2. Toa masharti muhimu yaliyoweza kumfanya mtu apewe mkopo kutoka benki.
3. Kwa nini Gakire na Izere walibaini kuwa walikuwa wametimiza vigezo vya kupewa mkopo mara tu baada ya kuelewa maelezo ya Afisa wa Mikopo?
4. Gakire na Izere walikuwa na akaunti gani?
5. Eleza ikiwa maombi yao yalikubaliwa na benki.
6. Gakire na Izere walikuwa na miradi gani?
7. Kwa sababu gani Gakire na Izere walihesabiwa miongoni mwa watu wenye kuaminika?
8. Unafikiri kuwa chanzo cha utajiri wa Gakire na Izere kilikuwa kipi?
9. Kulingana na kifungu ulichokisoma, onyesha nafasi ya vyama vya ushirika na mashirika madogo madogo kwa maendelo ya wanajamii.
10. Ni funzo gani unalolipata kutokana na kifungu cha habari ulichokisoma?

## 2.2. Msamiati kuhusu Manufaa ya Benki

***Zoezi la 2: Eleza maana za maneno yafuatayo yaliyotumiwa katika kifungu hapo juu***

1. Manufaa
2. Mchango
3. Mgawo
4. Kusuluhisha
5. Mshiriki
6. Dhamana
7. Kutimiza ahadi
8. Mashuhuri
9. Tajiri
10. Kuhimiza

***Zoezi la 3: Tumia maneno yafuatayo katika sentensi zenye maana kamili.***

1. kutosha
2. wakubwa kwa wadogo
3. fungu
4. Kujiepusha
5. Kugundua
6. shirika
7. kutatua
8. marafiki
10. kukaza mwendo

***Zoezi la 4: Soma sentensi zifuatazo kwa makini kisha ujaze mapengo yaliyoachiliwa wazi kwa kutumia maneno yafuatayo: mgawo, walipatiwa, kubahatika, walipokewa, marika, afisa wa mikopo, wateja, benki, pato, faida, ukumbi, zilizotengenezwa.***

1. Benki inapokea watu wa…………………………. mbalimbali.
2. Gakire na Izere ………………………na benki huduma nzuri.
3. Walipofika kwenye benki……………………vyema na afisa wa huduma kwa wateja wa benki.
4. Katika shirika dogo dogo, baada ya miezi sita kila mshiriki hupewa ……………wake.
5. ………………… ndiye mmojawapo wanaochunguza dhamana za wateja wanaoomba mikopo.
6. Wateja wanapokelewa katika ………………. wa benki.
7. Nguo zinazopendwa na watu wengi, ni zile …………… nchini Rwanda.
8. Hakuweza kutatua matatizo yake yote kwa sababu ya ………dogo.
9. Mtu akitumia vizuri mkopo kutoka benki, hupata …………….
10. …………………..huwasaidia wateja wake kujitajirisha.

***Zoezi la 5: Husisha maneno kutoka sehemu A na maana zake katika sehemu B.***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Hundi | a. Bila hangaiko la moyo |
| 2. Meneja | b. Makadirio ya mapato na matumizi |
| 3. Bajeti | c. Kikaratasi maalum cha kuchukulia au kuwekea pesa benki |
| 4. Riba | d. Kwenda mbio |
| 5. Kukaza mwendo | e. Mwenye madaraka ya kusimamia na kuongoza shirika au kampuni |
| 6. Mteja | f. Shughuli au biashara fulani inayomwingizia mtu kipato. |
| 7. Bila wasiwasi | g. Fedha zipatikanazo kwa makubaliano ya kuzirudisha pamoja na riba |
| 8. Mradi | h . Faida anayopata mtu aliyekopesha watu fedha ambayo ni ziada ya fedha aliyokopeshwa |
| 9. Mkopo | i. Mtu anayekwenda kununua au kuhudumiwa |

***Zoezi la 6: Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo: Benki, fedha, manufaa, afisa wa huduma kwa ateja, meneja, faida, barua, muda, pikipiki, biashara.***

1. Kufanya…………….hutajirisha watu.
2. …………….inawapatia wateja mikopo.
3. Alinunua ………………… mwaka jana.
4. Alimwandikia ……………..ya kuomba mkopo.
5. Alipokelewa vizuri na……………….
6. Wanafanya biashara kwa minajili ya kupata……………..
7. …………………..za benki huchungwa kwa makini.
8. …………………..ya benki kwa wateja ni mengi.
9. …………………ni kiongozi mkuu wa benki.
10. Mteja anapewa mkopo katika ………..mfupi.

## 2.3 Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi

***Zoezi la 7: Onyesha viini/mizizi na viambishi vinavyounda vitenzi vilivyotumiwa katika sentensi hapo chini:***

Kwa mfano : Mteja anaendа benki.

**Jibu: a-na-end-a**

**a-:**kiambishi awali cha nafsi

-**na-:**kiambishi kati cha wakati ama njeo

**-end-**:mzizi wa kitenzi

**-a:kiambishi tamati , kimalizio ama mwisho wa kitenzi.**

### *Eleza viambishi vinavyounda vitenzi vifuatavyo:*

1. Watoto hawa **wanapendana** sana.
2. Ukifanya makosa **utapigwa.**
3. **Alisimamisha** akaunti yake.
4. Mwalimu **alisomea** kitabu darasani.
5. Meza yake **imevunjika.**

***Zoezi la 8: Tunga sentensi tano kwa kutumia kitenzi 'kusoma' katika kauli zifuatazo:***

1. kutendesha
2. Kutendea
3. Kutendeka
4. Kutendwa
5. Kutendana

## 2.4. Matumizi ya lugha: Manufaa ya benki

***Zoezi la 9: Soma maelezo muhimu yafuatayo kisha, ujibu maswali hapo chini.***

## Maelezo Muhimu

Benki ni taasisi au shirika la fedha linalohifadhi na kukopesha fedha. Benki ina manufaa kwa njia mbalimbali. Kwanza, ina manufaa kwa mwekaji kwa kuwa inahifadhi pesa zake kwa usalama na kuziboresha riba ama faida. Benki inaweza kumkopa fedha kisha akatekeleza miradi tofauti ya kujitajirisha kama ya kilimo na ufugaji, ujengaji nyumba za kukodisha na nyinginezo, ufanyaji biashara, ununuaji vyombo vya kusafiria, n.k. Inamsaidia mwekaji kutosafiri na fedha chungu nzima mfukoni, inamsaidia kutatua matatizo kama kulipa deni fulani, kuhamisha pesa kutoka kwa benki moja hadi nyingine, kutumia simu ya mkononi akitoa pesa kwa kupitia njia ya kiteknolojia hata kutumia muda mfupi katika shughuli zihusuzo benki.

Kwa upande mwingine, benki ina manufaa kwa watu wote kwani benki inatambulikana kama msingi wa maisha ya ufanyaji biashara. Ni uhai na damu ya kazi yoyote inayozalishwa faida. Ni mojawapo ya njia rahisi za kujitajirisha ikiwa mteja anajiunga nayo, akafuata taratibu zake na kutekeleza miradi yake kwa makini, inamsaidia kutimiza ndoto zake.

Benki kama idara nyingine inahitaji watumishi mbalimbali kulingana na majukumu yao. Inawaajiri watumishi wake. Kwa hiyo watu hao hupewa mishahara na kuwa na maisha mazuri. Wafanyakazi wengine ambao si wa benki wanapokea mishahara yao kupitia benki na hawa wana haki ya kuomba mikopo. Aidha, husaidia wanaotaka kuanza kujiajiri kwa kufungua miradi ya maendeleo.

Benki inahitaji vifaa vya aina mbalimbali ili iweze kuhudumia wateja ipasavyo. Jambo hilo linaifanya benki kuvinunua vifaa hivyo kutoka kwa wafanyabiashara. Hivyo wafanyabiashara nao wanapata pesa kutoka benki. Kila mtu yeyote anayehitaji kuongeza pato lake inamlazimu kujiunga na benki.

### *Maswali*

1. Eleza manufaa ya benki kwa mwekaji pesa.
2. Jadili sababu watu hufananisha benki na uhai au damu ya biashara.
3. Onyesha miradi inayoweza kupewa mikopo na benki kwa urahisi.
4. Dhihirisha huduma mbalimbali za benki kwa wateja wake.

## 2.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

***Zoezi la 10: Kwa kushirikiana na wenzako, jadili mambo yafuatayo:***

1. Kujiunga na benki humaanisha kutajirika.
2. Faida za kuwa na akaunti katika benki.

## 2.6. Utungaji: Utungaji wa Kifungu cha Habari

***Zoezi la 11: Tunga aya tatu kwa kuchagua mojawapo ya mada zifuatazo:***

1. Nafasi ya benki kwa kuimarisha usawa wa kijinsia nchini .
2. Umuhimu wa mikopo ya benki kwa wateja wake.

## SOMO LA 3: AINA ZA BENKI

***Zoezi la 1: Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuatia hapo chini.***




***Maswali***

1. Eleza shughuli za watu ambao unawatazama kwenye mchoro hapo juu.
2. Toa maoni yako kwa kutofautisha matumizi na malengo ya majengo unayoyatazama kwenye mchoro huu.

### 3.1. Kusoma na Ufahamu: Benki Nchini Rwanda

*Soma kifungu cha habari kuhusu "Benki nchini Rwanda, kisha jibu maswali uliyopewa hapo chini.*

Zamani za kale watu walikuwa na namna tofauti za kuhifadhi pesa zao kwa kulinda usalama wake na kuzitunza vyema. Kuna wale waliotumia mbinu za kuziweka pesa katika pembe za ng'ombe, chini ya kitanda, ndani ya magodoro, katika mashimo, katika makasha ya miti na penginepo.

Siku hizi, mambo yameishabadilika. Watu wameishajua hatari za kuhifadhi pesa zao katika mahali pasipo na usalama. Serikali ya Rwanda ilianzisha mikakati ya

kuwahimiza wananchi wake kujiunga na benki mbalimbali kwa kufungua akaunti na kushirikiana nazo. Kulingana na malengo ya kila anayefungua akaunti, kuna wale wanaofungua akaunti za hundi, akaunti za akiba, na akaunti za amana katika benki nyingi zilizopo nchini. Kutokana na hali hiyo, idadi ya benki zilizomo nchini imeongezeka sana hata vijijini.

Nchini Rwanda, kuna benki mbalimbali na zenye majukumu tofauti. Benki Kuu ya Taifa huchunguza na kukagua matumizi yote ya fedha nchini na kutunga sheria zinazohusu fedha na matumizi yake. Benki za kibiashara nazo hushughulikia kuhifadha pesa za wateja, kutoa huduma ya kuhamisha fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine ndani ya benki moja au kwa benki tofauti, na kutoa mikopo yenye riba kulingana na sheria za kila aina ya mkopo ulioombwa. Mara nyingi wateja wa benki hizi ni wafanyabiashara na wafanyakazi wanaopitishia mishahara yao katika benki hizo.

Kuna aina nyingine za benki kama mfano wa Benki ya Dunia ambayo ni taasisi ya kimataifa yenye shabaha ya kusaidia maendeleo ya nchi za Dunia. Hii,si benki ya kawaida. Benki hii inashirikiana na Umoja wa Mataifa na hasa Shirika la Kifedha la Kimataifa lakini si chini ya Umoja wa Kimataifa. Ni mali ya wanachama 185 ambao huwa wanapiga kura kufanya uamuzi wowote. Makao makuu ya benki hii yapo Washington DC, nchini Marekani. Kuna Benki ya Maendeleo ya Afrika AfBD nayo husaidia nchi za Kiafrika katika maendeleo. Wanachama ni nchi kutoka bara la Afrika.

Wananchi wote wakubwa kwa wadogo bila kujali iwapo wana ulemavu wanahimizwa kujiunga na benki wakawa na akaunti zao. Akaunti hizi watazitumia katika shughuli zao mbalimbali za kimaendeleo.

***Maswali ya ufahamu***

1. Eleza namna wananchi walivyokuwa wakihifadhi pesa zao wakati wa kale.
2. Siku hizi wananchi wanahifadhi fedha zao wapi?
3. Eleza umuhimu wa benki kwa wananchi.
4. Andika aina za benki zinazozungumziwa katika kifungu cha habari cha hapo juu.
5. Ni watu gani wanaoruhusiwa kujiunga na benki?
6. Benki ina nafasi gani kwa kuimarisha uchumi na maendeleo ya wananchi?
7. Toa mifano ya aina za akaunti zinazofunguliwa na wateja katika benki.
8. Benki ya taifa ina wajibu gani?
9. Eleza huduma zinazotolewa na benki ya biashara.
10. Benki ya Dunia ina wajibu gani.

## 3.2. Msamiati wa Msingi

***Zoezi la 2: Tunga sentensi zenye maana kamili kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. kujiunga na benki
2. akaunti
3. benki za kibiashara
4. shirika la fedha
5. maendeleo
6. kuhifadhi
7. kuhimiza
8. Kufungua akaunti
9. Mfanyabiashara
10. kulipa deni

## 3.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi

***Zoezi la 3: Fanya zoezi lifuatalo kwa kukamilisha sentensi ukitumia mnyambuliko wa vitenzi katika kauli/hali kutendwa , kutendeka na kutendea.***

1. Wanafunzi……………..mtihani wa Kiswahili darasani. (fanya katika hali ya kutendea)
2. Nyumba yake ……………..vizuri. (jenga katika hali ya kutendeka)
3. Shamba la mama…………….... mwaka jana. (lima katika kauli ya kutendwa)
4. Kitabu hiki………………….. na walimu wa Kiswahili. (andika katika hali ya kutendwa)
5. Kiswahili ni mojawapo ya lugha ………... katika shule za sekondari nchini Rwanda. (kufundisha katika kauli ya kutendwa)
6. Mzazi ……….. karo mtoto wake. (kulipa katika hali ya kutendea)
7. Wali huu………..vizuri. (kupika katika hali ya kutendeka).
8. Mvua kali………….. wachezaji. (kunyesha katika hali ya kutendea)
9. Kazi hii……..  kwa uangalifu. (kufanya katika kauli ya kutendwa)
10. Shamba lile………...kwa urahisi. (kulima katika kauli ya kutendeka)

## 3.4. Matumizi ya Lugha: Aina za Benki

***Zoezi la 4: Soma maelezo kwa makini ili uweze kujibu maswali hapo chini.***

## Maelezo Muhimu

Benki ni taasisi inayoshughulikia pesa kwa kuhifadhi na kukopesha pesa wateja wake.

Kuna aina mbalimbali za benki kama vile mfano wa Benki ya Taifa ambayo ni benki kuu nchini inayochunguza na kupanga sheria za kifedha nchini. Kuna benki za biashara ambazo hutoa mikopo kwa watu ikiwemo wafanyabiashara. Hufanya hivi ili kuwasaidia wajiendeleze katika nyanja za kiuchumi na kijamii. Kuna tena vyama vya kifedha na mashirika ya kifedha ambayo husaidia watu kujiepusha na umaskini.

Kuna benki zisizo za kawaida kama vile BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA (AFDB ) ambayo majukumu yake ni kuwasaidia wanachama kujiendeleza kiuchumi.

Kuna BENKI YA DUNIA: Benki hii ni taasisi ya kimataifa yenye malengo ama shabaha ya kusaidia maendeleo ya nchi za dunia. Siyo benki ya kawaida. Hii inashirikiana na umoja wa kimataifa na hasa shirika la kifedha la kimataifa. Haifanyi kazi chini ya Umoja wa kimataifa bali ni mali ya wanachama 184 ambao ndio hupiga kura katika mikutano yake kulingana na thamani ya hisa zao katika rasilmali ya benki. Makao makuu yake yapo mjini Washngton DC nchini Marekani.

***Maswali***

1. Jadili kuhusu majukumu ya benki.
2. Benki ya taifa ina wajibu gani?
3. Eleza kuhusu Benki ya Maendeleo ya Afrika.
4. Jadili kuhusu shabaha za Benki ya Dunia.

***Zoezi la 5: Panga maneno unayopewa kwa kuunda sentensi zenye maana kamili.***

Mfano: Wanawake miradi ya inawatajirisha vizuri ikipangwa.

Miradi ya wanawake inawatajirisha ikipangwa vizuri.

1. Hizi wanapenda vijana kuzurura wa siku mjini.
2. Kiswahili kusoma sana tunapenda.
3. Kali uliangushwa mvua mti na.
4. Kote nchini unahitajika usafi.
5. Benki umuhimu sana zina maendeleo kuinua kwa.
6. Aina kuna mbalimbali benki za.

7. Rwanda mahali kuna nchini pakuvutia pengi.
8. Mtoto kila anapaswa shuleni kwenda.
9. Wangu walinifungulia katika wazazi akaunti benki.
10. Sana nyimbo zinafurahisha.

## 3.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

***Zoezi la 6: Jadili kuhusu mada ifuatayo:***

1. Umuhimu wa benki kwa jamii.
2. Nafasi ya Benki kupunguza uhaba wa ajira kwa vijana.

## 3.6 Kuandika: Utungaji wa Kifungu cha Habri

***Zoezi la 7: Tunga kifungu cha aya tatu kuhusu mada ifuatayo:***

"Nafasi ya benki katika kuimarisha uchumi vijijini."


# SOMO LA 4: WATUMISHI WA BENKI NA MAJUKUMU

***Zoezi la 1: Tazama mchoro ufuatao hapo chini kisha ujibu maswali husika.***


**Tazama mchoro ufuatao hapo chini kisha ujibu maswali husika.**




**1**




**2**




**3**




**4**




**5**

***Maswali***

1. Jadili kuhusu watumishi wa benki na majukumu yao.
2. Eleza vifaa vinavyotumiwa na watumishi wa benki.
3. Jadili kuhusu umuhimu wa ushirikiano wa watumishi wa benki kwa kutoa huduma vyema.

## 4.1. Kusoma na Ufahamu: Watumishi wa Benki na Majukumu yao

*Soma kifungu kifuatacho kuhusu watumishi wa benki na majukumu yao, halafu jibu maswali uliyoletewa hapo chini.*

Benki ni taasisi inayopaswa kuwa na watumishi mbalimbali kwa minajili ya kutimiza vizuri wajibu wake wa kutoa huduma za kifedha na kimaendeleo kwa wanajamii. Ili benki ifanikiwe kutoa huduma hizo, ni lazima watumishi wake wawe na ujuzi wa kiwango cha kutosha katika shughuli wanazofanya.

Benki huweza kuwa na matawi mbalimbali katika maeneo tofauti ya nchi ambapo kila tawi linasimamiwa na kiongozi wa tawi na kusaidiwa na wafanyakazi wengine katika tawi hilo. Kwa hiyo, watumishi wa benki wamo katika viwango tofauti kulingana na huduma wanazozitoa. Kwanza kuna Meneja wa benki ambaye ndiye kiongozi mkuu wa tawi linalohusika. Kiongozi huyu huwa na majukumu ya kusimamia tawi fulani la benki hiyo na huripoti kwa mkuu wake wa kazi kwenye makao makuu ya benki ambayo nayo huongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa benki husika. Meneja wa tawi la benki huongoza wafanyakazi wote wa benki na kuchukua uamuzi unaofaa kuhusu masuala yanayojitokeza katika benki hiyo. Yeye ndiye hupiga sahihi na kuidhinisha mambo yote yanayotendeka katika benki hiyo kwa kuhakikisha kwamba huduma zote zimeendeshwa kwa njia inayostahili.

Pili, kuna wafanyakazi wengine muhimu na ambao humsaidia meneja wa benki katika kufanikisha shughuli za benki. Mhasibu wa benki ni mfanyakazi ambaye huhusika na uwekaji hesabu za pesa. Afisa wa mkopo naye huwajibika kwa kupokea faili za kuomba mikopo, kutathmini dhamana na kuchunguza mambo mengine yanayohusu mikopo hiyo kwa ushirikiano na meneja pamoja na wafanyakazi wengine wa benki yao. Keshia ni karani mtunza fedha anayeshughulikia upokeaji na ulipaji wa fedha kwa wateja wanaozihitaji kutoka katika akaunti zao. Mkaguzi wa mahesabu naye hukagua mapato na matumizi ya benki na kuchunguza kuwa sheria na taratibu zilizowekwa zimezingatiwa ipasavyo. Mfanyakazi mwingine ambaye huwasaidia watu wengi wanaokuja kuomba huduma kwenye benki ni afisa wa huduma kwa wateja. Huyu ni mfanyakazi ambaye majukumu yake makuu ni kupokea vyema watu wote wanaokuja katika benki na kuwaonyesha mahali ambapo wanaweza kupewa huduma wanazozihitaji.

Mwisho, ni lazima kuelewa kuwa kila benki au tawi la benki huwa na watumishi mbalimbali kulingana na aina ya benki inayohusika na hata wateja wanaoomba huduma katika benki hiyo. Watumishi huweza kuwa wengi au idadi yao kuongezeka ili kuweza kuhudumia wateja wao kwa njia inayofaa. Kwa mfano, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na hata Benki ya Taifa ya Rwanda huweza kuwa na wafanyakazi wengi mno kutokana na majukumu yao mapana. Ni lazima benki iwe na mipango mingi ya kuwavutia wateja wengi ili iweze kupata faida na kutoa mchango katika maendeleo ya jamii.

***Maswali ya Ufahamu***

1. Ni nani anayeongoza tawi la benki?
2. Taja wafanyakazi wengine wanaomsaidia kiongozi wa benki katika tawi lake.
3. Teknolojia inasaidia nini katika utoaji huduma benkini?
4. Eleza aina za benki zilizozungumziwa katika kifungu hiki.
5. Eleza mchango wa benki katika maendeleo ya wanajamii.
6. Kwa sababu gani afisa wa huduma kwa wateja ni mfanyakazi muhimu katika benki?
7. Watumishi wa benki wakifanya kazi yao vyema, wanatoa mchango wao katika maendeleo ya wanajamii. Jadili.

## 4.2. Msamiati kuhusu Watumishi wa Benki na Majukumu Yao

***Zoezi la 2: Jaza nafasi kwa kutumia maneno unayopewa: meneja, afisa wa huduma kwa wateja, Mhasibu, keshia, Kuhudumia wateja, Afisa wa mikopo, kufungua.***

1. …………………ndiye hupokea wateja wa benki mara ya kwanza.
2. Mtumishi mkuu katika benki huitwa…………………
3. ……………………. huchunguza mambo yahusuyo utoaji mikopo.
4. ………………. anaangalia namna makeshia wanafanya kazi.
5. ………………. anawahifadhia na kuwatolea pesa wateja.
6. ……………. vizuri huwafanya wateja kuipenda benki yako.
7. ……akaunti katika benki ni hatua ya kwanza kuwa mteja wa benki.

***Zoezi la 3 : Tunga sentensi kwa kutumia maneno uliyopewa hapo chini.***

1. majukumu
2. watumishi
3. wajibu
4. huduma
5. tawi
6. wanajamii
7. kuripoti
8. afisa wa huduma kwa wateja
9. kupiga sahihi

***Zoezi la 4: Zikamilishe sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo: Watimize, itafanikiwa, vitengo, kusimamia, mhasibu, zinatoa mchango.***

1. Ni lazima wafanyakazi wote ........................... vizuri wajibu wao.
2. Benki hupata ……………….. kwa kutoa huduma nzuri kwa wateja.
3. Watumishi wa idara yoyote wanajigawa katika …………………tofauti.
4. Kazi ya …………………inahusika na utunzaji wa hesabu za pesa.
5. Kiongozi wa benki ana majukumu ya ………… tawi la benki.
6. Benki ……………. katika maendeleo ya wanajamii.

## 4.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi

***Zoezi la 5: Tunga sentensi zenye maana kamili kwa kuzingatia matumizi ya hali au kauli ya kutendwa, hali yakinishi.***

**Mfono:** Kupenda

Jibu: Kandanda inapendwa na watu wengi.

1. Kucheza
2. Kusema
3. Kuzungumza
4. Kusafisha
5. Kufuma
6. Kuchoma

**Maelezo muhimu kuhusu mnyambuliko wa vitenzi**

- Mnyambuliko wa vitenzi ni tendo la kupachika viambishi kwenye mizizi kwa madhumuni ya kuunda kitenzi kipya na kupata maana nyingine. Kwa hiyo ni kuzalisha kauli mbalimbali za tendo.
    - Mfano: Hali ya kutendwa hapa tendo linatendwa yaani kiima kinafanyiwa tendo fulani.

      Kitabu kinasomwa.

- **Hali ya kutendewa:** Kiima kinatendewa tendo.
    - Meneja wa benki **aliandikiwa b**arua ya kuomba mkopo.

- **Hali ya kutendana**: Kulingana na kauli hii kitenzi huunganisha sehemu mbili katika utendaji wa tendo moja kwa kiasi sawa.
    - Mfano: Watu wote inawalazimu **kupendana**
- **Hali ya kufanyafanya**: Kuhusu kauli hii tendo hurudiwarudiwa.
    - Mfano: Si vizuri kupoteza wakati kwa **kuzururazurura.**
- Hali badilifu ya kinyume: Hali hii huyakanusha mambo.
    - Mfano: Akaunti ya mteja **inatumika** vizuri → Akaunti ya mteja **haitumiki** vizuri.
- **Hali ya kutendesha/kusababisha:** Katika hali hii hutia sababu ya kutendesha jambo fulani. Hutumia viambishi tamati kama –ish na esh-a, n.k.
    - Mfano: 1. Utajiri **unafurahisha.** 2. Timu yetu **inachezesha** wachezaji wazoefu.
- **Hali ya kutenda:** hapa hudhihirisha kuwa kiima hutenda jambo.
    - Mfano: Meneja wa benki **anazungumza** na wateja.
- **Hali ya kutendeka:** Hali hii hujitokeza kwa kuonyesha kuwa kitendo fulani kinafanyika katika njeo tofauti.
    - Mfano: Chakula hiki **kimepikika** vizuri.

***Zoezi la 6: Geuza vitenzi vilivyopigiwa mstari katika hali badilifu ya kinyume.***

<u>**Mfano:**</u> Mteja <u>alifunga</u> akaunti ya mteja.

<u>**Jibu:**</u> Meneja alifungua akaunti ya mteja

1. Kabla ya benki kujulikana, kuna watu <u>waliofukia</u> na kuhifadhi pesa zao.
2. Aliponunua nguo mpya <u>alizivaa</u> zilizozeeka.
3. Bwana <u>aliezeka</u> nyumba yake ili abadilishe paa lake.
4. Mwenye nyumba <u>anazibua</u> tundu linalopitia maji wakati wa mvua.

## 4.4. Matumizi ya lugha: Wafanyakazi Mbalimbali na Shughuli zao

***Zoezi la 7: Unganisha vifungu vya maneno katika sehemu A na vile vilivyomo katika sehemu B ili upate sentensi kamili.***

| SehemuA | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mteja alifungua akaunti | a) Wamo katika vitengo tofauti |
| 2. Watumishi wa benki | b) Hupitishia mishahara yao katika benki |
| 3. Meneja | c) Katika benki |
| 4. Benki | d) Huhifadhi na kukopesha fedha |
| 5. Wafanyakazi | e) Hupiga sahihi |
| 6. Asiyesikia la mkuu | f) Hutibu wagonjwa |
| 7. Pole pole | g) Hufua chuma |
| 8. Mhunzi | h) Hujenga nyumba |
| 9. Mwashi | i) Huvunjika guu |
| 10. Daktari | j) Ndio mwendo |

***Zoezi la 8: Panga maneno yafuatayo ili uunde sentensi sahihi.***

1. Ni mwenye nguvu simba mnyama.
2. Hayazoleki yakimwagika maji.
3. Zinazotengenezewa Izere nguo nchini anauza Rwanda.
4. Mtihani Kiswahili lini wa utafanya ?
5. Kuheshimu vizuri ni wote watu.
6. Wanawake wanaume na wanalingana mwetu nchini.
7. Kulipa kukopa harusi matanga.
8. Mwindaji mazingira anaharibu.
9. Mazoezi haya utafanya asubuhi kesho.
10. Katika Afrika kinatumiwa sana Mashariki ya Kiswahili.

## 4.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Mazungumzo kati ya Afisa wa Mikopo na Mteja

***Zoezi la 9: Tunga kifungu cha mazungumzo kati ya Afisa wa Mikopo na mteja.***

## 4.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu cha Habari

***Zoezi la 10: Tunga kifungu kuhusu huduma za benki uliyoitembelea na majukumu ya watumishi wake.***

# SOMO LA 5: KARATASI MAALUM ZINAZOTUMIWA KATIKA BENKI

***Zoezi la 1: Tazama mchoro hapo chini kisha utoe maoni yako kuhusu mchoro huo.***



## 5.1. Kusoma na ufahamu: Mazungumzo kati ya Meneja wa Benki na mteja.

*Soma mazungumzo yafuatayo kati ya "Meneja wa Benki na Mteja Wake", kisha jibu maswali yaliyopendekezwa katika ufahamu.*

Mteja: Hodi! Hodi!

Meneja: Karibuni! Kaeni hapa.

Mteja: Asante Meneja!

Meneja: Nikusaidie nini?

Mteja: Tafadhali Meneja! Nilikuwa na akaunti yangu katika benki yenu lakini leo haitumiki.

Meneja: Naam! Nambari ya akaunti yako ni ipi?

Mteja: Nambari ya akaunti yangu ni 000-44567-00.

Meneja: Ahaa! Ngoja nichunguze vizuri kwenye tarakilishi hii ili nijue tatizo lilikuwa lipi.

Ahhh! Mbona akaunti yako ilifungwa! Kulipita muda mrefu bila kuitumia. Ulikutana na matatizo gani?

Mteja: Ni kweli, ilifungwa? Nilikuwa nikipitishia mshahara wangu kwenye akaunti hii na kibarua changu kikaisha miezi kumi iliyopita. Sijui kama naweza kuitumia tena!

Meneja: Aah! Uamuzi mzuri sana huo! Je, ulikuwa ukitumia hundi?

Mteja: Hundi ni nini Meneja?

Meneja: Hundi ni kikaratasi maalum ambacho hutumiwa kuchukulia na kuwekea pesa benki. Kikaratasi hiki humrahisishia mteja kupata pesa wakati wowote bila usumbufu au kuidhinisha malipo ya mtu mwingine bila ulazima wa kwenda naye benki. Jambo hilo humrahisishia mwenye akaunti kutotembea na pesa mfukoni kwani huweza kwenda kuzichukua wakati wowote kwa kutumia kikaratasi hicho. Mwenye akaunti kwa mfano huweza kujaza hundi na kuisaini kisha akampa mtu anayetaka alipwe. Hundi hiyo ndiyo anayoiwasilisha benkini ili apewe faranga zake hata kama mwenye akaunti hayupo.

Mteja: Asante sana kwa maelezo hayo Meneja. Lakini mimi sikutumia kikaratasi hicho. Lakini nilikuwa na kadi ya benki na ilikuwa muhimu sana kwangu.

Meneja : Haya. Hundi nayo ni muhimu na wateja wengi hupenda kuitumia. Angalia hapa nikuonyeshe! Hii ni hundi. Unachofanya ni kujaza nafasi hizi zilizo wazi ili uweze kuitumia. Kama unamwandikia mtu hundi, unajaza jina lake hapa na kuweka sahihi baada ya kuhakikisha kwamba umeandika kwa usahihi kila kitu, yaani kiasi cha faranga unazompa na majina yake sahihi.

Mteja : Je, mambo hayo yanatosha ili mwenye kuandikiwa hundi apewe pesa?

Meneja: Hapana! Kwanza kama nilivyokueleza, mwenye kuandika hundi anajaza nafasi hii ya mbele ya karatasi kwa kuandika jina la anayestahili kulipwa pesa, kiasi cha faranga anazostahili kulipwa kwa maneno na tarakimu pamoja na tarehe ya kutoa idhini yake. Lakini, anayepokea hundi naye anapaswa kujaza sehemu ya nyuma ya karatasi hiyo kwa kuandika jina lake, nambari ya kitambulisho chake, mahali na tarehe ya kuchukua pesa hizo, kisha akaweka sahihi.

Mteja: Aa ! Aah ! Asanteni sana ! Maelezo hayo yananifurahisha sana na ninaona kwamba mara hii nami ninapaswa kuwa na hundi.

Meneja : Si hayo tu ! Kuna karatasi nyingine muhimu sana zitumiwazo katika benki kama stakabadhi au risiti, nayo hutumiwa kwa kuweka na kutoa pesa kwenye akaunti ya mteja. Karatasi hii nayo hujazwa kulingana na maandishi ya maelekezo yaliyowekwa. Unachofanya ni kuisoma tu kisha ukaandika kila jambo katika nafasi yake.

Mteja: Vizuri sana. Ninaona kuwa karatasi hiyo haina utata wowote. Lakini, kadi yangu nayo ilimaliza muda wake. Ninafikiri kwamba nitapewa nyingine kwani hata na nenosiri la kadi silikumbuki. Nilifurahia jinsi ilivyoweza kunisaidia kuchukua pesa kwenye akaunti yangu kupitia njia ya teknolojia wakati wowote bila kuingia ndani ya benki.

Meneja: Haya. Ngoja tuiamshe tena akaunti yako. Mengine tutazidi kukufafanulia. Ninafurahia jinsi unavyoyaelewa yote yanayotendeka katika benki yetu na huduma zote tunazotoa kwa wateja wetu. Haya! Kila kitu kipo tayari, akaunti yako unaweza kuitumia. Nenda umwone afisa wa huduma kwa wateja, akupe fomu za kujaza ili uweze kupewa hundi na kadi mpya.

Mteja: Asante sana meneja kwa kunihudumia vizuri sana.

Meneja: Karibu sana. Kwa heri ya kuonana!

Mteja: Kwa heri ya kuonana!

***Maswali ya Ufahamu***

1. Akaunti ya mteja ilikuwa na shida gani?
2. Hundi ina manufaa gani kwa mteja?
3. Ni mambo gani yanayopaswa kujazwa na mwenye hundi ili atoe idhini ya kuchukua faranga kutoka kwa akaunti yake?
4. Kadi ya benki ina umuhimu gani kwa mteja?
5. Eleza mambo yanayozingatiwa na mpokeaji hundi kabla ya kupeleka hundi kwa benki ili alipwe faranga?
6. Taja aina mbalimbali za karatasi zinazotumiwa katika benki na kueleza matumizi yake.
7. Kwa nini akaunti ya mteja ilifungwa.
8. Kwa nini mteja alifurahia huduma aliyopewa na meneja?
9. Je, tatizo la mteja liliweza kutatuliwa? Eleza.
10. Meneja alimwambia mteja afanye nini kabla ya kuondoka?

## 5.2. Msamiati kuhusu Kifungu cha Habari

***Zoezi la 2:Tunga sentensi kwa kutumia maneno hapo chini:***

1. Hundi
2. Kadi ya benki
3. Kufungua akaunti
4. Kufunga akaunti
5. Uamuzi mzuri
6. Kibarua
7. Mshahara
8. Stakabadhi
9. Nenosiri
10. Kupiga sahihi

***Zoezi la 3: Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze mapengo. Tumia maneno yafuatayo: wateja, kutoa, akaunti, kuinua, benki, kuomba, kujiunga, meneja, mhasibu, hundi.***

Baada ya kugundua kuwa ………………ina manufaa mengi kwa ……………uchumi na maendeleo ya wananchi aliamua ……………na benki wakamfungulia ………… ili naye awe na uwezo wa kupeleka pesa ama…………..pesa kwenye akaunti yake,kuwa na haki ya………..mikopo kama ……………..wengine wa benki. ………………..ndiye kiongozi mkuu wa benki. Katika benki, kulingana na madaraka …………..ni mtumishi wa daraja la pili.

……………………inajazwa wakati wa kutoa pesa benkini.

## 5.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi

***Zoezi la 4: Soma sentensi katika jedwali kisha ujibu maswali kwa kufuata mfano uliopewa kuhusu matumizi ya mnyambuliko wa vitenzi.***

| Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| Wanafunzi wote wanasoma Kiswahili. | Wanafunzi wote hawasomi kiswahili. |
| Watoto wanapigana. | Watoto hawapigani. |
| …………………………………… | Wazee hawashindani katika mbio zozote. |
| Hadithi ilisimuliwa na bibi yangu . | …………………………………… |
| ………………………………… | Mvua haijamnyeshea fulani. |
| Ng’ombe wanafugwa nchini kote. | …………………………………… |
| Mkulima yeyote anaboresha shamba kwa hali ya juu. | . …………………………………….. |

***Zoezi la 5:Jaza sentensi zifuatazo kwa kuchagua jibu sahihi.***

1. Wanyama wafugwao..............maji na chumvi. (wanapeana, wanapa, wanapewa.)
2. Mtoto wangu............................ nguo.(amenifulia, nanifulia, anafulia)
3. Kiti hiki ............................(kimevunjika, kivunjikapo, kinavunja)
4. Walipokutania njiani ........................ (walisalimia, walisalimika, walisalimiana)
5. Watu wengi wanahitaji..............kuliko kupenda. (kupendeza, kupendwa, kupendeka)
6. Mzazi ....................kalamu. (ameninunulia, ameninunuliwa, ameninunulika)
7. Walipoanza ....................kiswahili alikipenda sana. (kusoma, kusomea, kusomeka)
8. Mashabiki wa timu yetu......ushindi wa timu yetu. (wanafurahia, anafuraha, anafurahika.)
9. Mwalimu wetu..............na kila mwanafunzi.(anapendwa, anapendeka,

anapendewa)

10. Mgonjwa...........dawa. (haulizwi, anaulizwi, hakuulizwi)

anapendewa)

10. Mgonjwa.................dawa. (haulizwi, anaulizwi, hakuulizwi)

***Zoezi la 6:Tunga sentensi tatu tatu kwa kutumia mnyambuliko wa vitenzi katika hali ya:***

- kutendesha au kusababisha.
- kutendwa.

## 5.4. Matumizi ya Lugha: Katarasi Maalum Zinazotumika katika Benki

***Zoezi la 7:Tafuta maneno yanayohusiana na benki katika mraba huu***

**Kwa mfano: Pesa**

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | T | A | K | A | B | A | D | H | I | **P** |
| Y | O | T | E | K | A | D | I | A | H | **E** |
| M | T | E | J | A | N | A | O | T | I | **S** |
| K | A | L | O | U | K | B | P | A | L | **A** |
| N | N | E | F | N | A | N | I | A | A | O |
| B | A | M | O | T | B | E | N | K | I | Y |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| G | Y | K | I | I | N | I | H | U | S | U |
| T | A | R | A | K | I | L | I | S | H | I |
| K | U | T | A | M | B | U | A | A | N | O |
| T | U | M | I | K | A | V | I | Z | A | B |
| H | U | N | D | I | N | A | F | A | S | I |

## MAELEZO MUHIMU

Benki ni taasisi au shirika la kifedha linalohifadhi na kukopesha fedha wateja. Watu wanaohitaji kuendesha miradi ya kimaendeleo hupewa mikopo. Miradi hii ya kimaendeleo ni kama vile kufanya shughuli za kibiashara, kilimo na ufugaji, kununua magari ya kubeba abiria ama kubeba mizigo, kujenga nyumba na majumba ya kupangisha, na hata kuanzisha kampuni mbalimbali.

Kwa upande mwingine, benki inapaswa kuwa na watumishi wenye majukumu mbalimbali ambao wanatumia vifaa mbalimbali kwa kuhudumia wateja. Vifaa hivyo ni vya aina mbalimbali kama vile hundi, stakabadhi, kadi ya benki, n.k. Kataratasi hizi hutumiwa na wateja wa benki ili kupata huduma mbalimbali za benki.

***Zoezi la 8: Tunga kifungu cha aya tatu kwa mada ifuatayo :***

"Umuhimu wa nyaraka zinazotumiwa benki"

## 5.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

***Zoezi la 9: Jadili kuhusu mada ifuatayo:***

Umuhimu wa kutoa huduma nzuri kwa wateja benkini

## 5.6. Kuandika : Utungaji wa Kifungu cha Habari

***Zoezi la 10: Tunga kifungu chenye aya nne kwa kuonyesha*** *"Umuhimu wa kuwa na akaunti benkini"*

TATHMINI YA MADA YA 1

Andaa kifungu cha chenye kuzingatia mambo muhimu yanayofuata huku ukihakikisha kwamba umetumia vitenzi walau vitatu katika hali ya kurudiarudia au kufanyafanya.

1. Aina za benki nchini Rwanda na huduma zinazotolewa
2. Nyaraka maalum zinazotumiwa benki kutoa huduma
3. Watumishi wa benki na majukumu yao
4. Teknolojia inayotumiwa benki
5. Manufaa ya benki katika maisha ya wananchi

# MADA KUU YA 2:

## FASIHI KATIKA KISWAHILI

# MADA KUU YA 2: FASIHI KATIKA KISWAHILI

## MADA NDOGO: TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI.

**Ujuzi Upatikanao katika Mada:** Kuelewa tanzu tofauti za fasihi andishi ya Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani.


**Malengo ya Ujifunzaji:** Mwanafunzi amalizapo kusoma mada hii atakuwa na uwezo wa : Kutunga shairi dogo, kuigiza Tamthilia na kutambua umuhimu wake katika jamii,kusoma na kuelewa riwaya pamoja na hadithi fupi kwa kujenga tabia ya kukuza utamaduni, kulinganisha na kutofautisha tanzu za fasihi andishi kwa kuzingatia mtindo wa wahusika na tabia zao.

Kidokezo


1. Una ujuzi gani kuhusu fasihi andishi?
2. Eleza nafasi ya riwaya katika jamii husika.
3. Eleza tofauti kati ya riwaya na tanzu nyingine za fasihi andishi.
4. Jadili aina za riwaya unazozijua.
5. Eleza umuhimu wa shairi kwa kufundisha jamii.
6. Jadili jinsi mtunzi wa shairi hufaidika.
7. Eleza uhusiano kati ya riwaya, ushairi na tamthilia.
8. Jadili umuhimu wa tamthilia katika kukuza na kuhifadhi utamaduni.

## SOMO LA 6: HADITHI FUPI

***Zoezi la 1: Tazama kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yanayofuata hapo chini***




1



2



3



4

***Maswali:***

1. Eleza wanachofanya watu unaowaona kwenye mchoro.
2. Eleza umuhimu wa maelewano katika maendeleo ya jamii.

### 6.1 Kusoma na Ufahamu: Majuto ni mjukuu

*Soma habari inayofuata kuhusu "Majuto ni mjukuu" ili uweze kujibu maswali uliyopewa hapo chini.*

Kijiji cha Ubwiza ni kijiji cha watu ambao wanashirikiana katika shughuli za maendeleo ya kijiji chao. Katika kijiji cha ubwiza, palikuwepo mwanamume mmoja aliyeitwa Ndishoboye. Mtu huyo alikuwa tajiri wa kupindukia. Utajiri wake ulimfanya kujivuna na kuwakejeli majirani zake. Kila mwanakijiji alisikitishwa na tabia mbaya za Bwana Ndishoboye ambaye alikuwa hataki kushirikiana na wanakijiji wenzake katika shughuli za maendeleo ya kijiji chao.

Ndishoboye alikaa muda mrefu kijijini mwake na kuendeleza tabia zake zilizochukiwa sana na majirani zake. Ndishoboye alijulikana hata kwa wapita njia ambao wote walikuwa wanamfahamu. Hakuna mtu aliyewahi kuingia kwake bila mwaliko wake. Mkewe alikuwa akisumbuliwa naye kila siku. Nyumbani kwake hapakuwa na amani na utulivu kama uliowatambulisha wakazi wa kijiji chake. Mkewe alikuwa amezoea kuvumilia maneno mabaya ya mume na alishinda siku zote nyumbani kwa kufanya kazi chungu nzima bila kusaidiwa na mtu yeyote. Badala ya kushukuriwa, alizoea kudharauliwa na kunyanyaswa bila sababu. Mume wake hakusita kamwe kumuambia chochote bila kumpa nafasi ya kutoa pendekezo lolote.

Ndishoboye alimwingilia mkewe katika kazi zote alizofanya. Kwa mfano, alihesabu kila pato lililoingia nyumbani kiasi kwamba alichukua hatua ya kumpimia mkewe chakula alichopaswa kuandaa kila siku. Nyumbani kwao walikuwa na mazoea ya kula chamchana na chajio. Haya yote yalikuwa yanajulikana kwa majirani zao ambao walimpenda sana Subira, mkewe Ndishoboye. Wote walifahamu kuwa Subira alikuwa mwanamke mwenye utulivu na aliyewajibika kwa kila kazi iliyomsubiri mpaka ikamalizika. Hali hii ndiyo ilikuwa imemfanya apate mavuno mengi kutokana na shughuli zake za kilimo. Hata kama wakati mwingine alikuwa ananyang'anywa mali yake na mumewe, mwanamke huyu alisifiwa kwa uwezo wake wa kifedha na majirani waliokuwa na shida walimwendea akawasaidia.

Siku moja, Bwana Ndishoboye alikuwa amepata pombe nyumbani kwake akaamua kuwaalika majirani zake. Badala yao kuja, wengi waliendelea na shughuli zao na kumjibu kuwa wangekuja siku nyingine. Majirani wawili ndio waliamua kwenda kuchunguza nini kilichomfanya awaalike siku ile. Kwani kwa muda mrefu waliokaa katika kijiji chao, hawakuweza kukanyaga katika nyumba ya jirani yao Ndishoboye. "Labda jirani yetu amebadilisha mienendo yake", majirani hao walifikiri.Walipofika nyumbani kwake, Ndishoboye aliwakaribisha akawaletea vinywaji wakaanza kufurahi. Lakini, la kuvunda halina ubani, Ndishoboye alikuwa na tabia ambazo hangeweza kuzibadilisha kwa muda mfupi kama huo. Baada ya majirani kuonja pombe aliyokuwa ameandaa kwa siku hiyo, alisimama na kuanza kuwaambia maneno ya kuwaudhi kwa kuonyesha maringo.

Yeye alianza kunena, "Nafurahia kwamba mmeitikia mwaliko wangu. Mnajua kwamba ndimi tajiri katika kijiji chetu, sasa nililotaka kuwajulisha ni kwamba utajiri haujileti wenyewe, lazima mwelewe kwamba mimi huwashinda nyote kufanya kazi. Nyinyi mnafikiria kuwa mnaweza kula vitu vya bure? Hii ndiyo sababu mara

nyingi ninawaona mkitamani vitu kutoka nyumbani kwangu.Tangu leo, sitaki yeyote anayethubutu kuingia hapa bila mimi kumwalika. Naomba na wale ambao hawakuja muwaambie kwamba mimi Ndishoboye sihitaji yeyote. Nina wafanyakazi wangu ambao wananitumikia kwa chochote!!"

Majirani hao walishikwa na bumbuwazi na kujiuliza kama maneno waliyoyasikia yalikuwa kweli. Hawakuamini macho yao. Wao waliamua kuanza kuondoka mmoja baada ya mwingine. Ndishoboye aliendelea kuwafokea mpaka wote wakatoka hapo.

Baada ya miezi miwili, wafanyakazi wa Ndishoboye walielemewa na kazi nyingi pamoja na ukatili wa Bwana Ndishoboye. Wote waliamua kwenda zao na kutafuta kazi kwa majirani wengine. Bwana Ndishoboye alianza kutambua kwamba mambo yalianza kwenda kombo kwake. Alikuwa hana watu wa kufokea na kudharau nyumbani kwake ila mkewe ambaye hakuacha kumuonya ajaribu kubadili tabia zake na mienendo yake ili aishi kwa amani na kila mtu. Miaka mitatu ilipopita, kwa Ndishoboye mambo yalikuwa yamebadilika. Nyumbani kwake hapakuwa na chochote. Ng'ombe aliokuwa nao walikufa kwa njaa, mmoja baada ya mwingine, kwani alishindwa kuwatafutia nyasi. Mashamba yake yaliyokuwa yamezoea kuota mazao mazuri na yenye kupendeza yalikosa rutuba na hayakuweza kutoa mazao kama ya zamani. Bwana Ndishoboye alianza kuona haya kila alipoenda, majirani wake wakaanza kumkejeli, Ndishoboye akageuka maskini kweli! Kitu cha thamani kilichobaki mikononi mwake kilikuwa ni gari moja tu ambalo hakutaka kuliuza kwa sababu ya tabia yake ya majivuno!

Siku moja, Bwana Ndishoboye alikwenda kumtembelea tajiri mmoja aliyekuwa akiishi mjini Kigali. Wakati alipokuwa anarudi kutoka Kigali, gari lake liliteleza na kuangukia katika mfereji ambapo alivunjika mguu na mkono. Katika kijiji chao cha Ubwiza, kulikuwa na jirani yake mwingine aitwaye Mugenzi ambaye naye alikuwa na gari jipya. Siku hiyo alikuwa akiendesha gari lake kutoka mjini Kigali alikozoea kwenda kwa shughuli zake za kibiashara. Alipofika hapo palipokuwa pametokea ajali ya gari la Ndishoboye, alimuona jirani yake akiwa mahututi ndani ya gari. Mara moja alisimamisha gari lake na kumpeleka hospitalini majeruhi.

Kwa kweli, majirani zake walikuwa watu wenye utu. Walipopata taarifa juu ya hali ya jirani yao Ndishoboye, hawakufikiria tabia na mienendo yake mibaya. Wengi walimtembelea kila jioni hospitalini.Hawakujali vitendo vyake viovu dhidi yao na dharau aliyokuwa nayo kwa muda mrefu, tangu anunue shamba katika kijiji hicho na kujijengea nyumba nzuri. Wao walimzuru na kumwuliza maendeleo yake. Wengi waliokwenda huko walimuona kama mtu wa kuhurumiwa kutokana na maumivu aliyokuwa nayo.

Wauguzi na madaktari walimsaidia sana kwenye hospitali hiyo alipolazwa mpaka alipopata nafuu na kurudi nyumbani.

Aliporudi nyumbani alianza kufikiria kuhusu jinsi alivyosaidiwa na majirani zake. Kila kitendo alichofanyiwa kilimchoma moyoni mwake mpaka akaamua kuanza maisha

mapya. Alimua kujenga urafiki na ushirikiano na majirani zake. Siku hiyo Ndishoboye alimuita mkewe ili waongee kuhusu matatizo yao. Wakati huo mkewe hakuogopa kumwambia ukweli wa mambo. Alikuwa ameshatambua kuwa mumewe angeweza kubadilika. "Ebu bwana yangu! Hujatambua kuwa ni wewe uliyesababisha hali hii katika familia yetu? Wewe uliamua kuvunja uhusiano na majirani zetu na hata wafanyakazi wote waende zao kutokana na dharau na kiburi chako dhidi yao! Huoni kuwa wewe ulikuwa chanzo cha matatizo yote ya nyumbani kwetu? Angalia vizuri, watoto wetu hawapati mahitaji ya shule, sisi sote hatuli chakula cha kutosha; mavazi yetu yameanza kuzeeka na hatuna uwezo wa kununua mengine. Mifugo wetu wamemalizika na mashamba yetu yamechakaa. Huoni kweli aibu kutokana na hali hii? Hakuna jirani anayeweza kukanyaga hapa na hata hawawezi kutusaidia kwa chochote. Fikiria, labda Mungu atatukumbuka siku nyingine kwani hajawahi kusahau watu wake!" Subira alimwelezea.

Bwana Ndishoboye aliyatafakari mawazo ya mkewe Subira, kisha akamwambia, "Mke wangu, ninaelewa vizuri hayo yote unayoyasema. Wahenga walisema, "Maji yakishamwagika hayazoleki." Acha tuuze nyumba yetu na mashamba yote ili twende kutafuta maisha mahali pengine. Ni hali ngumu kuendelea na maisha haya katika kijiji hiki. Mtu kwao hutuzwa! Sitaki kuvumilia aibu kama hii mahali ninapostahili kupewa heshima." Mkewe alikuwa ametambua kwamba mumewe alikuwa ameshaelewa athari za mienendo yake mibaya na kusema, " Sikiliza mume wangu, kule unakoita kuheshimiwa siyo heshima bali watu wote kijijini humu walikuogopa kutokana na dharau yako. Kila ulilosema walilichukia kiasi kwamba hawakupenda kuzungumza nawe wala kukujibu kwa lolote ulilosema. Kwa hiyo, kuhamia kwingine silo suluhisho mwafaka kwa maisha mema ya familia yetu. Jaribu kugeuza tabia zako na jizoeshe kushirikiana na kila mtu. Awe au asiwe tajiri, jaribu kumheshimu nawe utaheshimiwa."

Bwana Ndishoboye alilifikiria na kuwazia mengi aliyopaswa kufanya ili aweze kuonekana vizuri mbele ya majirani zake. Aliamua kwanza kumsogelea Mungu ili amuombe msamaha kwa dhambi zote alizofanya. Tangu siku hiyo, alianza kuingia kanisani ambapo alikumbuka kwamba alifika mara ya mwisho siku yake ya kufunga ndoa. Aliamua kukiri makosa na dhambi zake kwa kumuomba pia msamaha mke wake, majirani zake na wale waliowahi kuwa watumishi wake. Mbele ya mkewe, aliahidi kwamba angebadili mienendo yake na kuwa mtu mpya mbele ya kila mtu aliyeweza kukutana naye. Mkewe alifurahia uamuzi wa mumewe na akaona kuwa amegeuka mtu wa kuaminiwa. Siku iliyofuata, Subira aliamua kwenda benki na kuchukua fedha alizokuwa amehifadhi bila kumjulisha mumewe.

Yeye alikuwa amejifungulia akaunti ambapo alikuwa akiweka faranga kila alipovuna mazao yake, kiasi kwamba alikuwa na fedha za kutosha za kuanzisha miradi mikubwa. Alifikiri kuwa fedha hizo zingemfaa wakati wowote wa taabu.

Mumewe alipoona hayo, alianza kujuta sana kwa kumtendea ukatili mkewe. Yeye

na mkewe waliamua kununua tena mifugo ili wapate mbolea ya kutosha na kuanza upya maisha yao. Ili kufanikisha malengo yake na kufuta dalili zote za mienendo mibaya aliyoionyesha kwa majirani zake, Bwana Ndishoboye aliandaa vyakula na vinywaji akawaita majirani zake ili awaombe msamaha kwa kila jambo baya alilowatendea. Siku hiyo ilikuwa ya furaha kwake na familia yake pamoja na majirani zake. Aliwaahidi kwamba hangemtendea jambo baya lolote kila mtu aliyeweza kukutana naye.

Tangu wakati huo, yeye na familia yake huishi kwa amani na majirani zake humpenda sana. Ndishoboye hupata wakati kuwatembelea watu wa eneo alikotoka nao akawaomba msamaha. Alisamehewa na watu wote aliowaomba msamaha. Tangu wakati huo, aligeuka mtu mwema.

***Maswali ya Ufahamu***

1. Kwa sababu gani wanakijiji wote walisikitishwa na tabia za Ndishoboye?
2. Ndishoboye alikuwa anaishi katika kijiji kipi? Mke wake alikuwa nani?
3. Eleza tabia za mkewe Ndishoboye.
4. Ndishoboye alipowaalika wanakijiji, hawakuja, wengi walimjibu nini?
5. Eleza kilichowafanya waalikwa wa Ndishoboye kushikwa na bumbuwazi na kuondoka mmoja baada ya mwingine.
6. Onyesha uamuzi waliopata wafanyakazi wa Ndishoboye wakati walipoelemewa na ukatili wake.
7. Ndishoboye alipoishiwa na mali yake, alibaki na kitu kimoja. Je, kitu hicho ni kipi? Eleza sababu iliyomsababisha kutouza kitu hicho.
8. Dhihirisha alichokifanya Mugenzi wakati alipofika mahali ambapo Bwana Ndishoboye alipopatia ajali.
9. Eleza sababu iliyomfanya Ndishoboye kupendekeza kuhamia katika kijiji kingine.
10. Mwishoni, Ndishoboye alibadilika. Eleza aliyowaahidi wanakijiji ili kufuta dalili ya tabia zake mbaya.

## 6.2. Msamiati kuhusu Hadithi Fupi

***Zoezi la 2: Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno uliyopewa kulingana na matumizi yake katika hadithi uliyosoma hapo juu.***

1. Kudharau
2. Kunyanyasa
3. Pendekezo
4. Watu wenye utu
5. Kupata nafuu
6. Kuona haya
7. Alisamehewa
8. Uamuzi
9. Mtu mwema
10. Majirani

***Zoezi la 3: Husisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu ya B.***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Kuwajibika | a. Mazao yanayopatikana shambani |
| 2. Utulivu | b. Hali au uwezo wa kuvumilia |
| 3. Kilimo | c. Kuambia mtu maneno makali kwa hasira |
| 4. Mavuno | d. Mtu asiyekuwa na nguvu |
| 5. Bumbuwazi | e. Kutekeleza majukumu uliyonayo ipasavyo |
| 6. Kufokea | f. Hali ya kutokuwa na huruma |
| 7. kuelemewa | g. Hali ya kutoleta matata |
| 8. Ukatili | h. Hali ya kuwa kimya na kutojua la kufanya au kutosikia lisemwalo |
| 9. Subira | i. Kuwa na shughuli au kazi nyingi |
| 10. Mnyonge | j. Shughuli ya kulima |

***Zoezi la 4: Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia maneno yanayofaa kati ya haya yafuatayo: kushukuriwa, maumivu, msamaha, tajiri wa kupindukia, kujuta, maisha mapya, alisikitishwa, alihesabu, kumkejeli, aliandaa.***

1. …………analazimika kushiriki katika miradi mikubwa ya kuendeleza kijiji chake pamoja na nchi.
2. Mwanakijiji mmoja ………..na tabia za baadhi ya wanakijiji wasiokubali kushirikiana na wengine.
3. Mtu ambaye ana mwenendo mwema anastahili…………………..
4. Ndishoboye ………….. siku zilizopita bila kufanya jambo zuri akajuta.
5. Kama wewe ni tajiri, si vizuri ……….mtu ambaye hana uwezo wa kiuchumi.
6. Alipopata ……….jirani yake alimsaidia na kumpeleka hospitalini.
7. Walipoanza kushirikiana na wengine, walipata amani kisha wakaishi ………
8. Ili aendeleze amani na maadili katika kijiji chake, yeye …………. sikukuu nyumbani kwake.
9. Mume alipoona pesa zilizohifadhiwa na mke wake alianza………….. kwa sababu ya mambo mabaya aliyokuwa anayatenda kwa mke wake.
10. Ndishoboye aliomba ……….. , tangu wakati huo aligeuka mtu mwema kijijini.

## 6.3. Sarufi:Virai Nomino

***Zoezi la 5: Tazama sentensi hizi hapa chini kisha ujibu maswali yafuatayo:***

a. Maneno yanayopigiwa mistari ni ya aina gani?

b. Yanaitwaje katika muktadha wa kisarufi?

1. **Dada yangu** anaitwa Mutoni.
2. **Duka lake** linajaa vitabu.
3. **Mucyo na Mugabo** huwapokea wageni vizuri.

**Maana ya kirai**

Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye maneno zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina muundo wa kiima kiarifu. Muundo wa kiima kiarifu ni ule ambao unahusisha mtendaji wa tendo na tendo linalotendwa na ambao ndio muundo wa msingi katika lugha yoyote ile.

**Kwa mfano** :

- Mwanafunzi mwerevu
- Dereva mmoja
- Watoto wanene

Virai ni vya aina tofauti kulingana na neno kuu linalopatikana katika kundi la maneno linalounda kirai.

- **Chunguza maelezo yafuatayo kuhusu Kirai nomino (KN)**

Kirai Nomino ni kirai ambacho muundo wake umekitwa kwenye nomino; yaani nomino ndilo neno kuu linalotawala mahusiano kati ya nomino hiyo na maneno mengine katika kirai hicho.

***Mifano :***

1. **Maduka mengi ya vitabu** ni zao la miradi ya wasomi.
2. **Riwaya hii** ilipendwa na watu wengi.
3. **Mucyo na Mugabo** huuza vitabu.

- **Miundo ya virai nomino**

Muundo wa kirai nomino umejikita katika nomino au mahusiano ya nomino. Neno kuu linalotawala muundo huu ni nomino. Kirai nomino kinaweza kuundwa na:

**1. Nomino peke yake**

Mf:

- ***Mwalimu*** anafundisha.
- ***Usafi*** unahitajika.

2. Nomino mbili au Zaidi zilizounganishwa

***<u>Mf:</u> Wavulana na wasichana*** wanasomea darasani.

3. Nomino na kivumishi.

***<u>Mf :</u> Mfanyabiashara hodari*** amempatia mama bidhaa.

4. Nomino, kivumishi na kielezi.

***<u>Mf:</u> Mwanafunzi mwerevu sana*** amepewa zawadi

***Zoezi la 6: Pigia mstari kwenye kirai nomino katika sentensi zifuatazo:***

1. Duka kubwa linajaa vitabu.
2. Mtoto aliyetusimulia hadithi jana ameingia ukumbini.
3. Mimi na dada tulianza mazoezi ya kutunga riwaya.
4. Mucyo na Mugabo huwapokea wageni vizuri.
5. Adili na Nduguze ni riwaya iliyoandikwa na Shaaban Robert.
6. Watoto wengine wenye maadili mema wametutembelea.
7. Mgeni mpole amemtembelea rafiki yangu.
8. Mwenyekiti na katibu huongoza mdahalo.

## 6.4. Matumizi ya Lugha: Fani na Maudhui katika Hadithi Fupi

### 6.4.1 Mazoezi ya jumla

***Zoezi la 7: Tafuta katika mraba wa hapo chini maneno kumi yanayoweza kutumiwa katika hadithi fupi.***

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | B | I | O | M | U | U | N | D | O |
| A | A | M | A | W | A | Z | O | H | R |
| Z | B | A | N | A | O | U | V | I | O |
| I | A | R | A | N | A | R | E | H | D |
| N | H | A | I | D | H | I | L | I | H |
| G | A | R | G | I | S | I | A` | R | E |
| I | R | I | H | S | A | A | H | I | S |
| R | A | N | C | H | I | M | I | S | H |
| A | R | U | D | I | A | A | K | H | A |
| W | A | S | O | M | A | J | I | O | U |

***Zoezi la 8: Soma hadithi fupi " Pana nia pana njia". Chunguza mambo yafuatayo:***

1. Toa maana ya hadithi fupi.
2. Unaionaje fani ya hadithi ile?
3. Kwa kujiegemeza kwenye hadithi fupi uliyoisoma, eleza maana ya dhamira katika hadithi.
4. Tofautisha fani na maudhui.
5. Eleza dhima ya hadithi fupi katika jamii.

**Soma maelezo muhimu yafuatayo kisha ujibu maswali hapo chini.**

### Hadithi fupi

Hadithi fupi ni utungo wa kinathari ambao unazungumzia tukio moja kuu na unaosimulia kisa kinachomhusu mhusika mmoja au wahusika wachache sana na unazungumzia kipindi maalum kwa mtindo wa kibunifu. Utungo huu unajikita kwenye matendo ya binadamu na huweza kusomwa katika kikao kimoja.

### Fani katika Hadithi Fupi

Huu ni ufundi wa kisanaa atumiao msanii katika kutoa ujumbe wake kwa wasomaji wa hadithi yake. Fani ni sura ya nje ya hadithi fupi. Fani huwa na vipengele tofauti:

Vipengele vya fani:

- Wahusika
- Muundo
- Lugha
- Mtindo
- Mandhari
- Muda

### Wahusika

Wahusika ni watu, wanyama, vitu au viumbe wengine wanaopatikana katika hadithi fupi:

## Aina za wahusika

1. **Wahusika wakuu:** Mhusika mkuu ni mhusika mmoja au wawili ambao hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi fupi.

2. **Wahusika wadogo:** Ni aina ya wahusika muhimu sana ambao humsaidia mhusika mkuu kuipa hadithi mwelekeo wa kisanaa na kimaudhui.

### Tabia za wahusika

1. **Wahusika bapa:** Ni aina ya wahusika ambao hawabadiliki kitabia kutoka mwanzoni mpaka mwishoni mwa hadithi fupi.

2. **Wahusika duara:** Ni wahusika ambao wanabadilika kitabia kutokana na mabadiliko ya mazingira.

3. **Wahusika foili:** Ni wahusika wenye tabia zinazobadilika kinusu. Wako kati ya wahusika bapa na wahusika duara.

### Muundo:

Muundo ni namna msanii anavyopanga visa vyake au fikra zake katika hadithi fupi.

Muundo ni mtiririko wa matukio.

### Lugha:

Lugha ni kipengele muhimu katika uandishi wa kubuni. Fasihi ni sanaa ya lugha kwa hiyo jinsi lugha inavyotumiwa katika fasihi ni muhimu sana. Uchunguzi wa matumizi ya lugha unachunguza vipengele vifuatavyo: uteuzi wa msamiati ambao unahusu uchunguzi wa maneno na msamiati katika ujumla wake. Uchunguzi huu huangalia ikiwa maneno yaliyotumiwa yanafaa au hayafai na huchunguza pia ubunifu katika matumizi ya maneno. Tamathali za usemi na mbinu nyinginezo kama vile mbinu za kibalagha, usambamba, urudiaji, n.k.

### Mtindo

Mtindo ni namna ambavyo mwandishi huipa hadithi yake sura ya kifani na kimaudhui.

Mtindo ndio unaotofautisha wasanii. Katika mtindo tunachunguza sana matumizi ya lugha.

### Mandhari

Mandhari ni mazingira na mahali tukio la hadithi fupi lilipotokea. Kuna mandhari ya kubuni na mandhari ya kweli.

### Muda

Muda ni kipindi cha wakati kinachochukuliwa na hadithi nzima.

## Maudhui katika kazi ya fasihi

Maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumziwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo. Maudhui hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma mwandishi kuandika kazi ya fasihi. Maudhui huwa na vipengele vifuatavyo:

- Dhamira
- Migogoro
- Falsafa
- Ujumbe
- Msimamo wa msanii

### Dhamira

Dhamira ni wazo kuu linalojitokeza katika hadithi fupi. Dhamira hugawanyika katika makundi mawili. Kuna dhamira kuu na dhamira ndogo.

- **Dhamira kuu:** Wazo kuu lililomo katika hadithi fupi.
- **Dhamira ndogo:** Wazo dogo lililomo katika kazi ya fasihi.

### Falsafa

Kimsingi, falsafa ni elimu ya asili, busara au hekima. Katika hadithi fupi falsafa ya msanii hugusiwa kutokana na jinsi anavyoeleza matatizo ya jamii na jinsi anavyotoa suluhisho kwa namna ya busara, amani na utulivu.

### Migogoro

Migogoro ni hali ya kutokubaliana katika hadithi fupi.

### Ujumbe

Ujumbe ni mafunzo mbalimbali yanayopatikana katika hadithi fupi. Katika kazi ya fasihi, ujumbe wa msingi hubebwa na dhamira kuu, na dhamira ndogo hubeba ujumbe unaosaidia ujumbe wa msingi.

### Msimamo wa msanii

Mawazo, dhamira, mafunzo na falsafa huonyesha msimamo wa mwandishi kuhusu masuala mbalimbali. Msimamo wa msanii huonekana wakati anapoamua kufuata na kushikilia jambo fulani. Jambo hilo linaweza kukataliwa na wengine lakini akalishikilia tu.

## Sifa za hadithi fupi

- Huwa fupi
- Huwa na wahusika wachache
- Hurejelea wazo au kisa kimoja tu
- Huandikwa kwa lugha ya moja kwa moja
- Huwa na muundo rahisi kueleweka
- Hufanyika katika mandhari au mazingira moja tu au chache
- Huwa na sifa ya kubuniwa
- Huwa na mhusika mkuu mmoja anayejitokeza sana kuliko wengine katika hadithi
- Huwa na wazo moja lililopewa uzito kuliko jingine lolote.

### Dhima ya hadithi fupi

- Hadithi fupi huelimisha.
- Hadithi fupi huburudisha.
- Hadithi fupi huadhibu na hunasihi jamii. Kuna hadithi fupi ambazo hutungwa kwa madhumuni ya kuasa na kuadhibu juu ya mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii.
- Hadithi fupi hupiga vita kwa hali na mali mazingira yote ya ujinga, maradhi, njaa na umaskini.
- Kuna hadithi fupi ambazo husaidia katika kujenga misingi ya demokrasia miongoni mwa umma wa wakulima, wafugaji na wafanyakazi wengine.
- Hadithi fupi huwakosoa watu katika vipengele mbalimbali vya maisha yao.

***Zoezi la 9: Maswali:***

1. Fafanua maana ya hadithi fupi.
2. Maudhui ni nini katika hadithi fupi?
3. Tofautisha aina na tabia za wahusika.
4. Eleza sifa za hadithi fupi.
5. Dhihirisha dhima ya hadithi fupi katika jamii.

## 6.5 Kusikiliza na Kuzungumza

***Zoezi la 10: Kwa kushirikiana na wenzako, jadili kuhusu moja ya mada hizi:***

1. Umuhimu wa hadithi katika jamii.
2. Nafasi ya fasihi andishi katika kujikinga na magonjwa yanayoambukizwa.


## 6.6 Kuandika: Utungaji

***Zoezi la 11: Soma utangulizi wa hadithi fupi hapo chini kisha ikamilishe mpaka ifike mwishoni. Zingatia vipengele vya fani na maudhui pamoja na kichwa cha hadithi fupi.***

### Umoja ni Nguvu na Utengano ni Udhaifu

Familia ya Bwana Mugisha na Bibi Gasaro ilikuwa inaishi katika kijiji cha Terimbere. Familia hii ilikuwa na watoto wawili: Mugabo na Keza. Wao walikuwa wanaishi kwa amani na ushirikiano. Walikuwa wanashirikiana katika kazi zao za kila siku, jambo ambalo liliwasaidia kufanikiwa katika mifugo na mashamba yao makubwa yenye mazao mbalimbali. Wanakijiji wote walikuwa wanamuuliza Bibi Gasaro mbinu alizotumia pamoja na mumewe ili waweze kufanikiwa katika shughuli zote walizofanya.

# SOMO LA 7: USHAIRI KATIKA KISWAHILI



***Zoezi la 1: Chunguza kwa makini mchoro huu kisha ujibu maswali yafuatayo.***

1. Eleza kuhusu  mavazi ya vijana unaowaona kwenye mchoro. .
2. Eleza hali ya wazazi unaowaona kwenye mchoro hapo juu.

## 7.1. Kusoma na Ufahamu: Vaa vazi la Heshima

*Soma shairi lifuatalo ambalo liliandikwa na Said Karama kuhusu "Vaa Vazi la Heshima", kisha jibu maswali uliyopewa hapo chini.*

1. Kiumbe huwa ni mtu, aichungapo heshima,
   Vaa vazi la kiutu, uhifadhi wako wema,
   Hususa vijana wetu, ndio walo na lawama,
   Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

2. Wana leo hawajaali, hata vipi ukisema.
   Na kosa hawakubali, wafanyalo kuungama,
   Mi wapate badili, kuvaa mavazi mema,
   Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

3. Hasa wakiwa njiani, watu wanapowasema,
   Wala hawa hawaoni, maovu yao kukoma,
   Hawajali asilani, hata unapowazoma,
   Vaa vazi la heshima uchunge wako murua.

4. Utawaona vijana, nguo walizozipima,
   Kwanza huwa zawabana, na kuvua ni zahamu,
   Shingoni ukiwaona, mikufu imegandama,
   Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

5. Mikufu iko shingoni, manywele kichwa kizima,
   Ukija mikononi, bangili zimewakwama,
   Na mwao masikioni, vipuli viso gharama,
   Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

6. Kuna nao wasichana, na kesho ni kina mama,
   Wapendeleao sana, nywele zao kuzichoma,
   Na nyusi huwa hawana, kope machoni kuhama,
   Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

7. Pia huvaa mashati, na makoti kuazima,
   Marinda ni ya magoti, watupu wakiinama,
   Na kwenda kwenye umati, kuonya yao sinema,
   Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

8. Imekuwa ni ajabu, hebu tufikiri jama,
Kwao kufanya adabu, heshima ni ya kinyama,
Kwani nina jambo la aibu, huzidi kufanya hima.
Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

9. Na wote huo upuuzi, ni tokeo hizo zama,
Yote haya ni wazazi, kuwaonea huruma,
Ni shauri ya malezi, ya wao watu wazima,
Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

10. Tushike mwema wasia, unaotufaa umma,
Wazee walitwambia, wakati waliposema,
Ukicha mwana kulia, walia baba na mama,
Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

11. Wazazi nawashauri, mambo yataka kupima,
Tulee wana vizuri, wawe na tabia njema,
Walezi tutahadhari, tutimize yetu dhima,
Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.

12. Niyo niloandika, hapa nipo nasimama,
Patosha nilipofika, shairi natia tama,
Tuongozee Rabuka,wana wetu ya Karima,
Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua.
Said Karama, Nyota ya Ushairi (2013 uk. 45-47)

***Maswali ya Ufahamu***

1. Katika shairi ulilolisoma hapo juu, vijana wanashauriwa kufanya nini?
2. Eleza maana ya:
   a. "Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua".
   b. "Ukicha mwana kulia walia baba na mama".
3. Katika ubeti au kifungu cha mistari cha sita, msanii anatuelezea nini?
4. kutokana na kifungu ulichosoma, eleza maana ya "Kiumbe huwa ni watu, aichungapo heshima'.
5. Ni maadili gani yanayojitokeza katika shairi hili?
6. Kwa mujibu wa mshairi ni mavazi yapi ambayo hayafai kwa watu.
7. Kutokana na shairi hili, taja mambo yanayoweza kuaibisha mtu.
8. Eleza kuhusu sababu zilizomtia mshairi kutunga shairi hili.

## 7.2. Msamiati kuhusu Shairi

***Zoezi la 2: Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. Heshima
2. Vazi la heshima
3. Raha
4. Wasichana
5. Mtoto mzuri
6. Rabuka
7. Wazazi
8. Vijana
9. Kubana
10. Gharama

***Zoezi la 3: Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno unayopewa hapo chini:***

Rabuka, majirani, vijana, maungo wazi, heshima, mkononi, ungama, ushauri, nyuso, nguo.

1. Haifai kuvaa vazi lionyeshalo……………..
2. ………………wengi wa leo,wanavaa ovyo ovyo.
3. ……………….ndiye aliyeumba dunia na viumbe vyote.
4. …………….. wangu ni watu wema.
5. …………..haipiganiwi bali ni mtu hujiheshimu.
6. Kuna wasichana ambao wajikata…….. na kujipaka rangi.
7. Bangili huvaliwa………………..
8. Watu wengi hawapendi………… makosa yao.
9. Wazazi wanatoa…………kwa watoto wao.
10. Mtu yeyote lazima avae ……............... za heshima.

## 7.3 Sarufi : Virai Vitenzi

***Zoezi la 4: Chunguza kwa makini mifano ya sentensi zifuatazo, kisha ujibu maswali uliyopewa hapo chini :***

1. Mwanafunzi ***anafika shuleni.***
2. Baba namama ***wanashauri watoto.***
3. Vijana ***wavae nguo za heshima.***
4. Mwalimu na wanafunzi ***wanacheza mpira.***

***Maswali:***

1. Vifungu vya maneno yaliyopigiwa mstari vinaundwa na maneno mangapi (Bainisha idadi ya maneno kwa kila kifungu)?
2. Maneno mawili au zaidi ndiyo yanaunda fungu moja la maneno. Fungu hilo linaitwa namna gani?
3. Andika neno kuu katika kila fungu la maneno. Neno hilo ni la aina gani?

### Maelezo muhimu:

- Maneno yaliyopigiwa mstari katika zoezi la hapo juu huunda fungu la maneno au kipashio kimoja ambacho ni Kirai Kitenzi.
- Kirai kitenzi ni kirai ambacho kimekitwa katika kitenzi ambacho ndicho neno kuu kati ya maneno yote yanayounda fungu zima.

**Kwa mfano:**

1. Aliwaonea huruma
2. Anasimama hapa
3. Alivaa vizuri

**Miundo ya virai vitenzi**

1. Kitenzi pekee

**Kwa mfano:**

- Bangili zimewakwama.
- Mimi nimewashauri.

2. Kitenzi na kielezi

- Wao huvaa vizuri.

3. Kitenzi na nomino

- Wao huvaa mashati.

4. Kitenzi, nomino, kielezi

- Tulee wana vizuri.

5. Kitenzi, nomino, kivumishi na kielezi
   - Tufundishe watoto wetu vizuri.
6. Kitenzi, nomino, kivumishi na nomino
   - Baba mmoja alijengea mtoto wake nyumba

***Zoezi la 5: Pigia mstari kwenye virai vitenzi vinavyopatikana katika sentensi zifuatazo:***

1. Watu wale wanavaa mavazi mema.
2. Mzazi aliona vijana hao.
3. Wasichana wanavaa mikufu shingoni.
4. Wazazi wanalea watoto vizuri.
5. Rabuka anaongoza watu wote.
6. Wasichana wanapenda kuchoma nywele.
7. Mzee aliambia watoto neno muhimu.
8. Wanafunzi wanasoma Kiswahili
9. Dada yangu alitunga shairi zuri.
10. Baba na mama wanaenda sokoni.

## 7.4. Matumizi ya Lugha: Ushairi

***Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali***

**MAELEZO MUHIMU**

Ushairi ni eneo linalohusu kazi za kifasihi ambapo mtunzi hutumia maneno ya mkato na lugha yenye kuvutia na ambayo yamepangwa kwa urari wa mizani na vina maalum.

Kuna aina kuu tatu za ushairi: Mashairi, Ngonjera na Tenzi.

### Mashairi:

Shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalum na kutumia lugha ya mkato na mnato kwa kuelezea hisi na mawazo ya jamii husika na kuwasilisha ujumbe fulani. Mashairi hugawika katika makundi mawili: mashairi ya kimapokeo au mashairi arudhi na mashairi huru. Mashairi arudhi hutungwa kwa kufuata au kuzingatia

sheria na kanuni au kaida za utunzi kama vile kuzingatia vina, idadi fulani ya mizani, mishororo na vipande vya mishororo. Kulingana na idadi ya mishororo katika kila ubeti, mashairi huweza kugawika tena katika aina mbalimbali:

1. Tathmina ni shairi lenye mshororo mmoja kwa kila ubeti.
2. Tathnia ni shairi lenye mishororo miwili kwa kila ubeti.
3. Tathlitha ni shairi lenye mishororo mitatu kwa kila ubeti.
4. Tarbia ni shairi lenye mishoro minne kwa kila ubeti.
5. Takhmisa ni shairi lenye mishororo mitano kwa kila ubeti.
6. Tasdisa shairi lenye mishororo sita.

## Ngonjera:

Ngonjera ni shairi lenye malumbano na majibizano kati ya watu wawili au zaidi.

## Tenzi

Tenzi ni aina ya shairi ambalo ni mtungo mrefu wa kishairi unaoelezea historia au kisa fulani na ambao hauna vina vya kati katika mistari yake bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mstari wa mwisho wa ubeti.

Kuna mambo mengine muhimu kuhusu shairi. Mishororo ya shairi huwa na majina maalum.

Mwanzo huwa ni mshororo wa kwanza wa ubeti.

Mloto huwa ni mshororo wa pili wa ubeti.

Mlea huwa ni mshororo wa tatu wa ubeti.

Kituo huwa ni mshororo wa mwisho wa ubeti .

Kuna aina mbili za vituo ambazo ni kituo kimalizio na kituo kibwagizo. Kituo kimalizio ni kituo ambacho hakirudiwi mwishoni mwa kila ubeti katika shairi. Kituo kibwagizo ni kituo kinachorudiwarudiwa mwishoni mwa kila ubeti.

Vipande au sehemu za mishororo huitwa:

- ***Ukwapi:*** Ni kipande cha kwanza cha mshororo.
- ***Utao:*** Ni kipande cha pili cha mshororo.
- ***Mwandamizi:*** Ni kipande cha tatu cha mshororo.

***Zoezi la 6: Jibu maswali yafuatayo:***

1. Eleza maana ya mshorororo.
2. Fungu la mishororo huitwaje?
3. Shairi lenye mishororo mitano kwa kila ubeti huitwaje?
4. Mshororo unaorudiwarudiwa huitwaje?

***Zoezi la 7: Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali husika.***

**Mteja na Seremala**

**Mteja**

Kudanganywa nimechoka

Mara randa, mara shoka

Musumeno mevunjika

Huna ulilobakiza

**Seremala**

Kukusumbua sitaki

Kukuudhi siridhiki

Mbona wanitia dhiki

Kunisadiki hutaki

**Niyomugabo C. (2013). Mafunzo Kiswahili, Kidato cha tano.uk. 22**

***Maswali:***

1. Ngonjera ni nini?
2. Eleza tofauti kati ya ngonjera na shairi.
3. Jadili aina ya shairi hili.
4. Katika ubeti wa kwanza wa shairi hili wanatueleza nini?
5. Eleza wahusika wa shairi hili.

***Zoezi la 8: Tumia mishale kwa kuhusisha maneno kutoka katika sehemu ya A na maana zake katika sehemu ya B.***

| Neno | Maana |
|---|---|
| Shairi | Msitari mmoja wa ubeti. |
| vazi | Kifungu cha maneno katika shairi kilichokamilika. |
| Mshororo | Mtungo wa kisanaa wenye mpangilo maalum na kutumia lugha ya mkato na mnato kwa kuelezea hisi na mawazo ya jamii husika. |
| Mshairi | Mtunzi wa mashairi. |
| Ubeti | Shamrashamra. |
| Shangwe | Kitu kama nguo au ngozi kinachovaliwa. |
| Murua | Mwenye tabia njema. |
| Heshima | Mambo ayatendayo ili kuonyesha kwamba anathaminiwa. |
| Ajabu | Jambo la kushangaza. |
| Shauri | Mawaidha. |

## 7.5. Kuzungumza na kusikiliza: Majadiliano

***Zoezi la 9: Jadili mojawapo ya mada ulizopewa hapo chini.***

1. Ushairi ni chombo muhimu cha kukuza na kuhifadhi utamaduni wa jamii.
2. Kazi ya utunzi wa mashairi inamlazimu mtunzi kuwa na ujuzi wa kutosha katika fani hiyo na kuhusu matukio ya kijamii.

## 7.6 Utungaji: Utunzi wa Shairi

***Zoezi la 10: Tunga shairi lenye beti mbili kuhusu mapenzi***

# SOMO LA 8: UFAFANUZI WA RIWAYA

***Zoezi la 1: Tazama mchoro hapo chini kisha ujibu maswali.***




***Maswali:***

1. Unaona nini kwenye mchoro hapo juu?
2. Elezea kuhusu wahusika unowatazama kwenye mchoro huo."

## 8.1 Kusoma na Ufahamu : Muhtasari wa Riwaya ya Adili na Nduguze

*Soma muhtasari wa Riwaya ya "Adili na Nduguze" ambayo iliandikwa na Shaban Robert, kisha jibu maswali yaliyotolewa hapo chini.*

Siku moja, mfalme wa Ughaibu alipokuwa anachunguza malipo ya kodi ya nchi yake, aligundua kuwa kulikuwa na kasoro iliyotokana na kuwa Janibu ilichelewa kuleta kodi. Ikibali mshauri wa mfalme alitumwa Janibu kuona kilichosababisha kuchelewa huko.

Alipofika pale, Adili, kiongozi wa Janibu alimlaki vizuri na kumweleza kuwa kuchelewa huko kulitokana na kuwa walikuwa bado wakikusanya malipo hayo. Ikibali alishinda pale siku tatu.

Siku ya kwanza usiku, wakati ambapo alikuwa amelala chumbani pamoja na Adili, alimwona Adili akitoka nje na kiboko. Alimfuata na akamwona anawapiga manyani wawili. Jambo hilo lilikuwa haliruhusiwi Ughaibu kutokana na kuwa Mfalme Rai alikuwa anawapenda wanyama. Ikibali aliporudi Ughaibu alifikisha habari hiyo kwa mfalme Rai na yeye akaamua kumtuma Ikibali ili amfuate Adili na nyani wake.

Walipofika mbele ya mfalme, Adili alieleza sababu zilizomruhusu kuwatesa manyani wale. Kwanza alieleza kuwa manyani wale walikuwa ndugu zake. Baada ya kifo cha baba yao, wote watatu waligawana mali ya marehemu. Adili akafanya biashara nyumbani, nduguze wakaenda Ugenini kutajirika. Kilicho na mwanzo kina mwisho. Siku moja alipokuwa nyumbani aliwaona nduguze wanarudi wakiwa katika hali mbaya. Walimwelezea kuwa walikuwa wametajirika Ugenini lakini mwisho wao wakapata ajali ya jahazi lao na mali yao ikapotea.

Adili aliwalaki vizuri na kuwapa pole. Baadaye, Adili aligawa mali yake na kila ndugu yake akafungua duka na kutajirika zaidi. Walimwomba Adili kwenda pamoja na yeye akakubali. Walijipa jahazi wakasafiri wakipita huku na kule. Siku moja wakiwa ndani ya jahazi waliishiwa maji na jahazi hilo likatia nanga kwenye jabali.

Mabaharia walienda kutafuta maji. Adili alikutana na tandu aliyekuwa anakaribia kuuwawa na nyoka. Kwa kumwokoa tandu, Adili alimuua nyoka yule. Punde si punde tandu alijigeuza msichana na kumwambia Adili kuwa wema aliomtendea ungelipiwa baadaye. Baada ya kusema hayo akatoweka na kupotelea ndani ya ardhi. Adili alirudi chomboni na safari ikaendelea.

Kwa safari ya siku thelathini, jahazi lilikosa maji tena, na mabaharia wakapigwa na kiu. Walielekea Tanga kutafuta maji lakini wakakosa. Walipokuwa pale, Adili aliona ukuta mbali, akaamua kwenda pale lakini wengine hata ndugu zake wakakataa kumuunga mkono. Alienda yeye mwenyewe. Alipofika mjini aliona kuwa vitu vyote pale vilikuwa vimegeuka mawe. Ndani ya mji kulikuwepo msichana mrembo ambaye yeye hakugeuka jiwe. Jina lake ni Mwelekevu.

Mwelekevu alimwelezea Adili msiba ulioangukia mji na wananchi wa nchi ile. Adili alimchukua chomboni na tunu za majohari. Alipofika chomboni aligawa tunu zake lakini tendo hili liliwahuzunisha ndugu zake. Walimwomba Adili kumuoa msichana yule lakini Adili akakataa. Usiku alipolala walimtosa Adili baharini na wakamkabili msichana ili wamuoe. Msichana huyo alikataa akajitosa baharini.

Adili aliokolewa na ndege na kupelekwa katika nchi ya majini. Ndege yule alikuwa Huria, msichana aliyeokolewa na Adili wakati alipokuwa katika hatari ya nyoka. Pale Adili aliheshimiwa sana na wazazi wa Huria na wakampa hundi kama malipo ya wema wake.

Baada ya hayo kufanyika, Adili na Huria walitua chomboni. Kutokana na tendo baya walilomtendea, Huria aliwageuza manyani ndugu zake Adili. Akamlazimisha kuwapiga kila siku asingefanya kitendo hiki angepigwa yeye mwenyewe. Aliposikia hayo, Rai alitaka kumpatanisha Adili na nduguze ili watoke kwenye hali ya unyani,. Rai alimwandikia Huria barua kwa kuomba msaada wa kuwasamehe. Ili akutane

tena na Huria, Rai alimuomba Adili kurudi nyumbani na kutowapiga nyani wake.

Usiku alioacha kuwapiga nyani, Huria alijitokeza ili kumtesa Adili. Adili alimpa Huria barua ya Rai na yeye akaipeleka kwa baba yake Kisasi. Kisasi alikubali matakwa ya Rai na ndugu zake Adili wakawa watu tena. Asubuhi ndugu walienda Ughaibu kumuonyesha Rai kuwa kazi yake ilifaulu.

Rai aliwaomba ndugu zake Adili kutotenda maovu tena na wao wakakubali. Walisafiri pamoja kufika Janibu. Adili alimchukua Mwelekevu na kila ndugu yake akachukua binti mmoja wakafanya harusi siku moja.

*Kitabu cha Mafunzo ya Kiswahili, Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha Sita. Uk.6-8*

***Maswali ya ufahamu***

1. Taja wahusika tunaowakuta katika muhtasari wa riwaya ya Adili na Nduguze?
2. Nchini Ughaibu kulikuwepo kasoro. Kwa maoni yako, ni ipi sababu ya kasoro hii?
3. Eleza alichokuwa anafanya Adili kila usiku.
4. Ni shida gani waliyokumbwa nayo njiani nduguze Adili walipokuwa katika jahazi.
5. Dhihirisha alichokifanya Adili baada ya kulaani nduguze.
6. Jadili tendo alilowatendea Huria nduguze Adili.
7. Rai aliwaomba ndugu zake Adili kutotenda maovu. Husisha ushauri huu na maisha yako ya kila siku.
8. Eleza somo unalopata baada ya kusoma muhtasari wa Adili na Nduguze.

***Zoezi la 2: Baada ya kutoa maana ya maneno yafuatayo, yatumie katika sentensi zako binafsi.***

1. Kulaki
2. Malipo
3. Nyani
4. Marehemu
5. Jahazi
6. Jabali
7. Tandu
8. Kutoweka
9. Kupatanisha
10. Kutesa

***Zoezi la 3 : Husisha maneno katika sehemu A na sehemu B***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Ikibali | a. Kupotea machoni; kukosa kuonekana |
| 2. Kodi | b. Hali ya kutokuwa na raha |
| 3. Tabu | c. Mfanyakazi wa chombo cha baharini |
| 4. Baharia | d. Muamana wa kutenda jambo |
| 5. Kutoweka | e. Malipo kwa ajili ya kitu kilichochukuliwa au kupangwa na kutumiwa kwa muda. |

***Zoezi la 4: Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia nahau zifuatazo kutoka muhtasari wa riwaya "Adili na nduguze" : Punde si punde, kutia nanga, kupigwa na kiu.***

1. Nenda pale ambapo jahazi letu…………..
2. …………………..mgonjwa yule atapona.
3. Mtoto yule………………….. ndiyo maana anahitaji maji ya kunywa.

## 8.3. Sarufi : Vishazi

***Zoezi la 5: Tazama sentensi za hapo chini, kisha upige msitari sentensi zinazojitosheleza.***

1. Adili alipigwa kwa sababu ya huruma aliyoonea manyani.
2. Alipofika katika mji wa mawe, Adili alikutana na Mwelekevu.
3. Adili alikuwa na ndugu wawili walioitwa Hasidi na Mwivu.
4. Rai aliyekuwa mfalme wa ughaibu, alipendwa sana na wananchi.
5. Manyani waliposamehewa, waligeuka watu.

***Zoezi la 6: Soma maelezo muhimu kuhusu kishazi huru kisha ujibu maswali ya hapo chini.***

- ### Maana ya kishazi

Kishazi ni tungo inayotawaliwa na kitenzi. Kitenzi hicho kinaweza kuwa kinajitosheleza au hakijitoshelezi katika maana; hasa kishazi huwa ndani ya sentensi kuu.

Kile kinachojitosheleza kimaana, kinatoa taarifa kamili wakati kile ambacho hakijitoshelezi kimaana hakitoi taarifa kamili. Hivyo basi ni lazima kiambatane na kishazi kingine ndipo taarifa yake ikamilike.

## Kwa mfano:

1. ***Mwelekevu alimuelezea Adili msiba*** ulioangukia mji wa mawe.

Sentensi hii ina tungo mbili, kwenye tungo ya kwanza kuna kitenzi "alimuelezea" ambacho kinajitosheleza.

Kwenye tungo ya pili kuna kitenzi "ulioangukia" ambacho hakijitoshelezi kimaana.

2. ***Usiku alipoacha kupiga manyani,*** Huria alimtesa Adili.

Kwenye tungo ya kwanza kuna kitenzi "**alipoacha**" ambacho hakijitoshelezi.
Kwenye tungo ya pili kuna kitenzi "**alimtesa"** ambacho kinajitosheleza.

- ### Aina za vishazi

Vishazi hugawanyika katika makundi mawili yaani kishazi huru na kishazi tegemezi.

**a. Kishazi huru:** Kishazi huru ni tungo inayotawaliwa na kitenzi kinachojitosheleza kimaana. Yaani, ni tungo inayotawaliwa na kitenzi kinachotoa taarifa kamili. Ikumbukwe kuwa kishazi huwa hasa ndani ya sentensi kuu.

## Kwa mfano:

1. Rai aliyekuwa mfalme wa ughaibu, **alipendwa sana na wananchi.**
2. **Adili alipigwa** kwa sababu ya huruma aliyoonea nyani .
3. Alipofika katika mji wa mawe, **Adili alikutana na Mwelekevu.**

**b. Kishazi tegemezi:** Ni tungo inayotawaliwa na kitenzi ambacho hakijitoshelezi kimaana.

## Kwa mfano:

1. **Rai aliyekuwa mfalme wa ughaibu,** alipendwa sana na wananchi.
2. **Manyani waliposamehewa**, waligeuka watu.
3. **Adili alikuwa na ndugu** wawili **walioitwa Hasidi na Mwivu.**

***Maswali:***

1. Eleza dhana ya kishazi.
2. Je, kuna aina ngapi za vishazi ? zitaje.
3. Andika mifano mitano ya vishazi huru.

***Zoezi la 7: Tazama sentensi za hapo chini, kisha upige mstari kwenye vishazi huru.***

1. Wanyarwanda hufanya kila liwezekanalo ili wajikinge dhidi ya ukimwi.
2. Kila yeyote anayehifadhi mazingira,anatarajia kuishi maisha mazuri.
3. Elimu inakuza maendeleo ya nchi yanayohitajika.
4. Atakaye kuishi kwa amani, anaheshimu haki za wengine.
5. Anayekubali kosa, yeye husamehewa kwa amani.
6. Watu wa kijiji chetu ili waishi mahali safi, wao wanafanya kazi kwa bidii.
7. Tunaposomewa hadithi, tunajenga urafiki na ushirikiano.
8. Mtunzi anapotunga hadithi fupi, anapata fedha nyingi.
9. Alitajilika tena wakati aliposhirikiana na mkewe.
10. Ukitaka kutajirika, usiwe mzembe.

## 8.4. Matumizi ya Lugha: Sifa za Riwaya

Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa hapo chini:

**Maana ya riwaya**

Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni iliyoandikwa kwa maandishi ya nathari inayoeleza ukweli fulani wa maisha. Kazi hii ya riwaya, huhusisha watu binadamu,wanyama ama vitu vingine vinavyopewa uhai kama vile mizimu.

**Aina za Riwaya**

Kuna aina kadhaa za Riwaya katika Fasihi Andishi:

**Riwaya sahili** : ni aina ya riwaya ambayo visa vyake husimuliwa moja kwa moja na huwa rahisi kueleweka.

**Riwaya changamano**: hii ni riwaya ambayo huhitaji kusomwa kwa makini ili kueleweka.Aghalabu huwa na maudhui mengi na wahusika wengi ambao wanachangia katika tatizo kuu katika riwaya hiyo. Hujengwa kwa taharuki ili kuwavutia hadhira kutazamia jinsi tatizo kuu litakavyotatuliwa. Hutumia mbinu za taharuki na visengere nyuma/mbele.

**Fani na maudhui katika Riwaya**

## Fani

**Fani** katika riwaya huundwa na **wahusika, mtindo, muundo, mandhari, matumizi ya lugha.**

Wahusika ni watu, wanyama na viumbe wengine wanaotumiwa katika riwaya. Wahusika hawa wajigawa kati ya **wahusika wakuu** na **wahusika wasaidizi** au **wajenzi**. Wahusika wakuu ni wale ambao wanajitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Wahusika hawa wanaweza kuwa watu, wanyama, au viumbe wa kufikirika.

Wahusika wasaidizi au wajenzi ni wale ambao husaidia wahusika wakuu katika kusukuma migogoro ya hadithi mbele na kutoa maudhui.

Wahusika hawa wanaweza kuwa bapa, duara na foili. Wahusika bapa ni wale ambao hawabadiliki kitabia au kihulka kutoka mwanzo wa riwaya. Hawa wanatambulika kwa njia ya kuhukumu, kutoshaurika na kupenda kuongoza.

Wahusika duara ni wale ambao wanabadilika kitabia na kimawazo. Wahusika foili nao ni wale wanaojikita kati ya bapa na duara.

Muundo huonekana kama jinsi riwaya inavyopangwa kutoka mwanzo hadi mwisho.

Mtindo ni mbinu zinazomwezesha mwandishi kutimiza wajibu wake wa kutoa maadili katika jamii lengwa kwa kutumia lugha.

Mandhari ni neno linaloeleza mazingira, eneo, mahali, au wakati wa kazi hii ya fasihi inayohusika

## 2. Maudhui

Mtunzi anaanza kutunga sanaa hii akiwa na jambo la kulenga kwa njia ya kutoa fundisho, maonyo au maadili fulani kwa jamii. Lengo analo mtunzi ndilo huwa ni dhamira wakati maudhui huwa ni yaliyomo yaani yale yanayozungumziwa kwa jumla katika kazi ya sanaa hiyo. Katika kazi ya sanaa, kuna dhamira kuu na dhamira ndogo. **Dhamira kuu** inamaanisha wazo kuu linalomsukuma mtunzi kuitunga kazi ya sanaa. **Dhamira ndogo** nayo husaidia kuendeleza dhamira kuu.

**Falsafa:** ni elimu ya asili; busara au hekima. Falsafa ya msanii hugusiwa kutokana na jinsi anavyoelewa matatizo ya jamii na jinsi anavyoyatolea suhuhisho kwa njia ya busara, amani na utulivu

**Ujumbe:**riwaya huwa na ujumbe maalumu ambao msanii anataka uifikie jamii aliyoikusudia. Ujumbe katika kazi za kifasihi ni mafunzo mbalimbali ambayo

hupatikana ndani ya kazi hiyo

**Migogoro** katika riwaya ni hali ya kutokubaliana kimawazo na kimatendo kati ya wahusika.

Kulingana na matumizi ya lugha kama chombo madhubuti katika kazi hii, inamlazimu mtunzi kutumia maneno teule yenye maana kamili.

***Zoezi la 8: Chagua riwaya moja maktabani, usome na uchunguze fani na maudhui, kisha wasilisha kazi yako mbele ya darasa.***

### 8.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

***Zoezi la 9: Kwa kushirikiana na wenzako, Jadili mambo yafuatayo:***

1. Umuhimu wa riwaya katika jamii ya Wanyarwanda .
2. Riwaya hutofautiana sana na hadithi fupi.

### 8.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu

***Zoezi la 10: Tunga kifungu chenye aya nne uthibitishe umuhimu wa riwaya kwa kuhifadhi na kukuza utamaduni wa jamii husika.***

## SOMO LA 9: UFAFANUZI WA TAMTHILIA

***Zoezi la 1:***

1. Uliwahi kutazama ama kusikia mchezo wowote wa kuigiza? Kama upo ulikuwa mchezo gani?
2. Wahusika walikuwa kina nani?
3. Eleza mambo mawili yaliyozungumziwa katika mchezo huo.
4. Kuna maadili yoyote uliyoyapata kutokana na mchezo huo?
5. Husisha mchezo huo na sura moja ya tamthilia iliyopo hapo chini.

## 9.1 Kusoma na Ufahamu: Sura Moja ya Tamthilia

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, someni sura hii ya tamthilia ya Kijiba cha Moyo (iliyoandikwa na Timothy Arege) na baadaye mjibu maswali ya ufahamu yanayofuata.*

*(Baadaye siku ile ile. Nyumbani kwa mzazi wake Sele. Zainabu yuko ukumbini ameketi kwenye kochi huku akifuma kitambaa. Kuna mbisho mlangoni.)*

**Bi. Rahma:** *(Anaubisha mlango.)* Hodi! *(Kimya. Baada ya muda anabisha tena.)*

Hodi! *(kimya vile vile. Mara ya tatu anabisha kisha sauti yake inasikika.)*

Hodi! Wenyewe mpo? *(Zainabu anaondoka mbio kwenda kuufungua mlango.)*

**Zainabu:** *(Akielekea mlangoni.)* Karibu. *(Anaufungua mlango. Anachangamka anapomuona Bi Rahma)* Shangazi karibu ndani. Karibu!

**Bi. Rahma:** Asante. Asante mwanangu *(wakisalimiana kwa mikono.)* hii ilikuwa hodi ya mwisho. Nilipoita ya pili pasi kuitikiwa niliona hamna mtu lakini alhamdulilahi, nashukuru nimekupata.

**Zainabu:** *(akimwelekeza kwenye kiti.)* Karibu shangazi. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu Kwa kutujalia afya na uzima. *(wanaketi kutazamana.)* Nyumbani hawajambo?

**Bi. Rahma:** Hawajambo mwanangu, niliona mmenyamaza sana hivyo nikaamua niwajulie hali.

**Zainabu:** Umefanya vizuri shangazi kuja kutujulia hali.

**Bi. Rahma:** Vipi watoto?

**Zainabu:** hawana neno ila Sele kidogo ametutia wasiwasi.

**Bi. Rahma:** *(kwa mshangao.)* wasiwasi?

**Zainabu:** Si… ni kama … kama wasiwasi niseme.

**Bi. Rahma:** Anaumwa?

**Zainabu:** Hata sijui. Sisi tunamwona kama anayeumwa lakini yeye anasema haumwi.

**Bi. Rahma:** Wala ugonjwa haumlazi ndani?

**Zainabu:** Hata kidogo! Ila mara nyingi huwa mumo humo ndani peke yake. *(kimya.)*

ni kama anayejitenga na watu…

**Bi. Rahma:** Kumbe ndiyo maana kwangu hatii guu!

**Zainabu:** Ingawa halalamiki kuumwa popote, hamu ya chakula imemwisha. Mara nyingi anakitazama tu na kama akila atakigusagusa mara mbili tatu na kukiacha…

**Bi. Rahma:** Hamu ya chakula nayo wajua wakati mwingine hutegemea mpishi. Nyinyi siku hizi hamna muda kukiandaa chakula. Mnafukuzilia hekaheka nyingi. Na habasi. *(kimya.)* Hata muda wa kuandaa mapishi ya kisawasawa hawana. Umeliwa na hizi nenda rudi zenu. Watavilaje vyakula vya kuharakishwa? Heri huvutwa kwa subira . Vyakula visivyopata kutua sufuriani, vipi vitatua moyoni?

**Zainabu:** Shangazi, ni kweli zipo shughuli nyingi lakini zenyewe hazinizuii kuiandalia familia yangu Chakula Kizuri. Hata huyo Aisha mwenyewe siwezi kusema hafanyi inavyomjuzu. Anajitahidi sana…) *(kimya)*

**Bi. Rahma:** Au labda mkono ni ule ule mmoja wa upishi. Usisahau kuwa mchele mmoja lakini mapishi  mengi. Hili hukipa upya na ugeni chakula.

**Zainabu:** Hilo hatujalisahau. Aisha huandaa biriani akiwa na muda wa kutosha. Mara nyingine wali mweupe, mara nyingine pilau au chapati. Nani anayemshinda hapa katika upishi wa vitumbua au hata viazi karai? *(kimya.)* kuridhika kwa familia ndiyo raha yetu. Ila Sele naye ana mienendo ya ajabu siku hizi. Si kwa sababu ya chakula! La hasha!

**Bi. Rahma:** nini basi? Labda ni kitoweo.

**Zainabu:** Hata kitoweo chabadilishwa. Kama si pojo ni nyama; si ya kuku, si ya nyama au samaki…mara wa kupika, mara wa kukaanga…

**Bi. Rahma:** Tafi!

Zainabu: Si tafi tu. Hata kambare. Mwingine pweza.

**Bi. Rahma:** Hata vidagaa si vibaya.

**Zainabu:** Hivyo ndo hali kabisa basi. Anavichukia.

**Bi. Rahma:** Havipendi?

Zainabu: Anasema anavipenda sana…

Bi. Rahma: Basi mpikie hivyo na sima. Si chapatti na wali tu mwanangu!

**Zainabu**: Shangazi, sele ana tabia za ajabu sana siku hizi kama nilivyokueleza. Anasema eti anawaonea dagaa huruma kuliwa na papa na yeye pia awale. *(kimya.)*

anasema huku ni kuonewa maradufu. Anasema… anasema… eti tena kuwa hapendi vinavyoliwa huku vinatazama tu.

**Bi. Rahma:** *(Amekinaishwa na maelezo haya.)* basi mgonjwa kweli. Vipi mtu akihurumie kitoweo? *(kimya. Ana wazo jipya.)* Mbona basi usimpikie papa alipize kisasi kwa niaba ya vidagaa? *(wote wanacheka. Kisha kimya.)* Sasa utafanya nini? Basi mpikie hao papa.

**Zainabu:** Hao hataki kuwaona kabisa.

**Bi. Rahma:** Nao wana nini tena?

**Zainabu:** Sasa hao nao anadai wana nafsi zisizo zao. Eti wanaishi kwa kutegemea nafsi za vidagaa na hivyo kuwala si tofauti na kuvila vidagaa. Hivyo vidagaa vitakuwa vimeliwa mara ya pili! Hapendi hili kabisa.

**Bi. Rahma:** hiyo sasa itakuwa nafsi ya vidagaa katika papa au ni pepo za hao vidagaa katika papa?

**Zainabu:** Yeye haonyeshi tofauti. Leo atasemea ni nafsi lakini kesho atasema ni pepo. *(kimya kirefu kiasi.)*

**Bi. Rahma:** Basi Sele ni mgonjwa. Apelekwe kwa mganga apate dawa.

**Zainabu:** Dawa gani kwa mtu asiyeumwa?

**Bi. Rahma:** *(Anamtazama Zainabu kwa makini. Kwa sauti ya chini.)* Zamani kidogo angefaa kufanyiwa kafara ni haba maana mashetani wamepungua. *(kimya. Kama anayekumbukia kitu.)* Bora Zaidi apungwe kuwaondoa pepo. Kafara tu haitoshi. Kama kweli ni pepo waliomwingilia ni lazima yeye kupungwa.

**Zainabu:** Haina neno kumtafuta mganga. Unamfahamu mganga mzuri?

**Bi. Rahma:** *(baada ya kufikiri.)* hawapo tena wa kama zamani lakini huenda wapo. *(anamtazama Zainabu usoni.)* Hata hivyo, mchunguze Sele kwa makini. Huenda tatizo lake ni yeye. Labda hajielewi. Au labda yote mawili. Na ikiwa ni yote mawili basi ni hatari Zaidi. Kama uliyonieleza ni kweli, basi namwona kama ambaye anafukuzana na kivuli chake. Kwa kuwa sasa ana mke, mwambie alichunguze tatizo lake kwa makini. Tusifanye halahala. Hata mwenyewe ninataka kusema naye mara kwa mara. Kwa sasa tuanze na huyo mke wake.

**Zainabu:** Haya! Nitamwambia Aisha…

**Bi. Rahma:** Huenda itasaidia.

**Zainabu:** Huenda itasaidia ndiyo, ila mkewe naye haelekei kutoa habari za

kutupa mwelekeo wowote. Watoto wa siku hizi wanapenda kuyaweka siri mambo yawahusuyo. Si kama wakati wetu. Hatukuwaficha wazee hata moja wala hatukuwapinga katika maamuzi na ushauri waliotupa. Hawa wa leo ni mpaka mbishane. Nidhamu tuliyokuwa nayo hawana tena. *(Anarejelea kufuma.)*

**Bi. Rahma:** Hawa hiyo ndiyo dunia yao. Wewe ulikuwa na yako wakati wako. Mimi vile vile. Na hiyo ndiyo dunia. Mfano wa mto. Maji yaliyoujenga mto jana ni tofauti na yanayoujenga leo. Vivyo hivyo ya kesho yatakuwa tofauti lakini bado mto utakuwa ule ule. Tofauti hatuioni ila kwa mwenye moyo wa kupembua. *(Mara anaingia Aisha mbio. Anamsalimu Bi. Rahma haraka haraka)*

**Aisha:** *(Akimsalimu)* Aah Bibi. Shikamoo!

**Bi. Rahma:** Marahabaa Marahabaa mama. Hali gani mjukuu wangu?

**Aisha:** Nzuri. Hamna neno. *(baada ya kumsalimu anaelekea upande wa pili wa chumba. Anaanza kuchakura vitabu pembeni. Muda huu wote, wote wawili wamemtazama.)*

**Zainabu**: Aisha!

**Aisha:** Beee! *(ameinamia rundo la vitabu)*

**Zainabu:** Tabia gani hii? Hata kama ulikuwa hapa mapema watoka utokako unafululiza moja kwa moja penye vitabu! Humwoni bibi hapa? Kuna nini?

**Aisha:** *(Akiendelea na shughuli zake.)* Hamna kitu.

**Zainabu:** Hamna kitu?

**Bi. Rahma:** Aisha, desturi gani hii? Mtoto utoke kule nje sisi wazee wako tuko hapa kisha utupuuze na kuelekea kwenye vitabu! Ndivyo elimu yenu hii ya kiungu inavyowatuma kufanya? Huo ndio ustaarabu kwenu?

**Aisha:** Si hivyo. Kuna jambo ambalo aliniambia sele nami nikawa sielewi vizuri nikataka nilifuatilie na kupata usuli wake kabla sijasahau.

**Zainabu:** *(Kwa ukali.)* Jambo tu la kuambiwa ndilo linalokufanya utuvunje heshima sisi wazee wako! Eeh!

**Bi. Rahma:** *(kwa Zainabu.)* Jambo gani ambalo asingetuuliza sisi tukampa ufafanuzi? *(Kwa Aisha.)* Elimu hiyo mnayoitafuta na kuilipia vitabuni sisi mtatudharau ndo tunayo hapa. *(Aisha anamtazama.)* Wameitoa kwetu wakaitia humo na nyinyi sasa inawafanya kuwa na kiburi bila kufahamu kuwa waliyochota kutoka hapa *(Anaashiria kichwa.)* Ni kidogo tu. Ni kama kisima kila mtu anachota na kila kiumbe kunywa kipendavyo lakini maji yake hayaishi.

**Aisha:** Sivyo biibi. *(Kimya.)* Baada ya kusema na Sele kuna jambo alilosema nami nikahisi kama nimelisikia au nimelisoma mahali ila sikuwa na hakika. Nikaona kuwa nikiliachia litanichenga na kunitoka akilini maana ninahisi kama ninayechezewa mchezo fulani wa mawazo na maneno yake. Na mimi fikra zikanielekeza katika maandishi fulani ambayo sikumbuki vizuri kama yalikuwa kitabu au kitumeme. Ndiyo sababu ya kunifanya nje moja kwa moja mpaka hapa. Samahani sana. *(Kimya.)*

**Zainabu:** Jambo gani hilo hasa?

**Aisha:** Jambo dogo.

**Bi. Rahma:** Dogo ilhali linakufanya utupuuze sisi? Usipochunga utakuja tumwa kwangu nikutie skuli. Haya!

**Aisha**: Ni kama dogo si dogo; kubwa si kubwa. Mara nahisi ni dogo mara kubwa. *(Kimya. Anasonga kando na kuanza kuzungumza pekee yake.)* Kama lililotiwa hamira, linafura na kujaa fikirani. Kichwa kinakuwa kizito kama nanga. Hapa naona panahitaji upekuzi. (*Anarejea alipokuwa mwanzo.)*

**Zainabu:** Aisha!

**Bi. Rahma:** *(Anashituka)* Naam mama!

**Zainabu:** Na wewe umekuwa kama huyu mume wako?

**Aisha:** Hata kidogo!

**Bi. Rahma:** Mambo ya watoto! Wala hamna jambo dogo na kubwa. Ukubwa na udogo wa jambo hutegemea namna ilivyomtua mtu moyoni. Hiyo ndiyo tofauti ya ukubwa au udogo wa jambo.

**Zainabu:** Haswa! Aisha, hebu tuambie kimasomaso mbele ya bibi yako tatizo la mwenzako. Hivi anakuambia ana nini? *(anaonekana mwenye fikra nyingi.)*

**Aisha:** Hasemi. Huwa tunazungumza tu ingawa siyaelewi yale anayosema. Ni kama haya hivi yaliyonileta hapa. *(Wote wanamtazama kwa muda.)*

**Bi. Rahma:** Ni yepi hayo yaliyokuleta huku?

**Aisha:** *(Baada ya muda.)* Kuhusuuu… kuhu… kuhusu papa.

**Zainabu:** (Kama aliyeshtuka.) Papa tena?

**Bi. Rahma:** Papa upanga au papa ndege? (Kimya.)

**Aisha:** Papa tu.

**Bi. Rahma:** Basi kamuulize.

**Aisha:** Ningemuuliza lakini hapendi maswali mengi.

**Bi. Rahma:** Basi mrai. Mwanamke ni ulimi. Lakini utayajuaje haya kama mwenendo ndio huu unaotuonyesha? *(Anageuka kumtazama Aisha.)* Moyo wa mtu nyumba na mambo ya nyumba kweli kunga. Lakini siri za nyumba azijuaye mwenyewe. Usipozijua wewe atazijua nani? *(Kimya.)* Utie ulimi asali atakueleza kila kitu. Utamtoa nyoka pangoni mama. Hapana jambo kubwa kwa mwanamke kulipata. Ulimi wa nini basi?

**Aisha:** Lakini bibi huyo alikuwa mwanamke wa jana! Mwanamke wa siku hizi tofauti. Anakwenda na majira ya usasa. Hana tofauti na mwanamume.

**Zainabu:** Bi mkubwa wasichana wetu hawa si kama zamani tena. Wanashindana na wanaume...

**Bi. Rahma:** Sisi ndizo kunga tulizofundishwa. *(Kwa Zainabu huku akiinuka.)* Mimi naenda kumtazama nione hali yake hiyo. Na wewe mwanangu anza kutapatapa ukatafuta waganga. *(Anageuka na kumtazama Zainabu.)* Umesikia mwanangu?

**Zainabu**: Nimesikia.

**Bi. Rahma:** Haya! Usikawie sana. Utakuja chekwa.

**Zainabu:** Tayari wamekuja madaktari hapa wakamwona ila Sele mwenyewe haamini kama anaumwa. Wala hao madaktari nao hawaelezi waziwazi kama Sele ana nini? Sijui kama kwa kupenda au kwa kushindwa kueleza.

**Bi. Rahma:** Madaktari si wajinga usiwaone wametulia vile. Washindweje nao ndo manyakanga?

**Zainabu:** Nini basi?

**Bi. Rahma:** Mimi nitajuaje? Wanajua wao wenyewe. *(Anaondoka.)*

**Zainabu:** *(Kwa Aisha.)* Aisha!

**Aisha:** Beka!

**Zainabu:** Mwandalie bibi chai na vile vitumbua vilivyobaki asubuhi. Usimsahau Sele. Labda akimwona bibi yake atakula kidogo.

**Aisha:** Nitamwandalia. *(Anaondoka. Zainabu anarejelea kufuma kitambaa.)*

*(Kutoka Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Mchepuo wa Lugha, Kidato cha 6. (2017).* Longhorn Publishers. Nairobi)

***Maswali ya ufahamu.***

1. Onyesho hili linafanyika wapi?
2. Eleza uhusiano uliopo kati ya Aisha na Zainabu.
3. Zainabu na Sele wana uhusiano gani?
4. Fafanua mienendo na tabia za Aisha.
5. Kwa nini wanawake wa kisasa (siku hizi) hawajishughulishi sana na huduma za nyumbani?
6. Jadili sifa za Bi. Rahma.
7. Kuna tofauti gani kati ya wanawake wa zama za kale na zama hizi?
8. Bi. Rahma anaonaje ugonjwa wa Sele?
9. Eleza uhusiano uliopo kati ya Zainabu na Aisha.
10. Ni maadili gani mnayoyapata kutokana na onyesho hili?

## 9.2 Msamiati kuhusu Sura Moja ya Tamthilia

***Zoezi la 2. Tumia mshale kwa kuonyesha maana za msamiati wa maneno katika A kwa kuyahusisha na maelezo uliyopewa katika sehemu B***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Wasiwasi | A. mara mbili ya idadi, ukubwa,ujazo |
| 2. Kujuzu | B. mkusanyiko wa vitu vingi vilivyowekwa pamoja |
| 3. Biriani | C. kushika kidogo |
| 4. Pweza | D. dukuduku la moyo |
| 5. Maradufu | E. kushurutisha kufanya jambo |
| 6. Kugusa | F. mnyama wa baharini mwenye mikia minane |
| 7. Halahala | G. upesi upesi, haraka haraka |
| 8. Rundo | H. mambo ambayo hayatakiwi yajulikane |
| 9. Kunga | I. kukosa makini, kuwa na wasiwasi |
| 10. Kutapatapa | J. chakula kinachotengenezwa kwa wali uliokaangwa na kuchanganywa na nyama iliyokaangwa na masala. |

***Zoezi la 3: Eleza maana ya msamiati huu na kuutumia katika kutunga sentensi.***

1. Kuandaa
2. Kufukuzana
3. Ushauri
4. Kafara
5. Kubishana
6. Kupuuza
7. Ustaarabu.
8. Kuvunja heshima
9. Kitoweo
10. Kudharau

***Zoezi la 4: Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia msamiati huu: mienendo, wamepungua, usuli, mapishi, hamu ya chakula.***

1. Mume wangu hataki chakula, amekosa…………….
2. Siku hizi, wazazi hulalamikia…………… ya vijana wao.
3. Wanawake wa zama zilizopita walijivunia ……….. yao mazuri.
4. Aisha alipekuapekua vitabu ili atafute………….. wa jambo aliloambiwa na Sele.
5. Waganga wenye uwezo wa kupunga mashetani……………

## 9.3 Sarufi: Vishazi Tegemezi

***Zoezi la 5: Tazama sentensi zifuatazo na kujadili maswali yafuatayo:***

**Sentensi:**

1. *Imani za kishirikina hupingana na matibabu ya kisasa* lakini watu wengi huamini zaidi uwezo wa matibabu ya kisasa.
2. Aisha amerekebisha tabia na mwenendo wake *alipopewa mawaidha na wazazi wake.*
3. *Atakayejiingiza katika matendo yanayopingana na mila na desturi zetu,* atapata taabu nyingi.
4. *Madaktari si wajinga,* wao hufanya kazi zao kwa ustadi mkubwa.

***Maswali:***

1. Andika upya sehemu za sentensi zilizoandikwa kwa mlazo
2. Linganisha sehemu hizo za sentensi zilizoandikwa kwa hati ya mlazo baada ya kuziondoa katika sentensi kuu ambamo zimetumiwa.

***Zoezi la 6: Tunga sentensi zako nne zinazofuata muundo wa sentensi ulizopewa hapo juu katika zoezi la 5.***

**Maelezo muhimu: Vishazi**

- **Maana ya kishazi**

Kwa kawaida, sentensi huundwa na vifungu viwili muhimu ambavyo ni kirai na kishazi. Kirai ni neno au fungu la maneno ambalo husimamia mtendaji.

Kwa upande mwingine, kishazi ni sehemu ya sentensi ambayo hubeba dhana ya tendo linalotendwa na kirai. Kwa hiyo, kishazi hulazimisha kuwepo kwa kitenzi, kinyume cha kirai.

- **Aina za vishazi**

Kuna aina mbili za vishazi: Kishazi huru na kishazi tegemezi.

- **Kishazi huru**

Kishazi huru ni sehemu ya sentensi yenye maana kamili kutokana na kitenzi chake. Sehemu hii huweza kujitokeza yenyewe kama sentensi.

***Kwa mfano:***

Dawa za kulevya huharibu afya ya binadamu.

Imekatazwa kuvuta sigara hadharani.

- **Kishazi tegemezi**

Kishazi huitwa kishazi tegemezi kwa sababu hakiwezi kuwepo peke yake bila kutegemea kishazi huru. Kimuundo, kishazi tegemezi huwa na viambishi rejeshi kama "-ye", "-o" kulingana na ngeli za majina au huanza kwa vihusishi kama vile "baada ya", "kabla ya", n.k.

***Kwa mfano:***

- Atakayejiingiza katika matendo yanayopingana na mila na desturi zetu, atapata taabu nyingi.
- Aisha amerekebisha tabia na mwenendo wake baada ya kupatiwa mawaidha na wazazi wake.

***Zoezi la 7: Katika sentensi hizi bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi***

1. Bi. Rahma aliwaonya watu kuhusu mila na desturi na watu wote walimsikia.
2. Mtu ambaye hayaheshimu mawaidha ya wazazi atapata cha mtema kuni.
3. Kabla ya kuingia ndani Bi. Rahma alibisha hodi.
4. Anayezungumza na wazee hujua mambo mengi.
5. Walioonyesha mwenendo mwema walifanikiwa kujenga familia imara.

## 9.4 Matumizi ya Lugha: Fani na maudhui katika Tamthilia

***Zoezi la 8: Kumbuka mchezo wa kuigiza mmoja uliochezwa na « Itorero Indamutsa » kutoka Radio Rwanda au « Urunana » kisha jadili maswali yafuatayo:***

1. Kwa maoni yako, tamthilia ni nini?
2. Ni dhamira zipi zinazoendelezwa sana katika tamthilia?
3. Wahusika wake hutofautianaje na wahusika wengine k.v. wahusika wa hadithi simulizi ?
4. Ni sifa gani za mchezo wa kuigiza au tamthilia?

***Zoezi la 9: Soma maelezo hapa chini ili kujibu maswali uliyopewa chini yake.***

- **Maana ya tamthilia**
  - Tamthilia ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa ili uigizwe jukwaani kwa kuwasilisha ujumbe kwa jamii.Kuna aina mbili za jukwaa:
  - Jukwaa la akilini kama hali ya kujiundia akilini k.v. mchezo unaoigizwa redioni.
  - Jukwaa la hadharani, yaani mahali ambapo maonyesho ya tamthilia yanaigiziwa mbele ya watazamaji au wasikilizaji.
  - Tamthilia ni mojawapo ya kazi za sanaa ya fasihi andishi ambazo mtindo wake ni wa kimaandishi badala ya kimasimulizi.

- **Wahusika katika tamthilia**

Wahusika au watendaji wa tamthilia huwa wanadamu ambao huiga kwenye jukwaa tabia na matendo ya watu wengine wapatikanao katika jamii. Hutofautiana na wahusika katika fasihi simulizi kwa sababu wale hushika vitabia wao wenyewe wakati ambapo wahusika wa fasihi simulizi hujitokeza kwa njia ya masimulizi.

- **Aina za wahusika katika tamthilia**

Kama mojawapo ya tanzu za fasihi andishi, tamthilia huwa na wahusika wa aina sita kama ifuatavyo: Wahusika wakuu, wahusika wasaidizi, wahusika wadogo, wahusika bapa, wahusika duara pamoja na wahusika wafoili. Makundi haya ya wahusika yalielezwa wazi katika somo kuhusu hadithi fupi.

- **Aina za tamthilia**

Tamthilia au mchezo wa kuigiza huwa na aina mbalimbali kulingana na dhamira kuu inayoendelezwa. Utaipata tamthilia ya mapenzi, ya kihistoria, ya kisiasa, ya kidini, ya kiuchumi, n.k. Tamthilia hizi zote huangukia katika moja ya makundi makuu yafuatayo:

- **Tanzia**

Ni aina ya tamthilia iliyojaa huzuni ndani yake, mikasa, matokeo ya vifo na mateso makali. Mwisho wa hadithi za aina hii huwa ni wa masikitiko, maanguko na hasara kubwa kwa mhusika mkuu au jamii inayoibushwa. Wengine huita aina hii tamthilia simanzi au trejedia.

- **Ramsa**

Tamthilia zenye kuchekesha kutokana na utani, mzaha, kejeli, maneno yaonyeshayo ujinga, n.k. Iwapo hadithi hizi huwa na dhana ya uchekeshaji, lengo lake ni kukosoa jamii, watawala na tabia mbaya na watu binafsi. Aina hii huitwa tena Tamthilia cheshi au komedia.

- **Tanzia – ramsa**

Tanzia – ramsa au simanzi – cheshi ni mchezo wenye sifa za ramsa, lakini ndani ya uchekeshaji wake na tanzia kuna kama vile kifo cha mhusika mkuu au kuanguka kwa jamii. Pengine huitwa Trejikomedia.

## Sifa za michezo ya kuigiza

Unapotaka kuikabili michezo ya kuigiza inabidi uzingatie fani na maudhui yake kama yalivyoelezwa katika hadithi fupi pamoja na riwaya.

- **Maudhui** ni yaliyomo katika tamthilia. Mwandishi wa tamthilia ana jambo analotaka kulionyesha jamii. Maadili na maonyo huweza kupatikana kutoka katika tamthilia. Maudhui yanajengwa na dhamira kuu na dhamira ndogo.

- **Fani** inajengwa na:

    - ***Muundo:*** tamthilia hujengeka kwa muundo maalum. Huwa na mwanzo unaotujulisha kwa ufupi yale ambayo tunatazamia kukutana nayo hapo mbeleni. Mwanzo unasukumwa na mazungumzo yanayobeba migogoro ili kitendo kifike kwenye kilele na hatimaye mwisho wa mchezo.

    - ***Lugha :*** Mazungumzo katika tamthilia ni ya moja kwa moja.

    - ***Migogoro:*** Ni hali ya kutokubaliana kimawazo na kimatendo kati ya wahusika.

- ***Mtindo:*** Tamthilia inaweza kuchukua mtindo wa ishara, yaani huweza kuzungumzia kitu ambacho kinawakilisha kitu kingine. Huweza pia kuwa katika hali ya uhalisia. Huweza pia kutumia nyimbo kwa kusisitiza ujumbe.

Kwa kutegemea mambo hayo mawili, sifa za mchezo wa kuigiza hujitosheleza kama ifuatavyo:

- Wahusika wake huwakilishwa na watendaji ambao hujieleza au hutenda wenyewe.
- Watazamaji au wasikilizaji hushirikishwa.
- Mchezo hutokea kwenye jukwaa mbele ya hadhira.
- Mapambo hutumiwa ili kuashiria kubadilika kwa mazingira au wakati.
- Hutumia mbinu za lugha kama vile chuku, tanakali za sauti, tamathali na nyinginezo.
- Huhusisha aina nyingine za sanaa kama vile ushairi na nyimbo.

## Umuhimu wa michezo ya kuigiza

Kama tanzu zote za fasihi, lengo kuu la tamthilia ni kutoa maadili, maonyo au kurekebisha tabia mbaya za jamii. Licha ya hayo, tamthilia huwa na madhumuni ya kuburudisha, kuelimisha, kukuza uwezo wa kukariri kwa watendaji bila kusahau njia ya kufikia manufaa kiuchumi.

***Maswali:***

1. Kwa maneno yako, eleza maana ya tamthilia.
2. Tamthilia ni za aina tofauti. Eleza aina hizo na kutoa mifano ya tamathilia unazofahamu kwa kila aina.
3. Ni mambo gani yanayochunguzwa katika uhakiki wa fani ya tamthilia?
4. Ni mambo gani yanayozungumziwa katika uhakiki wa maudhui ya thamthilia?

## 9.5 Kusikiliza na Kuzungumza : Majadiliano

***Zoezi la 10: Shirikiana na wenzako na kujadili au kutetea misimamo ifuatayo:***

- Michezo ya kuigiza ni sanaa ambayo humfaidisha msanii.
- Matumizi ya dawa za kulevya ni pingamizi kubwa kwa maendeleo ya nchi.
- Michezo ya kuigiza ni mojawapo ya shule za kuelimisha maadili na mwenendo mwema.
- Michezo ya kuigiza hukuza akili.

## 9. 6. Kuandika : Uandishi wa Muhtasari wa Tamthilia

***Zoezi la 11:Tega sikio au fuata kipindi chochote cha thamthilia kitokeacho kwenye Redio au televisheni yoyote kisha uandike muhtasari wake na kuwasilisha kazi yako mbele ya darasa.***

**TATHIMINI YA MADA YA PILI**

1. Eleza umuhimu wa hadithi fupi katika jamii husika.
2. Tunga shairi la aina ya tarbia lenye beti tatu kuhusu mojawapo ya mada hizi:
   a. Usafi
   b. Mavazi
   c. Heshima
3. Jadili umuhimu wa riwaya kwa kuhifadhi na kukuza utamaduni.
4. Jadili umuhimu wa tamthilia kama mojawapo ya njia ya kuhifadhi utamaduni wa jamii na kukuza tabia ya kujitegemea maishani.
5. Tunga sentensi tano zenye vishazi huru na nyingine tano zenye vishazi tegemezi.

# MADA KUU YA 3:
## UBUNAJI

# MADA KUU : UBUNAJI

## MADA NDOGO: HOTUBA NA UFUPISHO

**Uwezo Upatikanao katika Mada:** Mwanafunzi ataweza kuelewa mtindo wa hotuba na kuuzingatia katika mazoezi ya utungaji pamoja na ufupisho na kujua kuchambua kitenzi kwa njia ya uambishaji.

**Malengo ya Kujifunza:** Baada ya kujifunza hotuba, mwanafunzi ataweza kutathmini hotuba kulingana na sifa zake, kulinganisha hotuba na insha nyingine alizozisoma, kuendeleza hotuba kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa, kufupisha hotuba husika na kulinganisha ufupisho uliotolewa kutoka makundi tofauti.

**Kidokezo:**

1. Kiongozi anapokutana na wananchi huwa anaweza kuzungumzia nini?
2. Je, mazungumzo hayo huwa ni ya kutayarishwa au huwa ni ya ghafla?
3. Kuna tofauti yoyote iliyopo kati ya mazungumzo yaliyotayarishwa na mazungumzo ya ghafla? Eleza maoni yako.
4. Mazungumzo kama hayo yanaitwaje?
5. Uliwahi kuhudhuria mkutano wowote?
6. Eleza kwa ufupi mambo yaliyozungumziwa kwenye mkutano uliowahi kuhudhuria.

## SOMO LA 10: MAANA YA HOTUBA

**Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali yaliyopo hapo chini yake.**



***Zoezi la 1: Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro hapo juu***

1. Wahusika hawa wanafanya nini?
2. Ni vifaa gani unavyoona kwenye mchoro huu?

### 10.1. Kusoma na Ufahamu: Hotuba ya Meya baada ya Kazi za Umuganda

*Soma hotuba ya Meya baada ya shughuli za Umuganda, kisha jibu maswali uliyopewa hapo chini:*

Mheshimiwa mgeni rasmi mkuu wa mkoa, Mheshimiwa mkuu wa kikosi cha askari jeshi wa wilaya yetu, Mheshimiwa bibi mkuu wa askari polisi wa wilaya yetu, Mheshimiwa katibu mtendaji wa wilaya yetu, mabwana na mabibi mliokusanyika hapa leo, Hamjambo? Ninachukua fursa hii kuwakaribisha hapa katika wilaya yetu.

Ninapenda kumshukuru mgeni rasmi kwa kuja kujiunga nasi leo kwa lengo la kushiriki pamoja nasi katika kazi za umuganda mwishoni mwa mwezi huu ili tuweze kujitengenezea barabara hii.

Mgeni wetu mheshimiwa, kazi hizi za umuganda zinatoa mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa letu na nguvu za kila mtu zinahitajika kwa ujenzi wa maendeleo ya nchi yetu. Mfano wa karibu, leo tumemaliza kujitengenezea barabara itakayotuunganisha na majirani zetu kutoka wilaya nyingine. Barabara hii bila shaka itatusaidia katika kurahisisha kazi ya ufanyajibiashara, utalii, kurahisisha uchukuzi wa wagonjwa mahututi kutoka zahanati kwenda hospitali. Aidha hata matembezi nayo yatakuwa rahisi kwa kila mtu. Zaidi ya hayo, usafi utaongezeka, na usalama barabarani utaweza kuimarishwa kwa kujiepusha na ajali zisizokuwa za lazima.

Mheshimiwa mgeni rasmi, haya yote yameweza kufanikiwa tu kutokana na ushirikiano miongoni mwetu. Ushirikiano huu umefanikisha maendeleo ya watu binafsi na hata ya nchi nzima. Bila ya kufanya kazi kama hizi, maendeleo hurudi nyuma. Shughuli za umuganda ni wajibu wa kila mwananchi anayependa nchi yake na maendeleo ya jamii nzima. Kumbukeni kuwa hakuna mtu mwingine atakayetujengea taifa letu. "Taifa letu litajengwa na sisi wenyewe, ni sisi tutakaojijengea taifa letu." Ni lazima sisi sote tujiunge pamoja ili tuweze kufanikiwa kuokoa fedha nyingi ambazo huweza kutumiwa katika shughuli nyingine za kimaendeleo kama vile kuleta huduma za afya, kulipa mishahara ya watumishi, kuleta maji safi na hata umeme.

Isitoshe, shughuli hizi za umuganda husaidia katika upandaji wa miti kwa kuzuia mmonyoko wa ardhi, kuwajengea nyumba watu wasiojiweza, kujenga shule, hospitali, masoko na madaraja kwenye mito. Kama wahenga wasemavyo "Umoja ni nguvu na pia kidole kimoja hakivunji chawa". Tushirikiane sote ili tuzidi kuiendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa mgeni rasmi, mheshimiwa mkuu wa kikosi cha askari jeshi, mheshimiwa bibi mkuu wa askari polisi, mheshimiwa katibu wa wilaya yetu, na wananchi wapendwa, mabibi na mabwana, ni vyema tuelewe kwamba mtaka cha uvunguni sharti ainame, na ukiona vyaelea vimeundwa. Ni vizuri sote tuelewe kila mwananchi hana budi kutoa mchango wake katika kulijenga taifa letu kwa kushiriki katika shughuli kama hizi za umuganda ambazo hufanyika kila mwisho wa mwezi. Tulinde miundo mbinu iliyojengwa, kwani ni kielelezo kizuri cha nguvu zetu na ushirikiano wetu. Bila shaka tutaweza kuimarisha maendeleo ya nchi yetu na maisha yetu yatakuwa mazuri zaidi.

Nawashukuru sana kwa kunisikiliza kwa makini, asanteni.

### *Maswali ya ufahamu*

1. Kwa kutumia sentensi moja, eleza jambo linalozungumziwa katika kifungu ulichosoma.
2. Ni watu gani wanaozungumziwa katika hotuba hii?
3. Eleza umuhimu wa kazi za umuganda katika ujenzi wa nchi.
4. Ni nani mgeni rasmi katika hotuba hii?
5. Taja shughuli zinazofanywa na watu wanaoshiriki katika kazi za umuganda?
6. Kufanya kazi za umuganda kunamaanisha nini kwa mwananchi?
7. Baada ya kusoma hotuba hii, umepata fundisho gani?
8. Eleza umuhimu wa barabara kwa wananchi.
9. Wananchi wanahimizwa kufanya nini ili waweze kuimarisha maendeleo na kuboresha maisha yao?

## 10.2. Msamiati kuhusu Hotuba ya Meya

***Zoezi la 2: Husisha maneno kutoka sehemu A na maana zake kutoka sehemu B.***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mheshimiwa | a. Neno la heshima linalotamkwa kabla ya kutaja jina la mtu maarifu. |
| 2. Wilaya | b. Sehemu ndogo katika jimbo au mkoa. |
| 3. Taifa | c. Jamii ya watu wanaoishi katika nchi moja na wanaounganika kutokana na matukio ya kihistoria. |
| 4. Barabara | d. Tukio lenye madhara linalotokea ghafla. |
| 5. Utalii | e. Korongo lenye maji yanayotiririka wakati wote. |
| 6. Ajali | f. Enye kushikwa na ugonjwa sana. |
| 7. Nyasi | g. Hali ya kusafiri mbali au kuvinjari huku na huko ili kuyafurahia mandhari. |
| 8. Mto | h. Mmea pori wenye majani madogo madogo ya kijani unaoliwa na ng'ombe. |
| 9. Mgeni | i. Mtu ambaye si mwenyeji wa mahali fulani. |
| 10. Mahututi | j. Njia ipitayo magari na binadamu. |

***Zoezi la 3: Tunga sentensi zenye maana kamili kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. Kazi za umuganda
2. Askari jeshi
3. Askari polisi
4. Kukaribisha
5. Kushukuru
6. Kujenga
7. Kufanya kwa bidii

***Zoezi la 4: Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno uliyopewa: mikoa, katibu mtendaji, ilitengenezwa, ujenzi wa taifa, rahisi, kazi, kupanda miti, kukata nyasi, mmomonyoko wa ardhi, asanteni.***

1. Kusini ni mojawapo ya ………………………. ya Rwanda.
2. ……………………….. ndiye anayeongoza tarafa.
3. Barabara hii …………………….. vizuri.
4. Ushirikiano wetu unahitajika kwa ………………………………... letu.
5. Itakuwa ………………………….. kujijengea taifa kila mtu akifanya kazi kwa bidii.
6. …………………….. ni mojawapo ya kazi za kulinda mazingira.
7. Tunapaswa ……………………………… ili tujikinge na ugonjwa wa malaria.
8. Katika majira ya mvua, tufanye iwezekanavyo ili tujikinge ………………
9. ……………. sana kwa kunisikiliza kwa makini.
10. ………………………. ndiyo msingi wa maendeleo.

## 10.3. Sarufi: Uambishaji wa Vitenzi

***Zoezi la 5: Onyesha viambishi vinavyounda vitenzi vifuatavyo:***

***Mfano:*** 1. Ninapenda kumshukuru mgeni rasmi – Tunapenda kumskuru mgeni rasmi

Ni-na-pend-a

Ni: kiambishi awali nafsi ya kwanza/ umoja.

-na-: kiambishi kati cha wakati

2. Unapenda kumshukuru mgeni rasmi – Mnapenda kumshukuru mgeni rasmi

3. Anapenda kumshukuru mgeni rasmi – Wanapenda kumshukuru mgeni rasmi

***Zoezi la 6 : Soma maelezo hapo chini kisha ujibu maswali yote husika***

- Uambishaji ni utaratibu wa kuambatisha viambishi mbalimbali kwenye mzizi wa kitenzi.

Viambishi vinavyoambikwa kwa vitenzi huwa na kazi au uamilifu tofauti :

**a. Kuonyesha nafsi katika vitenzi**

**Mfano:**

*1. Ninafanya kazi za umuganda – Tunafanya kazi za umuganda.*

Ni-na-fany-a / tu-na-fany-a

Ni: kiambishi awali nafsi ya kwanza /umoja

Tu-: kiambishi awali nafsi ya kwanza /wingi

*2. Ulifanya kazi za umuganda – Mlifanya kazi za umuganda.*

u-li-fany-a

u-: kiambishi awali nafsi ya pili/ umoja

m-li-fany-a

m-: kiambishi awali nafsi yapili/ wingi

*3. Alifanya kazi za umuganda – Walifanya kazi za umuganda*

a-li-fany-a

a-: kiambishi awali nafsi ya tatu /umoja

wa-li-fany-a

wa-: kiambishi awali nafsi ya tatu/ wingi

**b. Kwa kuonyesha uyakinishi na ukanushi :**

Mfano: Nitaenda sokoni kesho - Sitaenda sokoni kesho – Hatutaenda sokoni kesho

Utaenda sokoni kesho - Hutaenda sokoni kesho - Hamtaenda sokoni kesho

Ataenda sokoni kesho - Hataenda sokoni kesho – Hawataenda sokoni kesho

Si-ta-end-a ha-tu-ta- end-a

Si-: kikanushi ha-: kikanushi

**c. Kwa kuonyesha njeo/ wakati**

Mfano: Kazi za umuganda zi**na**toa mchango katika ujenzi wa taifa.

zi-**na**-to-a: wakati uliopo

Barabara i**ta**tusaidia katika ufanyaji biashara.

i-**ta**-tu-saidi-a: wakati ujao

Tu**me**maliza kujitengenezea barabara.

tu-**me**-maliz-a: wakati uliotimilika

Nchi **hu**jengwa na nguvu za wananchi wake.

**Hu**-jeng-w-a: wakati wa mazoea

Tu**li**jitengenezea barabara mwezi huu.

tu-**li**-ji-tengenez-e-a : wakati uliopita

***Zoezi la 7: Nyambua vitenzi vifuatavyo kwa kuonyesha kiambishi awali na kikanushi.***

**Mfano:** Nilipanda miti mwezi jana.

**Ni**-li-pand-a

Ni: kiambishi awali

1. Yeye **anafanya** kazi za umuganda kila mwisho wa mwezi.
2. Wanafunzi **watapanda** miti kwenye shule zao.
3. Wewe **hujui** umuhimu wa barabara?
4. **Hakuna** mtu mwingine atakayetujengea nchi yetu
5. **Ulikata** nyasi nyuma ya nyumba yako.
6. **Ninapenda** kumshukuru mgeni rasmi.
7. Mimi **siwezi** kuharibu mazingira.
8. **Mtafanya** mazoezi haya katika makundi yenu.
9. **Tutajenga** taifa letu tukifanya kazi kwa bidii.
10. Kidole kimoja **hakivunji** chawa

***Zoezi la 8: Onyesha nyakati za vitenzi zilizotumiwa katika sentensi zifuatazo:***

**Mfano:** Tunafanya kazi kwa bidii: Wakati uliopo.

1. Tuliwashukuru kwa kushiriki katika kazi hii.
2. Wanafunzi wanasafisha darasa lao.
3. Dada yangu husoma katika kidato cha nne.
4. Meya ametuhutubia kuhusu umuhimu wa kazi za umuganda.
5. Nyasi na miti huzuia mmomonyoko wa ardhi.
6. Vijana wenu watakuwa mashujaa wakifanya kazi kwa nguvu.
7. Watoto wote wanapaswa kuenda shuleni.
8. Tunalala kwenye vitanda vinavyotandikwa vyandarua.
9. Hakuonyesha uvivu hata kidogo.
10. Hajafika mjini Kigali.

***Zoezi la 9: Badilisha sentensi zifuatazo katika nyakati ulizopewa:***

1. Barabara hii itatusaidia katika nyanja mbalimbali (uliopita).
2. Kitabu hiki kiliandikwa na walimu wa Kiswahili (uliopo).
3. Rwanda yetu itajengwa na sisi wenyewe (uliotimilika).
4. Wavulana na wasichana wote watapaswa kwenda shuleni(uliopo).
5. Wanafunzi walisomea darasani(mazoea).
6. Baba atalipa fedha za bima ya afya (uliotimilka).

## 10.4. Matumizi ya Lugha: Mambo Muhimu katika Hotuba

***Zoezi la 10: Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa hapo chini***

- **Mambo ya kuzingatia katika hotuba:**

Hotuba ni maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya kundi la watu. Hotuba inaweza kutolewa kwa madhumuni ya kutaka kuhimiza kazi, kufanya kampeni fulani, kutoa taarifa fulani kwa watu. Aina za hotuba ni:

a. Mahubiri: Ni hotuba za mafundisho ya kidini, zinazotolewa makanisani, misikitini, n.k.

b. Hotuba za kisiasa: Ni hotuba zihusuzo taarifa ya serikali kama vile kuwahimiza watu na kuwaalika kutenda jambo fulani, n.k.

c. Mihadhara: Ni hotuba au mafundisho ya mwalimu shuleni anapofundisha kundi la wanafunzi na hasa wanafunzi wa vyuo vikuu.

**Sifa za hotuba:**

- Ukweli wa habari na taarifa
- Kujua vizuri aina ya watu unaowatolea hotuba, umri wao, kazi zao, n.k.
- Ufasaha wa lugha ili iweze kupendeza na kueleweka vizuri
- Nidhamu au adabu njema ya mzungumzaji mwenyewe asimamapo mbele ya watu
- Mantiki nzuri au mfuatano mzuri wa mawazo
- Sauti ya kusikika vizuri
- Kuvaa vizuri.

**Maswali**

1. Eleza maana ya hotuba.
2. Hotuba hutolewa kwa lengo gani?
3. Eleza aina za hotuba.
4. Eleza sifa muhimu za hotuba.

## 10.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

***Zoezi la 11: Jadili "Umuhimu wa hotuba"***

## 10.6. Kuandika: Utungaji wa Hotuba

***Zoezi la 12: Wewe ni kiranja mkuu wa wanafunzi katika shule yako. Tunga hotuba kwa ajili ya kufunga mwaka wa shule.***

# SOMO LA 11: MUUNDO WA HOTUBA

***Zoezi la 1: Jibu maswali yafuatayo:***

1. Uliwahi kusoma Hotuba yoyote?
2. Wahuhusika wake walikuwa wapi? Eleza
3. Ni mafunzo yapi uliyofaidika na hotuba hiyo?
4. Kuna uhusiano wowote uliopo kati ya hotuba hiyo na kichwa cha habari hapo chini?

## 11.1. Kusoma na ufahamu: Hotuba ya Mkuu wa Kamisheni ya Umoja na Maridhiano

*Soma hotuba ya Mkuu wa Kamisheni ya Umoja na Maridhiano wakati wa kuanzisha Utaratibu wa "Ndi Umunyarwanda"*

Mheshimiwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Waheshimiwa wengine katika ngazi zinazohusika, Mabibi na Mabwana, Hamjambo nyote! Ninayo furaha kubwa ya kuwakaribisha hapa kwenye Uwanja wa Amahoro. Watu wote walionitangulia walizungumzia mambo mengi kuhusu umoja wetu kama wananchi wenye utamaduni mmoja na mitazamo sawa ya kujiendeleza na kujitegemea. Kwa kuwa umoja wetu kama Wanyarwanda ndio nguvu na nguzo ya maisha yetu, tumekutana hapa leo hii ili tuweze kuanzisha rasmi utaratibu muhimu wa "Ndi Umunyarwanda".

Waheshimiwa mlioshiriki katika tendo hili maalumu la "Ndi Umunyarwanda", ningependa kuwakumbusha kwanza kuwa nchi yetu iliteseka miaka mingi kutokana na ubaguzi ambao uliharibu watu na vitu vyao pamoja na mali ya nchi.

Hotuba za ubaguzi zilitungwa mara nyingi na mwishowe zilisababisha ukimbizi na vifo vya Wanyarwanda wengi. Mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi mnamo mwaka 1994 yalikuwa kilele cha ubaguzi huo. Idadi ya watu zaidi ya milioni moja waliuawa na wananchi wenzao kwa uchungu unaopita kiasi. Baadaye, nchi ilikuwa na matatizo mengi.

Mheshimiwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,Waheshimiwa wengine katika ngazi zinazohusika, Mabibi na Mabwana!

Wahenga walisema, "Umoja ni nguvu." Hivyo basi, Serikali ya Rwanda iliamua kujengea nchi yetu kwenye msingi wa umoja na maridhiano na hivi sasa imefanikiwa. Utaratibu wa Ndi Umunyarwanda tunaouzungumzia leo, unahusu uimarishaji wa umoja wa Wanyarwanda ambao unatuwezesha kuwa na umoja na mshikamano katika namna endelevu. Katika utaratibu huu kila mwananchi atajitambulisha kwanza kama Mnyarwanda kuliko kujitambulisha kwa utambulisho mwingine wowote. Hivi ni kusema kwamba Mnyarwanda ni mtu mmoja na ni lazima awe na mwelekeo mmoja kwa kufuatilia amani, usalama na maendeleo.

Malengo ya Ndi Umunyarwanda ni kuwapa Wanyarwanda fursa ya kufikiria Unyarwanda yaani uhusiano wao, utamaduni wa kupenda nchi yao, kuilinda nchi na kuiendeleza kwenye viwango vya juu kadiri iwezekanavyo. Vilevile kila Mnyarwanda anatarajiwa: kulinda usalama, kuwasaidia watu ambao hawajiwezi kama vile watoto yatima, wazee, walemavu na maskini. Hili linafanikishwa kwa kuhakikisha makundi haya yote yanapata huduma za shule, afya, chakula, na kuwapatia makazi.

Mheshimiwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mkuu wa Mkoa, Waheshimiwa wengine katika ngazi zinazohusika, Mabibi na Mabwana,

Kila Mnyarwanda anapaswa kuzingatia uhusiano wetu kama wananchi kwa kuendeleza umoja wetu, kupenda kuilinda na kuiendeleza nchi, na kujiepusha na ubaguzi wowote ili tuwe na amani ya kudumu. Ninamalizia kwa kuwashukuru nyote. Asanteni sana kwa kushiriki.

***Maswali ya Ufahamu***

1. Nani aliyekuwa mgeni wa heshima?
2. Mkutano ambamo kulitolewa hotuba hii ulifanyikia wapi?
3. Taja vyeo vya waheshimiwa waliokuwepo katika mkutano huo.
4. Maneno "Mnyarwanda ni mtu mmoja" yanamaanisha nini katika kifungu cha habari?
5. Kwa nini Serikali ya Rwanda iliamua kujenga nchi kwenye msingi wa umoja na maridhiano?
6. Kulingana na historia ya Rwanda, kwa nini ubaguzi ni jambo baya sana?
7. "Umoja ni nguvu." Husisha methali hii na kifungu ulichosoma.

8. Utaratibu wa Ndi Umunyarwanda una malengo gani?

9. Taja mambo muhimu matatu ya kimaendeleo ambayo hufanywa katika utaratibu wa Ndi Umunyarwanda.

10. Kwa ufupi, utaratibu wa Ndi Umunyarwanda unahusu nini?

## 11.2. Msamiati kuhusu Hotuba

***Zoezi la 2: Jaza sentensi ambazo zinafuata kwa kutumia maneno haya: usalama, maendeleo, umoja, maridhiano, mauaji ya kimbari, mahakama za Gacaca, Wanyarwanda, Mheshimiwa, hotuba, wananchi.***

1. Nitatunga……. nzuri siku ya kuanzisha rasmi Shirika la Umoja na Maridhiano shuleni kwetu.

2. Kwa minajili ya……… wa Rwanda, tunapaswa kuishi kwa amani na kuilinda nchi yetu ili maisha yaendelee kuwa mazuri.

3. Wanajeshi, askari polisi, askari wa mgambo pamoja na watu wengine wanatarajiwa kuungana mkono kwa kulinda ……………..

4. Ndi Umunyarwanda ni utaratibu wa kutilia nguvu umoja wa … …na kuimarisha maridhiano kati yao.

5. Wafanyadhambi walikuwa wengi baada ya mwaka wa 1994 lakini … …zilifanya kazi nzuri kwa hali ya juu.

6. Watu zaidi ya milioni moja waliuawa katika ……… dhidi ya Watutsi.

7. Kutokana na kwamba nchi yetu iliumia sana, ni lazima Rwanda ijengee msingi wake kwa siasa ya umoja na ………..

8. Wahenga walisema jambo zuri na imara sana kwamba … ………..ni nguvu.

9. Taratibu kadhaa za ngazi ya kitaifa huanzishwa mara nyingi na … ……….Rais.

10. Ni jambo muhimu sana kujua kwamba maendeleo yangu, yako na yake ndiyo … ………ya nchi yetu.

***Zoezi la 3: Husisha maneno katika sehemu A na maana yake katika sehemu B***

| A Neno | | B Maana ya neno |
|---|---|---|
| 1.Hotuba | | a.Hali ya kuwa pamoja, ushirikiano |
| 2.Umoja | | b.Neno linalotamkwa kabla ya kutaja jina la mtu maarufu |
| 3.Maridhiano | | c.Namna maalumu ya kutekeleza jambo |
| 4.Mheshimiwa | | d.Kusema maneno au kuonyesha ishara ya kufurahia jambo la wema unalofanyiwa, kutoa shukrani |
| 5.Utaratibu | | e.Kuanzisha jambo au kitu kwa kufuata utaratibu au kanuni zilizowekwa |
| 6.Kushukuru | | f.Mahali ambapo kesi na mashtaka mbalimbali husikilizwa na kuamuliwa, korti au baraza |
| 7.Kuanzisha rasmi | | g.Mwafaka unaofikiwa baina ya mataifa au makundi yaliyokuwa yanapingana na kutofautiana kiitikadi, maafikiano |
| 8.Mahakama | | h.Hali ya kuwa na maadili au mwenendo mwema kulingana na utamaduni, mila na desturi za Wanyarwanda |
| 9.Unyarwanda | | i.Mfumo wa kijamii wa kutoa huduma kwa upendeleo kwa misingi ya rangi, jinsia, kabila, n.k. |
| 10.Ubaguzi | | j.Maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mmoja mbele za watu |

## 11.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi Awali Utendewa na Mzizi

***Zoezi la 4: Onyesha viambishi utendewa katika vitenzi ambavyo vimepigiwa msitari:***

**Mfano:** Jana tuliufanya mtihani wa Kiswahili.

**Jibu:** tu-li-**u**-fanya

1. Sisi <u>tumeuona</u> mwongozo wa wanafunzi.
2. Watu wakubwa kama wale hawapendi vyakula lakini vinywaji <u>wanavipenda.</u>
3. Walinzi walitafuta mpira msituni hadi <u>waliuona.</u>
4. Mvulana huyo <u>aliyamwaga</u> maziwa bila yeye kujua.
5. <u>Nitalitembelea</u> bara la Amerika mwaka kesho.

6. Wanafunzi wana vitabu vipya, walivitoa maktabani leo.
7. Hali ya hewa barani Afrika ni nzuri kiasi kwamba tunaifurahia sana.
8. Nchi ya Rwanda ina milima mingi na milima hiyo inayamiliki mabonde ambayo yanavutia sana.
9. Tunampenda mwalimu wetu wa Kiswahili kwani ni mwerevu na mpole.
10. Kiti hicho nilikikalia kikaniangusha mara kwa mara.

## Maelezo muhimu: Mzizi

Mzizi ni umbo la msingi la kitenzi ambalo ndilo kiini cha kitenzi hicho na hutumika kama msingi wa kuundia maumbo mengine yanayohusiana na kitenzi hicho. Mzizi pia ni mofu ya mwisho ambayo haiwezi kugawanywa katika mofu nyingine. Sehemu hii ndiyo inabeba dhana ya kitenzi. Katika lugha ya Kiswahili kuna mizizi ya vitenzi vya silabi moja na mizizi ya vitenzi vyenye mizizi zaidi ya silabi moja.

**Mifano ya mizizi ni kama:**

1. Kucheza : ku-*chez*-a — Kuenda : ku-*end*-a
2. Kuimba : ku-*imb*-a — Kucheka : ku-*chek*-a
3. Kupiga : ku-*pig*-a — Kula : ku-*li*-a
4. Kunya : ku-*nye*-a — Kuzaa : ku-*zal*-a

Kwa kupata mzizi wa kitenzi cha silabi moja, tunaweka kitenzi hicho katika hali ya kutendewa. **Kwa mfano:** Kula: ku-li-wa, kuja: ku-ji-wa.

Pengine, vitenzi vya silabi zaidi ya moja hutafutiwa mizizi kwa kutafuta silabi mbili tu za shina. Lakini vitenzi vya mkopo hufuata mtindo wake kwani tunateua shina zima hivi tukitoa kiambishi ngeli –ku-.

***Zoezi la 5: Toa mizizi (kiini) ya vitenzi vilivyopigiwa msitari katika sentensi zifuatazo:***

1. **Nimekula** chakula changu cha mchana.
2. Wanaume na wanawake **wanaweza** kusoma sawasawa.
3. Walimu wetu **walitembelea** mbuga ya wanyama ya Akagera.
4. Watoto wote siku hizi **wanavaa** viatu shuleni.
5. Babu na Shangazi **watakuja** kwetu wiki kesho kutwa.

6. Mvua **inanyesha** na nyinyi **mnafurahi.**

7. Wao **wanataka** kunywa maziwa mkahawani kule.

**8.** **Tunasonga** mbele na masomo yetu.

9. Matunda haya **yalivaa** kwelikweli.

10. Magari **yanatembea** kwa wingi mjini Kigali na hata nje yake.

## 11.4. Matumizi ya Lugha: Sifa za Hotuba

***Zoezi la 6: Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali hapo chini***

- **Muundo wa hotuba**

**Hotuba ina sehemu zifuatazo:**

1. Anwani: Anwani, mada au kichwa cha hotuba huchukua mada ya hotuba. Hiki ndicho kichwa chake hotuba.

Mfano: Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Rwanda  katika Sikukuu ya Mashujaa.

2. Utangulizi: Mazungumzo kwenye utangulizi yanatoa mwangaza ama picha ya habari inayokusudiwa kuzungumzwa. Anza hotuba yako kwa kuwatambua waliohudhuria mkutano). Wataje kwa majina au vyeo vyao kuanzia yule wa cheo cha juu hadi wa chini, mabibi na mabwana. Kumbuka kwamba huhitaji kuwasalimia. Kuwatambua kwa vyeo vyao ya pekee kunatosha.

Mfano: Waziri wa Elimu, Gavana wa Jimbo la Kusini, Mkuu wa Wilaya ya Nyanza, Wanachama wa kikundi hiki cha Elimu Bora, mabibi na mabwana. Ni matumaini yangu kwamba nyote mna afya nzuri.

3. Mwili/Kiini: Hakikisha kuwa kuna mtiririko wa hoja kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ujumbe wako wote unapaswa kuwa katika usemi halisi wala si wa taarifa. Panga mawazo kufuatana na uzito ama umuhimu wake. Wazo muhimu lazima lianze kuzungumziwa kwa ukamilifu halafu lifuatiwe na mawazo mengine, nayo kwa kikamilifu.

4. Mwisho: Hapa mazungumzo yajumuishe mawazo yote yaliyozungumziwa kwa maelezo fasaha. Ni vizuri kwa hotuba kufungwa kwa picha inayofanana na ile ya utangulizi ili kumbukumbu ya habari ibaki katika mawazo ya wasikilizaji.

- **Sifa za hotuba**

**Hotuba huzingatia mambo haya:**

a. Ukweli wa habari na taarifa: Ni lazima mhutubi ahakikishe kuwa yale anayozungumzia yana uhusiano na ukweli.

b. Ufasaha wa lugha: lazima mhutubi kutumia lugha fasaha, nzuri, safi na yenye kusikika vizuri kwa kila msikilizaji. Si vizuri kutumia lugha ya mafumbo.

c. Mantiki nzuri: Ni lazima kuwe na mfuatano mzuri wa mawazo au fikra.

d. Nidhamu: Yaani adabu njema ya mzungumzaji mwenyewe asimamapo mbele ya watu.

e. Sauti ya kusikika wazi pamoja na ishara zinazoeleweka na zinazohusiana na yasemwayo. Ishara hizo si za lazima iwapo hotuba inatolewa kwa njia ya redio.

***Maswali***

1. Hotuba inatarajiwa kuwa na sehemu zipi?
2. Katika kuanza hotuba yake, mhutubi hufanya nini?
3. Habari yenyewe hutolewa katika sehemu gani? Kwa nini?
4. Mwisho wa hotuba una maumbile gani?
5. Taja sifa tatu ambazo hotuba nzuri huzingatia.

## 11.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

***Zoezi la 7: Kwa kushirikiana na wenzako, jadili mambo yafuatayo:***

1. Hotuba inaweza kuharibu na kujenga taifa.
2. Mnyarwanda ni mtu mmoja.

## 11.6. Kuandika: Ufupishaji wa Hotuba

***Zoezi la 8: Soma hotuba iliyopo hapo juu na uifupishe katika aya moja yenye mistari tisa.***

## SOMO LA 12: UFUPISHO

***Zoezi la 1: Jibu maswali haya.***

1. Je, ufupisho ni nini?
2. Ufupisho unawasaidia kwa namna gani kama wanafunzi?
3. Hatua gani ambazo huzingatiwa katika kuandaa ufupisho wa habari?

### 12.1 Kusoma na Ufahamu: Hotuba ya Daktari Mkuu

*Soma hotuba ya Daktari Mkuu wa Kituo cha afya kwa wanafunzi wa shule ya Sekondari, hafalu jibu maswali yaliyotolewa hapo chini*

Mheshimiwa Mkurugenzi wa shule, Mwenyekiti wa kamati ya shule; Msimamizi wa masomo,

Afisa wa nidhamu, waheshimiwa walimu, Wanafunzi washiriki wa klabu ya usafi na mazingira kwenye shule hii, Mabibi na mabwana, Hamjambo? Kwanza ninayo furaha kupewa nafasi hii ili niwaelezee kinagaubaga juu ya umuhimu wa kushirikiana sisi sote katika kulinda na kufanya usafi wa mazingira. Hii inatusaidia sana kupiga vita uchafu pamoja na madhara yake hapa shuleni hata nyumbani kwetu. Wahenga wanasema: Kinga ni bora kuliko tiba. Hiki tunachokifanya ni kitendo cha kudumu.

Kama mnavyofahamu, watu wanakumbwa na magonjwa ya kuharisha yanayosababishwa na uchafu. Uchafu huu unajitokeza hata majumbani kutokana na vitendo vya watu wasiofanya usafi na kutunza mazingira ya nyumbani. Kuna wanaoacha vyombo bila ya kuviosha kwa maji safi, hawakati nyasi na vichaka vinavyozunguka makazi yao. Aidha watu hawa hawaondoi vidimbwi kando na nyumba na wanarundika maganda ya matunda bila ya kuyatupa jalalani. Mara nyingi, watu hawa hawanywi maji yaliyochemshwa au kuchujiwa vizuri wala kuhifadhiwa katika vyombo safi. Zaidi ya hivyo, inawezekana kuwa watu hawa hawapigi mswaki kabla ya kulala ama baada ya kula. Mambo hayo yasiofaa yanapaswa yarekebishwe tangu leo!

Kulingana na uharibifu wa mazingira, kuna watu wanaochoma taka na kutoa moshi ukapanda angani na kuliharibu sana anga hata kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa. Hili ni tatizo kubwa linalohuzunisha ulimwengu mzima. Nafikiri kati yetu hakuna mtu ambaye hapendi kuwa na maisha mema. Tushirikiane sana kwa kufanya usafi na kuyatunza mazingira yetu. Kulinda usafi wa mazingira kuwe jukumu la kila mtu. Barabara zetu ziwe na usafi, busitani nazo zisafishwe, mahali ambapo kuna mikusanyiko ya watu kuwe na mapipa ya taka na kutumiwa vizuri.Kwa hiyo tujijengee utamaduni wa kufanya usafi.

Kabla ya kumaliza, naomba kila mtu awe makini kuhusu suala la usafi wa mazingira yetu kwa kufanya bidii na kujitolea pale inapowezekana kurekebisha yote yaliyoharibika. Waswahili husema "Usipoziba ufa utajenga ukuta" na "Maji yakimwagika hayazoleki." Nina imani na matumaini kuwa sisi sote tutashirikiana katika kufanikisha usafi wa mazingira yetu kwani tunaamini kuwa"Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu." Msisahau kuwa "Usafi ni Tabia." Fanyeni usafi kwa njia zozote ziwezekanazo kwani usafi wa mazingira ni zoezi endelevu na msingi wa afya na maisha mema.

Asanteni sana. Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza.

***Maswali ya ufahamu***

1. Eleza madhumuni ya hotuba hii.
3. Hadhira hii imetolewa mwito gani?
4. "Usafi wa mazingira ni nini' Jadili.
5. Kwa nini watu wanapaswa kunawa mikono kabla na baada ya kula.
6. Eleza tatizo linaloweza kujitokeza kwa watu wasiotumia vyoo.
7. Ni kwa namna gani wachoma taka huharibu mazingira?
8. Ni madhara gani yanayosababishwa na kitendo cha kuchoma taka ngumu?
9. Eleza maana ya methali hii:
   (i) Maji yakimwagika hayazoleki
   (ii) Usipoziba ufa utajenga ukuta.
   (iii) Kinga ni bora kuliko tiba
10. "Kinga ni bora kuliko tiba" Eleza uhusiano uliopo kati ya methali hii na kifungu ulichokisoma hapo juu.

## 12.2 Msamiati kuhusu Hotuba

***Zoezi la 2: Unganisha maneno ya sehemu A na maana zake kutoka sehemu B***

| Neno | Maana |
|---|---|
| 1. Usafi | a. Maji machafu ya mvua yasiyotiririka ambayo yametuama. |
| 2. Mazingira | b. Osha meno kwa brashi na maji safi |
| 3. Kuzoleka | c. Kitu cha kuwekea taka |
| 4. Kipipa | d. Uchafu |
| 5. Taka | e. Ondoa uchafu ama takasa. |
| 6. Pipa la taka | f. Pipa dogo |
| 7. Kusafisha | g. Maji yasiyokuwa na uchafu |
| 8. Maji safi na salama | h. Kukusanya tena vitu vilivyomwagika. |
| 9. Kupiga mswaki | i. Kuwa bila uchafu |
| 10. Kidimbwi | j. Hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu anapoishi. |

***Zoezi la 3: Tunga sentensi zenye maana kamili kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. Shule
2. Bidii
3. Kupiga vita
4. Uchafu
5. Nyasi
6. Kutupa
7. Jalala
8. Maganda ya matunda
9. Vyombo vya mekoni
10. Kulinda mazingira

***Zoezi la 4: Jaza sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. Kiongozi wa zahanati aliendesha hotuba kuhusu…………..(Usafi wa mazingira,ugonjwa wa zinaa, ufanyaji biashara)
2. Mtu akiambukizwa magojwa huenda zahanati kupata………….(tiba, chakula, maji)
3. Kila familia inalazimishwa kuwa na……………. chenye vipimo sahihi( Choo,chochote, chake)
4. Maji huchemshiwa katika maziga……vyema.(iliyosafishwa, isiyosafishwa,

   isiyo kuwa na masizi)
5. Viongozi wa shule wote na wanafunzi wao …………….. kutunza usafi wa mazingira shuleni (wanashirikiana,wanapendana,wanalinda)
6. Inamlazimu mtu yeyote kunywa maji safi na…………(salama,salimu,salamati)
7. Si vizuri kurundika maganda mahali……………….(chochote,popote,lolote)
8. Taka huhifadhiwa …………………...(jalalani,jalbe,jalada)
9. Wanafunzi watakaotupa karatasi ndani ya ……………..wataadhibiwa .(jalala,busitani,jaa)

## 12.3 Sarufi : *Uambishaji wa Vitenzi: Viambishi katika Vitenzi na Viambishi tamati*

***Zoezi la 5: Chunguza vizuri sehemu ya vitenzi vilivyoaandikwa kwa rangi, iliyokoza na kupigiwa mstari***

1. **Al**itup**i**a watoto chupa tupu barabarani.
2. Usafi **uki**fany**ik**a ifaavyo,watu watakuwa na afya nzuri.

- A-li-tup-i-a: A kiambishi awali nafsi ya tatu.

  -li-:Kiambishi cha kati wakati,wakati uliopita.

  -tup-:mzizi wa kitenzi

  -i-: kiambishi tamati kauli tendea

  -a: kiishio

U-ki-fany-ik-a: U: kiambishi awali nafsi ya pili umoja.

Ki: kiambishi cha hali ya masharti

-fany-: Mzizi

-ik-:Kiambishi tamati kauli tendeka

-a: kiishio.

*Maswali:*

**1. Soma sentensi zifuatazo kisha uonyeshe viambishi vya vitenzi vilivyopigiwa mistari.**

a. Usafi unafanyika mahali popote nchini Rwanda.

b. Alitupia watoto chupa tupu la maji barabarani na kuadhibiwa na polisi.

A. Kama vile viambishi tamati huambishwa baada ya mzizi wa neno navyo ni vya aina mbalimbali.

***Soma maelezo muhimu kisha ujibu maswali husika.***

- Maelezo muhimu kuhusu viambishi tamati na viishio

Viambishi tamati ni viambishi ambavyo hufuatana na mizizi ya vitenzi. Viambishi hivi vimo katika aina mbalimbali kutokana na hali au kauli ya tendo.

**Zifuatazo ni baadhi ya kauli za vitenzi:**

- Kutenda: Som-**a**
- Kutendwa: Som-**wa**
- Kutendewa: Som-**ew**-a
- Kutendea: Som**-e**-a
- Kutendesha: Som-**esh**-a
- Kutendeka: Som-**ek**-a

- Viambishi tamati vya Kauli ya kutenda ambavyo hueleza jambo ambalo mtendaji alitendalo.

***Mfano:*** Ni vizuri kukat**a** nyasi na vichaka vilivyopo kando na makazi.

Viambishi tamati vya kauli ya kutendwa huonyesha kuwa tendo linapokewa na mtu / watu au kitu fulani. Vina maumbo ya **[-w-,-lew-,-liw-]**

***Mfano:*** Maji huhifadhi***w***a katika pipa safi.

Ujumbe kuhusu usafi, ulito***lew***a na kuenea nchini kote na

kukuba***liw***a na kila mtu.

- Viambishi tamati vya kauli ya kutendewa.kauli hii huonyesha tendo linalotendeka kwa niaba ya mhusika fulani. Maumbo ya viwakilishi vyake huwa ni kama**[-iw-,-ew-, n.k]**

***Mfano:*** Maji yanayomwagika hayawezi kuzol***ewa*** tena.

Maji ya kunywa huchemsh**iw**a katika maziga safi sana.

- Viambishi tamati vya kauli ya kutendea huonyesha kuwa tendo hutendwa kwa faida ya mtu au kitu kingine. Kauli hii ina muundo wenye viambishi vya

**{-i-,-e-,-li-,-le-}**

***Mifano:*** Msipende kutup**i**a watoto chupa tupu za maji ama juisi.

Inakatazwa kuchoma wala kuchom**e**a taka mahali popote.

Watu wote wakimbi**li**e mbali na uchafu ili wawe na maisha bora.

- Viambishi tamati vya kauli ya kutendeka ni vile vinavyoonyesha kuwa kitendo fulani hufanyika na huwakilishwa na maumbo ya **[-ik-;-ek-;-lik,...]**

***Mfano:*** **Mazingira** huharibi***ik***a kwa kuchimba madini ovyo ovyo.

**Maji** yakimwag***ik***a hayazo***lek***i

**Makala** haya yanasom***ek***a sana

Viambishi tamati vya kauli ya kutendeana huonyesha kuwa wahusika wanatendeana kitendo fulani katika wakati mmoja. Hali hii huwakilishwa na kiambishi –***an***-.

***Mfano:*** Sisi sote tushiriki***an***e kwa kuendeleza usafi wa mazingira yetu.

Baba na mama wanapend**an**a sana.

**Viishio au vimalizio: Ni irabu au vokali zinazijitokeza kwenye miisho ya vitenzi. Viishio hivyo vinaweza kuwa : –a, -*u* ama –i**

Wasichana na wavulana wanafany**a**usafi.

**Kuharibu mazingira kunasabisha madhara makubwa.**

**Karake atarudi kesho**

**Ninafikiri kazi ilianza jana..**

***Zoezi la 6: Kulingana na maelezo uliyoyasoma hapo juu ,onyesha viambishi vya mwisho pamoja na viini vya vitenzi vifuatavyo:***

***Mfano:***

1. Haribika :

harib— Mzizi wa kitenzi

**-ik—Kiambishi tamati -tendeka**

**-a** - Kiishio au mwisho wa kitenzi haribika

1. Piga
2. Hifadhiwa
3. Kimbilia
4. Shirikiana

5. Chemshiwa
6. Mwagika
7. Katwa
8. Timizika
9. Chomwa

***Zoezi la 7:* Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo:**

Washirikiane, huhifadhiwa, kukatwa; viondolewe, kutupia; kuharibika;unasababisha;

wanaochoma.

1. Watu ……………….kulinda usafi wa mazingira ili maisha yao yawe bora.
2. Maji safi na salama …………….ndani ya pipa safi sana.
3. Si vizuri ……………. watoto chupa tupu kwenye barabara.
4. Nyasi na vichaka vinapaswa………………….vinapokuwa kando na makazi kwa faida mbalimbali za kiafya.
5. Vidimbwi ………………. kwa minajili ya usafi.
6. …………………..hali ya hewa kunatishia ulimwengu mzima.
7. Watu……………….taka ngumu wanaharibu mazingira.
8. Uchafu ………………….magonjwa ya kuharisha.

## 12.4 Matumizi ya Lugha: Ufupisho

***Zoezi la 8: Soma kifungu kisha ujibu maswali.***

### Kinga ni Bora Kuliko Tiba

Usafi wa mazingira ni kitendo cha kudumu kinacholinganishwa na msingi wa maisha mema ya binadamu. Kwa hiyo ni sharti kwa kila mtu ili aishi vyema.Watu wanapaswa kufanya usafi mahali popote wanapoishi. Inawalazimu tena watu wawe na utamaduni wa kufanya usafi kama wanavyosema kuwa "Usafi ni tabia".

Watu wamedokezwa kuwa si vizuri kuchoma taka kwani wanapochoma wanaharibu anga na kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa yanayoleta maafa ya kuenea kwa jangwa na ukosefu wa mvua. Kwa lugha ya mkato, aliiambia hadhira kuwa, maji yakimwagika hayazoleki na kuwa watu wote wakishirikiana wanaweza kutimiza lengo la kupiga vita uchafu wakajenga utamaduni wa kulinda usafi na mazingira. Kwa hiyo kufanya usafi wa mazingira ni wajibu wa kila mtu yeyote ili ulimwengu mzima uwe na usalama kiafya.

1. Kifungu hiki kinahusu nini?

2. Bainisha mambo makuu yanayozungumziwa katika kifungu hiki.

3. Linganisha kifungu hiki na hotuba ya Daktari Mkuu wa Kituo cha Afya kwa wanafunzi wa shule za Sekondari.

***Zoezi la 9: Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini***

- **Maana ya ufupisho**

Ufupisho ni ustadi ama ufundi wa kuielewa habari na kuweza kuieleza tena habari hiyo kwa maneno machache kuliko yaliyotumiwa awali. Anayeyaeleza hapunguzi hata kidogo kulingana na maana yake ya asili.

Kufupisha habari yoyote inamlazimu kuisoma sana na kuweza kuisimulia kwa mambo machache bila ya kupotosha ama kuongeza kuhusu maana yake ya awali. Kazi hii hupima kiwango cha ufahamu wa mtu katika kazi za utungaji.

Kufupisha habari hulingana na maelezo ya yule aliyeandaa kazi hiyo.

Kuna wanaoomba kufupisha habari kulingana na idadi fulani ya mambo, aya fulani, idadi ya sentensi fulani lakini kwa ujumla ufupisho mzuri unakuwa theluthi(1/3)ya habari ya awali.

- Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kufupisha habari

    1. Kusoma habari husika zaidi ya mara moja.
    2. Chagua mawazo makuu yanayojitokeza katika habari kisha uyaandike
    3. Andika ufupisho wako kwa kuzingatia kwa makini mawazo makuu
    4. Zingatia urefu kulingana na maelezo uliyopewa.

- Hatua za kufanya ufupisho:

1. Lazima kukisoma na kukielewa kifungu kilichotolewa
2. Chagua taarifa na maneno maalum
3. Unganisha mawazo makuu na habari ya awali na yaeleweke kwa kudondoa.
4. Muhtasari kama inavyotakiwa katika lugha inayoeleweka.
5. Linganisha usawa wa ufupisho na habari ya awali. Mara nyingi huwa 1/3 wa habari ya awali.

***Maswali***

1. Eleza hatua za kufanya ufupisho.
2. Eleza mambo muhimu yanayozingatiwa wakati wa kufupisha habari.
3. Kwa nini anayetarajia kufupisha habari huisoma zaidi ya mara moja?

***Zoezi la 10: Tumia baadhi ya semi hizi kwa kujaza nafasi wazi:***

**tupige vita; kupiga mswaki, fanya bidii, ufanye mbinu zote, fanya juu chini, kuwa na imani**

1. Usipo………………..hutatimiza lengo lako.
2. Ali……………..lakini hakushinda vizuri.
3. Sisi sote …………. uchafu ili tuwe na afya njema.
4. Ulimwengu mzima lazima………… kulinda mabadiliko ya hali ya hewa.
5. Inalazimu ……………….mtu akiamka, baada ya kula na kabla ya kulala.
6. Mkurugenzi ali ………. ya.kuwa wanafunzi wanafanya usafi.

***Zoezi la 11: Toa kinyume cha maneno yafuatayo:***

1. Uchafu ≠
2. Shindwa ≠
3. Lala ≠
4. Huzunika ≠
5. Mwaga ≠
6. Acha ≠
7. Afya mbaya ≠
8. Kipipa kichafu. ≠

***Zoezi la 12: Ambatanisha maelezo ya safu A na maneno kutoka safu B ili kuunda sentensi kamili.***

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| 1. Uharibifu wa mazingira | a. Kufanya kazi kwa bidii |
| 2. Ukosefu wa usafi husababisha | b. Kunahuzunisha ulimwengu mzima. |
| 3. Kutimiza lengo | c. Magonjwa ya kuharisha |
| 4. Kukata vichaka kando na nyumba | d. Kwa kufanya usafi. |
| 5. Wavulana na wasichana | e. Kunakinga maradhi kama Malaria |
| 6. wanashirikiana | f. cha kudumu |
| 7. Mojawapo ya wadudu waishio ndani ya vidimwi | g. Mbu |
| 8. Maganda yakikusanyika sehemu moja hufanya | h. Rundo |
| 9. Usafi wa mazingira ni kitendo | |

## 12.5 Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

***Zoezi la 13: Jadili mambo yafuatayo kwa kuzihusisha methali zifuatazo na mazingira ya afya na ya shuleni ili kudhihirisha matumizi yake.***

1. Usafi ni tabia
2. Maji yakimwagika hayazoleki
3. Kinga ni bora kuliko tiba
4. Usipoziba ufa utajenga ukuta
5. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

## 12.6 Kuandika : Ufupishaji wa Hotuba

***Zoezi la 14: Toa ufupisho wa kifungu cha habari ulichokisoma hapo juu kwa theluthi (1/3) ya kifungu cha awali.***

### TATHMINI YA MADA YA 3

Wewe ni Mkurugenzi Mkuu wa Masuala ya Jinsia katika Wizara ya Jinsia na Maendeleo ya Jamii. Andika hotuba utakayoisoma kwenye sikukuu ya Wanawake kuhusu **"Ushirikiano wa kijinsia katika malezi ya watoto"** kisha, dhihirisha mambo yafuatayo kutokana na hotuba uliyoiandika:

1. Hotuba yako imeangukia katika kundi gani la aina za hotuba? Eleza, maoni yako.
2. Ni hatua zipi ulizozizingatia katika kuiandaa hotuba yako?
3. Chagua vitenzi vitano ulivyovitumia katika hotuba yako, kisha bainisha viambishi vyake.
4. Fupisha hotuba yako ili iwe 1/3.
5. Bainisha njia muhimu zinazopitiwa katika ufupisho.

# MADA KUU YA 4:
## UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO

# MADA KUU YA 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO

## MADA NDOGO: MIDAHALO NA MIJADALA

**Uwezo Upatikanao katika Mada:** Mwanafunzi ataweza kuongoza midahalo na mijadala na kushiriki katika kazi za majadiliano kwa kuzingatia mada zilizotolewa kujadiliwa na kujua jinsi ya kuchambua maneno ya Kiswahili kwa kutumia njia ya uambishaji.


**Malengo ya Ujifunzaji:** Baada ya kujifunza mdahalo, mwanafunzi ataweza kutofautisha pande zinazoshiriki kwenye mdahalo na mjadala kama mtetezi au mpinzani, kutoa suluhisho katika majadiliano kwa kutetea hoja zinazomkera, atatumia lugha sahihi na yenye kuvutia, kutumia ishara za mwili kulingana na hoja inayotolewa na kutoa hitimisho kwa kuzingatia maoni tofauti yaliyotokea kwa upande wa utetezi na upande wa upinzani.

**Kidokezo:**

1. Uliwahi kushiriki katika mazungumzo na watu wengine?
2. Kama ni kweli, mazungumzo yenu yalihusu nini? Andika mada ya mazungumzo mliyofanya.
3. Walioshiriki katika mazungumzo hayo walikuwa na mitazamo ipi?
4. Je, mazungumzo hayo yalishirikisha kina nani?
5. Kuna tofauti gani kati ya mdahalo na mjadala?
6. Unaelewa nini na "uambishaji wa maneno"?

## SOMO LA 13: MDAHALO

**Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali hapo chini.**



***Zoezi la 1: 1.Wahusika wanaoonekana kwenye mchoro wanafanya nini?***

***2. Wahusika hawa wako wapi?***

### 13.1. Kusoma na ufahamu : Mdahalo

*Soma mdahalo ufuatao wenye mada* "Hali ya maisha ya vijana wa leo ni bora zaidi kuliko ile ya vijana wa karne zilizopita", *kisha jibu maswali yaliyotolewa hapo chini.*

**Mwenyekiti (anasimama):** Waheshimiwa mabibi na mabwana mliokusanyika hapa hivi leo, hamjambo? Mada ya mdahalo wetu wa leo ni kama mnavyoiona ubaoni." HALI YA MAISHA YA VIJANA WA LEO NI BORA ZAIDI KULIKO ILE YA VIJANA WA KARNE ZILIZOPITA."

Sasa ningependa kumkaribisha bwana (ataje jina lake) ambaye ni msemaji mkuu wa kwanza upande wa utetezi ili atoe hoja zake kuhusu mada yetu. (anakaa)

**Msemaji wa 1 (Utetezi):** Mheshimiwa bwana mwenyekiti na washiriki wote, ni wazi kabisa kwamba hali ya vijana wa leo ni bora zaidi kuliko ile ya vijana wa karne zilizopita katika nyanja tofauti.

Kwa mfano, katika uwanja wa elimu, vijana wa leo wana haki ya kwenda shuleni wakati wangali wadogo kuanzia shule za chekechea hadi vyuo vikuu na kupata elimu ya kiwango cha hali ya juu. Wanapohitimu masomo hayo, hupewa shahada na kuajiriwa kwa kufanya kazi tofauti kama vile ualimu, udaktari, ukatibu, uhasibu, udereva, utangazaji habari, uongozi wa aina mbalimbali, ulinzi na usalama, ufanyaji biashara wa ndani na nje ya nchi, ujenzi wa majengo ya aina mbalimbali, ukarabati wa barabara, utafiti katika nyanja tofauti n.k. Wanapoajiriwa kwa kazi hizo wao hufaidika sana kwa kupata mshahara unaowasaidia kuboresha maisha yao na yale ya jamii nzima, jambo ambalo ni muhimu sana ukilinganisha na jinsi vijana wa zamani walivyokuwa wakiishi.

Vilevile, vijana hawa wa leo hawasumbuki sana kwa kufanya safari ndefu wanapoenda shuleni kama ilivyofanyika karne zilizopita. Shule zimejengwa mahali pengi sana na hata wanapohitaji kuendelea na masomo yao katika vyuo vikuu, huweza kuchagua kujiunga na chuo chochote kwani vyuo navyo vimekuwa vingi mno katika pande zote za nchi. Aidha, wale wanaochagua kusomea mbali na makazi yao, mabasi makubwa yameletwa na kampuni tofauti ambazo huendesha biashara za kubeba abiria kutoka eneo moja hadi jingine. Barabara zimetengenezwa kiasi kwamba wanafunzi hawa hawapati shida yoyote ya kusafiri kwa ajili ya masomo yao. Kumbukeni kwamba nyakati zilizopita, tunasikia kwamba mababu zetu walikuwa wakitembea kwa miguu usiku kucha kila walipotaka kutoka mahali fulani na kwenda mahali kwingine. Hali hii iliwafanya wamalize muda huo wa safari bila kula wala kunywa mpaka walipofika kule walikotarajia kwenda. Hili lilikuwa tatizo kubwa kwao kwani mara nyingine walipobahatika kupata kitu cha kuweka tumboni kilikuwa hakina usalama wowote kiasi cha kuambukizwa magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa nyinyi nyote mnaoshiriki katika mdahalo huu; haya ni baadhi ya mambo mengi yanayoweza kututhibitishia kwamba vijana wa leo huishi vizuri kuliko wale wa zamani. Kwa sasa namalizia hapa, nina imani kwamba wasikilizaji washiriki hamtasita kuniunga mkono kwa haya yote na mengine yatakayozungumziwa na wenzangu watetezi wa mada yetu. Asanteni sana kwa kunitega sikio.

**Mwenyekiti:** Naam, wasikilizaji washiriki. Baada ya kusikiliza hoja za msemaji mkuu wa kwanza upande wa utetezi, sasa ningependa kumkaribisha msemaji mkuu wa kwanza upande wa upinzani.

**Msemaji wa 1 (Upinzani):** Asanteni sana bwana mwenyekiti na wasikilizaji washiriki. Mimi sikubaliani kabisa na hoja ya utetezi wa mada hii. Msemaji aliyetangulia amesema kwamba vijana wa leo wanaanza kusoma wangali wadogo kufika kwa viwango vikubwa na kupewa shahada za hali ya juu wakapewa kazi na kunufaika. Bali, ni lazima tukumbuke kwamba vijana wa karne zilizopita nao walikuwa na namna yao ya kujifunza na kujua mengi ya maisha ya nyakati zao. Chunguza kwa mfano shughuli zilizokuwa zikifanywa katika "Itorero" ambapo walisomea uzalendo, kupenda kazi, ushirikiano, ushujaa, utii na mambo mengine. Kwa kweli, hizi zilikuwa shule za wakati wao na ziliwafunza mengi ambayo yaliwasaidia vijana wengi kuwa watu wazima na kufaulu katika maisha yao. Wakati wa karne hizo zilizopita kulikuwepo pia na shule zilizokuwa zikifundisha mambo ya ufundi kulingana kama vile ujenzi wa nyumba, utengenezaji wa nguo, uchongaji, uchoraji, usukaji, kubadilishana bidhaa kama ufanyaji biashara, haya yote yaliwawezesha kuboresha maisha yao na yale ya jamii kwa ujumla. Kwa hivyo, jamii ilikuwa na utulivu wa wakati huo kiasi kwamba mfadhaiko wa mawazo tunaoushuhudia siku hizi miongoni mwa vijana haukuwepo kwani kila kitu kiliweza kupatikana kwa urahisi na vijana wa nyakati hizo. Wao walikuwa wamejifunza mengi kuhusu namna ya kuendesha maisha yao na kuvumilia kila lililotokea. Ushujaa ndio ulikuwa kauli mbiu ya jamii nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waheshimwa wasikilizaji, vijana wa karne zilizopita, walikuwa na nguvu na miili yao ilikuwa thabiti kutokana na mazoezi mengi ya kutembea kwa miguu kwa muda mrefu. Nyakati zile, wao hawakuwa na magari ya kuwapeleka huku na kule na hali hii ilichochea uwezo mkubwa wa miili yao kujilinda na magonjwa mbalimbali ambayo hutokana na ukosefu wa mazoezi. Siku hizi huwa tunasikia vijana wanaopata magonjwa ya kisukari na mengine kutokana na desturi ya uvivu waliojijengea ambapo kila wanakoenda wao huhitaji kupanda gari ili liwapeleke hata kama ni mwendo wa dakika chache.

Mbali na hayo, vijana wa zamani waliweza kufaidika kwa kuelewa mazingira yao na kwingine walikopaswa kwenda. Hapo

waliweza kujenga urafiki na watu mbalimbali na kutafuta kazi kila walikofika.

Vijana wa leo pamoja na masomo ya jiografia wanayopewa hukumbwa na matatizo ya kujua maeneo mbalimbali ya nchi ilhali wahenga walisema kwamba mtembeaji hula miguu yake na pia kwamba mgaagaa na upwa hali wali mkavu. Kwa hivyo, kutembea kwa miguu kuliweza kuwanufaisha wakawa na maisha mazuri ambayo vijana wa leo hunyimwa na hali za anasa zilizojengwa na maendeleo ya kijamii. Asante sana kwa kunisikiliza.

**Mwenyekiti:** Waheshimiwa wasikilizaji washiriki, tumeisha sikiliza hoja za wasemaji wakuu wa kwanza kutoka pande zote mbili. Sasa ningependa kuwakaribisha wasemaji wakuu wa pili ili nao watoe hoja zao. Zamu ni ya msemaji mkuu upande wa utetezi.

**Msemaji wa 2 (Utetezi):** Bwana mwenyekiti, bwana katibu na waheshimiwa wasikilizaji washiriki! Asanteni sana kwa kunipa fursa hii ili niendelee kutoa hoja zangu. Nyote mmeelewa kwamba maoni ya msemaji mpinzani aliyepita yamesisitiza kwamba maendeleo ndiyo shida ambayo huwafanya vijana wa leo waishi maisha yasiyo mazuri akilinganisha na nyakati zilizopita ambapo watu walikuwa wakitembea kwa miguu. Kumbukeni kwamba watu anaowasema, walifanya matembezi hayo bila viatu au mavazi yenye kuwatia joto wakati wa baridi. Aidha hawakuwa na kitu chochote cha kujikinga dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa kama vile mwavuli tunaoutumia wakati wa mvua. Je, tukubali kwamba hayo ndiyo maisha yaliyokuwa mazuri zaidi kuliko maisha ya leo? Nafikiri kwamba hakuna yeyote anayeweza kuliafiki jambo hilo. Vijana hao walikumbwa na matatizo mengi na walisumbuka kabisa kwa kuyatafuta maisha mazuri. Lakini kama watu hawana zahanati wala hospitali, maisha huwa namna gani? Magonjwa tunayoyaona siku hizi si kitu kilichoanza leo ama juzi; ni hali iliyokuwepo tangu zamani za kale.

Je, kama mtu aliweza kupata ugonjwa aliende kutibiwa wapi zaidi ya kuwaendea waganga wale wa kienyeji ambao walifanya shughuli yao kwa kubahatisha au kubabaisha? Zaidi ya hayo, malezi ya mtoto huanza akiwa tumboni mwa mama yake hadi anapokuwa mtu mwenye nguvu.

Wakati huo yeye hupewa chanjo zote za kumlinda dhidi ya magonjwa mbalimbali kama surua, kifuakikuu, pepopunda, polio, n.k. Je, umejaribu kulinganisha na nyakati za zamani alizojaribu kusifu msemaji alienitangulia na nyakati hizi ambapo kuna maendeleo katika sekta zote za maisha? Bila shaka, kila mtu ataelewa kwamba vijana wa leo huishi maisha mazuri kuliko vijana wale wa zamani.

Kuhusu suala la michezo lililogusiwa na msemaji huyo, ningependa kusema kuwa siku hizi michezo ni kitu kilichotia fora sana miongoni mwa vijana. Yeye alisema kwamba michezo iliyokuwepo ilikuwa ya kutembea kwa miguu, lakini chunguza michezo iliyopo na ambayo inapendwa na vijana wengi. Michezo kama kandanda, mpira wa kikapu, mpira wa wavu, tenisi, michezo ya riadha kama vile kurusha mkuki, mbio za miguu, mbio za baiskeli, mbio za magari, mbio za pikipiki, kuruka n.k huwafurahisha watu wengi. Michezo kama hiyo na burudani nyingine ni mojawapo ya mambo muhimu ambayo huunganisha watu, kujenga urafiki na mshikamano kati ya watu. Zaidi ya hayo, michezo hiyo na burudani za nyimbo, ngoma, muziki na filamu huwastarehesha sana vijana na akili zao zikaweza kufanya kazi vizuri kwa kupanga miradi mbalimbali ya kujiendeleza na kuendeleza jamii nzima

Isitoshe, vijana wa leo wanaonekana vizuri kutokana na mavazi yao ya kisasa ambayo huwafurahisha wengi ukilinganisha na mavazi ya magome ya miti yaliyovaliwa nyakati za kale. Hivyo basi, unapomwona kijana amevaa nguo maridadi humfanya apendeze kuliko ilivyokuwa karne zilizopita. Mara nyingi mavazi haya ni kama suruali kwa wavulana na wasichana, kanzu, blauzi, sketi, chupi, magagulo, sweta, suti, vikoi, kofia, viatu vya aina mbalimbali na mapambo ya aina tofauti kama vile hereni, vidani, mikufu, pete, n.k. Mapambo haya huchangia sana kumfanya kijana aonekane maridadi kuliko kijana wa zamani. Na jambo tena tunalolifurahia siku hizi ni kwamba mengi ya mavazi haya yanayopendwa na watu wengi, hutengenezwa nchini Rwanda. Hivyo kila mtu anayeyataka huweza kuyapata kwa urahisi na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa mwenyekiti, wasikilizaji washiriki wapendwa, siwezi kumaliza fursa yangu bila kugusia jambo muhimu sana la matumizi ya teknolojia ya kisasa na mitandao ya kijamii. Vijana wa leo wamebahatika sana na kunufaika zaidi kwa kutumia teknolojia hii.

Hivi leo, ni jambo rahisi kuwasiliana na mtu aliye Amerika, Ulaya, Asia, Australia, na maeneo mengine ya bara la Afrika bila gharama kubwa. Kupitia njia za mitandao ya intaneti, simu za mikononi, mitandao ya fesibuku, tarakilishi, na teknolojia nyingine, vijana wa leo huweza kushirikiana katika maeneo yao tofauti na mambo haya huwasaidia kupashana habari, kuelimishana na kuimarisha urafiki na mshikamano kati yao kuliko ilivyokuwa nyakati za zamani. Njia za teknolojia huweza kutumiwa mara nyingi kwa kuboresha maisha ya vijana wa leo. Mheshimiwa mwenyekiti, wasikilizaji washiriki, kutokana na haya yote na mengine yaliyozungumziwa na mwenzangu yanadhihirisha kwamba vijana wa leo huishi maisha mazuri kuliko vijana wa karne zilizopita. Asante sana kwa kunitega sikio.

**Mwenyekiti:** Naam, waheshimiwa wasikilizaji washiriki, mawazo yote mmeyasikia, sasa ninamkaribisha msemaji mkuu wa pili kutoka upande wa upinzani.

**Msemaji wa 2 (Upinzani):** Bwana mwenyekiti, waheshimiwa wasikilizaji washiriki, asanteni sana kwa kunipa furasa hii ili nami nitoe maoni yangu. Sikubaliani na hoja za msemaji wa pili wa upande wa utetezi. Kumbukeni kwamba zamani kulikuwepo waganga waliozoea kutumia dawa za mitishamba na kusaidia wagonjwa wakapona kwa haraka. Dawa hizi zingali zinatumika hata siku hizi na mara nyingine madaktari wa kisasa huweza kushindwa kutibu baadhi ya maradhi na hivyo hutibiwa na waganga wa kienyeji. Jambo hili ndilo liliwafanya waganga hawa wajiunge katika mashirika yao ili waweze kufanya kazi yao vizuri. Mbali na hayo, nyakati zilizopita kulikuwepo pia wakunga ambao walisaidia kina mama wakati wa kujifungua. Wao walikuwa na ujuzi na uzoefu wa kutosha ambao uliwawezsha kufanikisha kazi yao. Magonjwa kama vidonda, upele, magonjwa ya ini, uyabisi wa choo, magonjwa ya utapiamlo, kuharisha, n.k. hayakuwa na nafasi katika jamii ya nyakati hizo kwani yaliweza kutibiwa haraka. Baada ya mtoto kuzaliwa, kulikuwepo na jinsi ya kumlea na kufuatilia afya yake ili kumlinda dhidi ya magonjwa yote yaliyodokezwa na msemaji aliyenitangulia. Hivyo mtoto aliweza kufikia umri wa kuwa kijana akionekana kuwa na nguvu za kumwezesha kufanya kila jambo alilotakiwa kulifanya. Hali hii ndiyo iliwafanya watu wa karne hizo waishi muda mrefu bila kupatwa na magonjwa kama yale yaliyopo siku hizi.

Kuhusiana na michezo na burudani, ningependa kuwajulisha kwamba jambo hili si kitu kilichobuniwa siku hizi. Vijana wa karne zilizopita walikuwa na michezo mbalimbali ambayo iliwafurahisha wengi na kuwastarehesha. Chunguza kwa mfano mchezo wa kupiga miereka, michezo ya "Intore", majigambo, kutupa mikuki, kuruka, kuvutana, michezo ya bembea za kienyeji, kwa vijana na mingine. Michezo hii ilikuwa bora kwa maisha yao na ilikuwa imeendelezwa kwa kiwango cha juu. Burudani nazo zilipewa kipaumbele ambapo kupiga mbiu, kucharaza nanga, nyimbo za aina mbalimbali zilizoimbwa kulingana na shughuli zao, kucheza ngoma, majigambo, ucheshi, kutamba hadithi, kutega vitendawili, kufumba na kufumbua na mengine mengi yaliweza kuwafurahisha na kuwastarehesha sana vijana wa karne zilizopita. Ukiangalia vijana wa leo, mambo haya yote hawayajui. Badala yake, wao hupoteza muda mrefu kwa kutumia teknolojia zile zilizozungumziwa na msemaji aliyenitangulia. Teknolojia hizi ndizo chanzo cha mienendo mibaya na tabia mbaya miongoni mwa vijana wa leo na mara nyingi vijana hawa huzitumia kwa kuangamiza maisha yao badala ya kuyaboresha au kuwaendeleza.

Kuhusu mavazi, vijana wa karne zilizopita, walikuwa wakivaa mavazi kulingana na wakati wao. Mavazi haya yalikuwa yakitengenezwa katika ngozi za wanyama, nyuzi na magome ya miti na yaliwafaa wakati huo. Lakini, chunguza mavazi ya vijana wa leo, jamani, ni ya kushangaza sana! Kwa kawaida mavazi ni pambo kwa binadamu na huonyesha utamaduni wa mtu na humfanya mtu aonekane maridadi siyo kuvaa uchi au kuonyesha utupu wao. Mavazi mengi ni ya kupotosha kabisa na ya kudhalilisha wanaoyavaa. Siku hizi huweza kumkuta msichana akitembea kitovu nje, mgongo wazi kutokana na mavazi aliyoyavaa. Mavazi mengine kama sketi fupi zinazowabana nyonga na makalio huonyesha ukosefu wa nidhamu na heshima anayostahili kijana. Nao vijana wa leo wa kiume hawana haya ya kuvaa suruali zilizochanika kwenye magoti na zinazoning'inia kwenye makalio. Vijana wengine wa kiume hujichora kwenye miili yao, hubadilisha nywele zao na kuzifanya au kuzisuka kama wasichana. Kwa kweli haya yote na mengine mengi yanayofanywa na vijana wa leo ni hatari kwa afya yao. Wengi huweza kuambukizwa magonjwa tofauti na kila wanapobadilisha mienendo yao. Hii

inatokana na kujitoma katika tabia mbaya ambazo mwishowe huweza kuwaangamiza.

Kwa hivyo, ni wazi kwamba wasikilizaji washiriki hamtakosa kuniunga mkono kwamba maisha ya vijana wa leo si mazuri ukilinganisha na maisha ya vijana wa zamani kwani ving'aavyo, vyote si dhahabu. Asanteni sana kwa kunitega sikio.

**Mwenyekiti:** Mengi mmeyasikia kutoka kwa wasemaji wakuu kutoka pande zote mbili, nina matumaini kuwa mmeyazingatia yote. Sasa ninapenda kuchukua fursa ya kuwakaribisha wasikilizaji washiriki ili nao watoe hoja zao kwa mada hii. (Mwenyekiti achague msikilizaji mshiriki aliyenyosha mkono).

**Msikilizaji mshiriki 1:** Asante sana bwana mwenyekiti, hoja zote zilizotolewa kutoka upande wa utetezi na upande wa upinzani ni nzuri; lakini kwa upande wangu ningependa kuwaunga mkono watetezi wanaposema kuwa maisha ya vijana wa leo ni bora zaidi kutokana na maendeleo na teknolojia ya kisasa. Hata hivyo, ningependa kutoa wito kwao ili watambue kwamba teknolojia hii huhitaji uangalifu mno. Ni lazima waitumie kwa shughuli za kujiendeleza kielimu, kisayansi na kijamii badala ya kujiharibu kwa kujiingiza katika vitendo vibaya na mienendo mibaya. Wengi wa vijana hawa wanahitaji kubadilisha tabia zao ili wajenge maisha yao na kuwa watu wazima wenye nafasi na majukumu katika jamii nzima. Asante sana mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Bibi (ataje jina lake) Ninaona unanyosha mkono.

**Msikilizaji mshiriki 2**: Asante bwana mwenyekiti. Mimi ninaunga mkono upande wa upinzani kwa sababu vijana wa karne zilizopita ndio walikuwa na maisha mazuri. Wao walikuwa na nidhamu na heshima kuliko vijana wa leo. Tabia na mienendo mizuri iliyowatambulisha ndiyo iliwawezesha kuwa na ndoa zilizoimarika kiasi cha kuaminiana, tofauti na hali ilivyo ya leo ambapo familia nyingi zinafarakana kwa sababu ya kusalitiana. Siku hizi uchumba hufanyiwa kwenye simu na mitandao ya kijamii na jambo hili husababisha kutofuata mila na desturi za jamii ambazo zilimshirikisha mshenga katika masuala ya ndoa. Matokeo yake kujenga familia zisizodumu muda mrefu. Familia kama hizo ndizo huishia mahakamani na kupeana talaka baada ya muda mfupi wa kufunga ndoa. Hivyo basi, maisha ya vijana wa leo siyo mazuri kuliko yale ya

vijana wa zamani. Asanteni sana.

**Mwenyekiti:** Waheshimiwa, baada ya haya yote, ninaona kuwa ni wakati wa kusikiliza hoja zote kutoka mdahalo huu. Ninapenda kumkaribisha katibu wa mdahalo ili atusomee muhtasari wa hoja zilizotolewa na pande zote mbili na hatimaye kupiga kura na kuona ni upande gani umeshinda. Zamu ni yako katibu.

**Katibu:** Asante bwana mwenyekiti. Wasemaji wa upande wa utetezi walitoa mawazo yafuatayo:

- Vijana wa leo wana haki ya kwenda shuleni wangali wadogo kutoka shule za chekechea hadi vyuo vikuu na kupata elimu inayowawezesha kufanya kazi mbalimbali za kujiendeleza.
- Shule ni za karibu na makazi yao na hawafanyi safari ndefu kufika shuleni.
- Shuleni wanajifunza adabu na nidhamu nzuri zinazowafanya kuwa watu wazuri katika jamii.
- Afya yao ni nzuri kwa kuwa wanazaliwa zahanatini na hospitalini
- Wanajistarehesha kwa kushiriki katika michezo na kujiburudisha kwa kucheza ngoma na kutazama filamu mbalimbali
- Wanatumia njia za teknolojia kwa kuwasiliana na kufanya kazi za kujiendeleza wao wenyewe na jamii kwa ujumla.

Wasemaji wa upande wa upinzani wametoa hoja zifuatazo:

- Vijana wa karne zilizopita nao walikuwa wanafanya" Itorero" walipojifunzia uzalendo, utii na maadili mengine.
- Kuenda kwa miguu ni vizuri kwa kuwa ni kufanya spoti, kuangalia vitu vinavyowavutia na kufahamiana na watu wengine.
- Vijana wa leo hawana nidhamu na adabu nzuri
- Katika karne zilizopita kulikuwepo waganga wanaowasaidia wagonjwa
- Walikuwa na michezo kama vile miereka, michezo ya " Intore", n.k.

- Vijana wa leo wanavaa nguo fupi na zinazobana sana na wengine wanavaa nusu uchi
- Kutokana na teknolojia, wanaiga tabia mbaya, wanapiga ubwana hata kuwa wavivu.

**Mwenyekiti:** Naam, baada ya kusikiliza hoja zote, ni wakati wa kupiga kura ili tujue ni upande gani umepata ushindi. Sasa wanaounga mkono upande wa utetezi wanyoshe mikono. Katibu! Andika idadi ya watu hao. Wanaounga mkono upande wa upinzani nao mikono juu. Na wasiounga mkono upande wowote? Katibu wa mdahalo, tusomee matokeo ya kura.

**Katibu:** Watu wanne hawakuelekea upande wowote.

Upande wa utetezi umepata kura ishirini na moja (aandike 21 ubaoni). Upande wa upinzani umepata kura kumi na tano (anaandika 15 ubaoni). Wasikilizaji washiriki wanawapigia makofi.

**Mwenyekiti:** Mabibi na mabwana, baada ya kupiga kura na kuona matokeo ya kura, ushindi katika mdahalo wetu umekwenda kwa upande wa utetezi.

Hadhira inawapigia washindi makofi na mwalimu wa somo atoe maoni yake juu ya mdahalo huo.

***Maswali ya ufahamu***

1. Andika kichwa cha mada ya mdahalo wa hapo juu.
2. Ni pande gani zinazoonekana katika mdahalo huu?
3. Eleza hoja za mtetezi wa I katika mdahalo huu.
4. Ni aina gani ya michezo inayozungumziwa katika mdahalo huu?
5. Eleza madhara yanayotokana na matumizi mabaya ya teknolojia ya kisasa.
6. Ni magonjwa gani yanayohitaji chanjo au kinga ili kulinda afya ya mtoto?
7. Eleza jinsi vijana wa kale walivyoweza kuburudika.
8. Michezo huwa na faida gani kwa mwili wa mtu?
9. Kwa nini baadhi ya ndoa huvunjika au zisidumu kwa muda mrefu?
10. Taja namna za kuvaa zilizozungumziwa katika mdahalo huu.

## 13.2. Msamiati

***Zoezi la 2: Unganisha maneno ya safu A na maana zake katika safu B.***

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| 1. Mwenyekiti | a. enye kupendeza macho |
| 2.Unyago | b. Shule za watoto wadogo wasiozidi miaka mitano |
| 3. Mwenendo | c. Shughuli inayofanywa kwa ajili ya kufurahisha na kuchangamsha watu. |
| 4. Shule za chekechea | d. Matendo ya mtu yanayojirudiarudia au tabia. |
| 5. Shahada | e. Karatasi maalumu anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo ili kuthibitisha kwamba amemaliza au amefaulu mitihani yake. |
| 6. Maridadi | f. Adabu |
| 7. Nidhamu | g. Maonyesho ya sinema. |
| 8. Filamu | h. Ngoma ya kuwafundisha wari mila za kabila lao. |
| 9. Jando | i. Mtu aliyechaguliwa na watu kuongoza kama vile mkutano au mdahalo. |
| 10. Burudani | j. Kumbi la watoto wanaume wanapotahiriwa na kufundishwa mambo ya utu uzima. |

***Zoezi la 3: Tunga sentensi zenye maana kamili kwa kutumia maneno hapo chini:***

1. Chuo kikuu
2. Michezo ya riadha
3. Mbio za miguu
4. Kuvaa maridadi
5. Polio
6. Udaktari
7. Mfadhaiko
8. Kufaulu
9. Kura
10. Elimu

***Zoezi la 4: Jaza sentensi hapo chini kwa kutumia maneno uliyopewa: kitovu wazi, mvivu, utafiti, wasikilizaji, abiria, utetezi, surua, karne, mwanamwali, upinzani.***

1. Si vizuri kuwa mtu …………………………. maishani .

2. Vijana wa ………………………. hii wanasoma kwa wingi.

3. ………………………… wanatega sikio wakati wa mdahalo.

4. Ni lazima watoto wote kuchanjwa chanjo ya……………………….. wangali wadogo.

5. Upande wa …………………………. hupinga hoja zinazotolewa na upande wa ………………………….

6. ………………………………… hafanyi matendo yanayomdhahilisha.

7. ……………………………….. si nguo zinazofaa wanawali.

8. ……………………………….. ni uchunguzi wa kitaaluma wenye lengo la kutafuta habari.

***Zoezi la 5: Panga maneno yafuatayo kwa kuunda sentensi sahihi***

**Mfano:** Filamu kuchunguza na ni video vizuri mnazozitazama.

- Ni vizuri kuchunguza filamu na video mnazozitazama.

1. Wanapaswa wao kuwasaidia wazazi watoto

2. Vijana makosa na vizuri ni kuwaonyesha yao upendo kwa kuwaadhibu

3. Wako mwana mwenzako ni wa

4. Kushindwa siku usikubali moja hata

5. Wananchi apande kulinda kwa kila miti mazingira.

6. Bei ghali si vitu mapenzi kuwanunulia vya

7. Dhahabu adabu ni.

## 13.3 Sarufi: Uambishaji wa maneno

***Zoezi la 6: Yaweke majina yafuatayo katika wingi, kisha ueleze mabadiliko yaliyojitokeza kwa kuhusisha na uliyojifunza kuhusu uambishaji katika somo la 12.***

**Mfano:**

Mtoto – watoto

Mschana – wasichana

1. Mwenyekiti
2. Msemaji
3. Kiatu
4. Mchezo
5. Mgonjwa

- **Chunguza maelezo yafuatayo:**
  - Uambishaji katika hali hii umedhihirishwa kupitia viambishi vya umoja na wingi.
  - Kumbuka kuwa uambishaji ni utaratibu wa kuambatisha viambishi kwenye mizizi.
  - Uundaji wa maneno ya Kiswahili hufanywa kwa kuonyesha hali ya wastani, udogo, ukubwa na dhana ya dhahania.
- **Wastani** huonyesha maneno ya kawaida kwa umoja au wingi.

**Mfano:** Mtu – watu

Mlango – milango

Kitabu - vitabu

Kwa kuonyesha **hali ya udogo**, nomino inayozungumziwa huwekwa katika ngeli ya **KI-VI.**

**Mfano:** Mtoto – kitoto - vitoto

Mwana – kijana – vijana

Msichana – kisichana - visichana

Kwa kuonyesha ukubwa, nomino inayozungumziwa huwekwa katika ngeli ya **LI – YA**. Kiambishi **ji** huwekwa mwanzoni ili kuonyesha ukubwa

**Mfano:** Mtoto –jitoto - matoto

Mji – jiji - majiji

Mtu –jitu - majitu

Suruali – jisuruali – majisuruali

Ngoma – jigoma - majigoma

Dhana ya **dhahania ni** dhana ambayo nomino ni za kufikirika tu au hazishikiki. Dhana hii huonyeshwa na kiambishi **u** kinachoambikwa kwa mizizi ya maneno mengine.

**Mfano:** mtoto – utoto

Mwana - ujana

Mzee –uzee

***Zoezi la 7: Andika majina ya dhahania yanayotokana na maneno yaliyoandikwa kwa rangi iliyokoza***

1. **Daktari** ni mtu imara maishani mwetu.
2. **Mzalendo** hupenda nchi yake.
3. **Pendo** ni jambo jema kati ya watu.
4. **Mwalimu** anafundisha wanafunzi.

***Zoezi la 8: Andika sentensi zifuatazo katika hali ya udogo***

1. Gari lake ni zuri.
2. Mji wetu una usafi.
3. Shamba lake ni kubwa.
4. Sabuni inatumiwa kwa kufua nguo.
5. Mvulana huyu anapenda kucheza mpira.

***Zoezi la 9: Andika sentensi ulizopewa hapo chini katika hali ya ukubwa***

1. Kichwa chake kinamuuma.
2. Kiatu changu kimepotea.
3. Ni vizuri kutega sikio msemaji.
4. Duka lake linajaa sahani.
5. Kitanda hiki kilitengenezwa jana.
6. Ufagio utanunuliwa kesho.

## 13.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Mdahalo

***Zoezi la 10: Soma maelezo hapo chini kisha ujibu maswali husika***

**MAELEZO MUHIMU**

Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja maalumu. Kuna mada inayozungumziwa, wazungumzaji wakuu wanaotetea mada (upande wa utetezi) na wazungumzaji wakuu wengine wanaopinga mada (upande wa upinzani). Aghalabu huwa wazungumzaji wakuu wawili kwa kila upande.

Mwenyekiti wa mdahalo ana wajibu wa kufungua na kuendesha mdahalo, kuwapa wasemaji nafasi ya kuzungumza, kupigisha kura na kufunga mdahalo.

Katibu wa mdahalo ndiye huandika hoja zinazotolewa na wazungumzaji mbalimbali, kufanya na kusoma muhtasari wa hoja zilizotolewa na pande mbili mwishoni mwa mdahalo na kutangaza matokeo ya kura zilizopigwa.

Mdahalo ukifanyiwa darasani, mwalimu atatoa maoni yake juu ya mdahalo.

***Maswali:***

1. Eleza wajibu wa katibu katika mdahalo.
2. Jadili wahusika wa mdahalo.

***Zoezi la 11: Jibu maswali yafuatayo kuhusu mdahalo***

1. Andika wahusika wa mdahalo.
2. Eleza maana ya mdahalo.
3. Ni pande gani zinazoonekana katika mdahalo?

## 13.5. Kusikiliza na Kuzungumza : Mazungumzo na Majadiliano

***Zoezi la 12: Kwa kushirikiana na wenzako, jadilini mada zifuatazo :***

1. " Umuhimu wa mdahalo kwa wanafunzi".
2. " Ueneaji wa teknolojia katika maendeleo ya nchi"

## 13.6. Kuandika: Utungaji wa Mdahalo

Tunga mdahalo kuhusu mada ifuatayo, kisha uiwasilishe mbele ya darasa kwa kushirikiana na wenzako

"NDOA YA KALE ILIKUWA BORA KULIKO NDOA YA LEO".

# SOMO LA 14: MJADALA

***Zoezi la 1: Jibu maswali yafuatayo.***

1. Ulishawahi kuhudhuria mjadala wowote?
2. Ulikuwa unahusu mada ipi ?
3. Ni mafunzo gani uliyoyapata kutokana na mjadala huo?

## 14.1. Kusoma na Ufahamu: Mjadala

*Soma mjadala ufuatao kuhusu* "Mambo muhimu yanayohitajika ili kuimarisha desturi ya kujitegemea kwa jamii ya Rwanda", *kisha jibu maswali yaliyotolewa hapo chini*

**Kiongozi:** Waheshimiwa mabibi na mabwana mliokusanyika hapa, ninawakaribisha kwanza katika mjadala huu. Mada ya mjadala wa leo kama mnavyoisoma mbele yenu **"Mambo Muhimu Yanayohitajika ili Kuimarisha Desturi ya Kujitegemea kwa Jamii ya Rwanda."** Karibuni sana nyote. Bila kupoteza muda, ningependa kumkaribisha mshiriki aliye tayari ili atoe mchango wake.

**Mshiriki wa 1:** Ninamshukuru sana mwenyekiti na washiriki wenzangu. Ni kweli kabisa kwamba kuna mambo muhimu yanayohitajika ili kuimarisha desturi ya kujitegemea kwa jamii ya Wanyarwanda. Kama inavyoonekana siku hizi, sekta ya kilimo na ufugaji ni muhimu sana katika maisha ya jamii. Watu wengi nchini Rwanda huishi kwa pato la kilimo na ufugaji. Hii ndiyo sababu tunapaswa kutilia mkazo sekta hii ili mapato yaongezeke. Ni lazima kutumia mbinu za kisasa na kiteknolojia. Kilimo na ufugaji vikifanyika ifaavyo, watu watakuwa na mavuno ya kujitosheleza nchini na kuuza katika masoko ya nje ya nchi. Vile vile watapokea pesa za kigeni zitakazosaidia katika maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Haya yote yatatimizika tukisaidiwa na wataalam wa sekta hii watakaowafundisha wananchi mbinu mpya za kutekeleza miradi ya ufugaji na ukulima kwa kushirikiana na ngazi za serikali kuanzia ngazi za vijiji.

Namna ya kutimiza wajibu huu, inalazimu kuendelea kulima na kupanda mbegu zile zinazochaguliwa kulingana na utafiti uliofanyika kuhusu ardhi ya eneo fulani. Ufugaji uendelee kufanyika ili wakulima waendelee kupata mbolea ya kurutubisha mashamba yao, wavune vyakula vya kutosha na wapate baadhi ya malighafi za kutumia katika utengenezaji wa vitu mbalimbali.

Sasa hivi Serikali ya Rwanda ilianzisha mpango wa "GIRA INKA MUNYARWANDA" kuimarisha sekta ya kilimo na ufugaji. Mpango huu unalenga kuwasaidia wananchi wasiojiweza kujijengea uwezo kwa kufuga ng'ombe ili waweze kujiepusha na umaskini, kuanzia kwa wale wanaoishi maisha duni kwa kiwango cha chini na kuendelea kwa wengine. Waliofikiwa na mpango huu wanakunywa maziwa, wanapata mbolea na kuongeza mazao ya kilimo, wanajilipia bima ya afya na mengine mengi yahusuyo maisha ya msingi. Kwa ufupi, walipiga hatua ya kupendeza sana na kujiendeleza kiafya. Asanteni kwa kunisikiliza.

**Kiongozi:** Asante sana kwa hoja yako. Kama mlivyosikia, msemaji huyu ameelezea kuwa kilimo na ufugaji ndio msingi thabiti wa maendeleo ya nchi yetu. Kilimo na ufugaji vifanyike ifaavyo ili maendeleo ya nchi yawe ya kudumu. Wasiojiweza waendelee kujenga na kukuza uwezo wao na tabia ya kujiendeleza kutoka daraja moja hadi jingine. Hebu tumsikilize msemaji mwingine. Karibu sana bwana!

**Mshiriki wa 2:** Asante sana mwenyekiti kunipa fursa hii ili nitoe hoja zangu. Kwa maoni yangu, watu hawawezi kuwa na desturi ya kujitegemea bila elimu maalumu katika nyanja mbalimbali. Serikali ya Rwanda ilianzisha elimu kwa wote isiyo na ubaguzi wowote. Kwa hiyo kila mtoto ana

haki ya kusoma na kupata elimu ya msingi ya miaka kumi na miwili na hata kuendelea katika vyuo vikuu. Jambo hili ni la kumtayarisha kila mwananchi kuwa na uwezo wa kujitegemea katika maisha, kwani kuendelea kwa nchi hutokana na ujuzi walio nao wananchi. Kwa hiyo, masomo ya udaktari yanahitajika kwa lengo la kutibu magonjwa yanayowakumba wananchi na mifugo. Ualimu unahitajika kwani kila msomi hufundishwa na mwalimu. Masomo ya kilimo yanatakiwa kukuza utafiti na kuongeza mazao katika sekta ya ukulima. Shule za ufundi na ustadi zinaendelea kuenezwa nchini kote kwa ajili ya kufanya kazi zenye ufanisi, kujitafutia ajira na kutoa suluhisho la uhaba wa kazi.

Kusoma hurahisisha utekelezaji wa miradi na mikakati ya serikali. Kutokana na elimu, nchi inashirikiana na nchi nyingine zilizoendelea kupitia njia za misaada ya masomo ya kitaalamu katika taaluma mbalimbali.

Wasomi kwa kiwango hiki cha hali ya juu, ndio wanaosaidia nchi kufanya utafiti na kutoa masuluhisho kuhusu matatizo yanayoweza kuwa kizuizi chochote cha maendeleo katika sekta zote za maisha ya nchi. Hata hivyo, elimu huwezesha baadhi ya Wanyarwanda kufika kwenye daraja la kusimamia mojawapo ya mashirika ya kimataifa katika nyanja mbalimbali. Elimu ni msingi wa maisha mazuri yenye maendeleo ya kudumu. Asanteni kwa kunisikiliza.

**Kiongozi:** Ninamshukuru sana mshiriki aliyepita kwa hoja zake. Anasema kwamba elimu ni jambo muhimu sana katika maendeleo ya nchi yenye nia ya kujitegemea. Analinganisha elimu na maisha mema pamoja na msingi wa maendeleo endelevu yanayoleta ustawi kwa kila mwananchi. Bila elimu, nchi yetu haiwezi kutimiza lengo hilo. Tumsikilize sasa mama yule atoe mchango wake.

**Mshiriki wa 3**: Nami namshukuru sana kiongozi kwa kunipa fursa ya kutoa hoja zangu. Siku hizi, teknolojia ni muhimu sana ulimwenguni. Na hapa nchini kwetu imefika kwenye kiwango cha kuthaminiwa tukilinganisha na siku zilizopita. Inatumiwa katika nyanja zote mathalani katika elimu: wanafunzi wanasomea kwenye tarakilishi na mitandao mbalimbali, walimu wanaandika vitabu vitumiwavyo kwa kuandaa na kufundisha masomo mbalimbali. Utafiti wa aina tofauti pia hufanywa kupitia tarakilishi na mitandao.

Teknolojia hutumiwa pia katika taaluma ya afya kama vile upasuaji, kuchanja na kutibu maradhi na utengenezaji na uhifadhi wa chanjo na dawa zitumiwazo kwa kutibu magonjwa mbalimbali. Teknolojia hutumiwa tena katika kukusanya, kutangaza na kuhifadhi habari kwa njia ya sauti au picha mithili ya utangazaji wa habari redioni au kwenye

runinga yaani televisheni. Zaidi ya haya, teknolojia hutumiwa kwa kupashana habari zenye miradi ya kuzalisha mali kupitia njia ya simu ya mkononi. Katika nyanja za biashara, usafirishaji wa abiria na bidhaa katika njia ya hewani, barani na majini ulirahisishwa na teknolojia.

Nchini kwetu, baadhi ya wafanyabishara wanaweza kuagiza na kulipa bidhaa ugenini bila ya kwenda pale kwa kutumia njia ya teknolojia. Ndege bila marubani leo nchini kote kwa kupeleka damu kwenye hospitali na zahanati kwa kutumia muda mfupi.

Katika uwanja wa uchumi, benki zote na mashirika ya kifedha hutumia teknolojia kwa kuhudumia wateja wao na kutimiza wajibu wao. Huduma nyingi za serikali hutolewa kupitia mitandao ya intaneti kwa lengo la kurahisisha kazi na kutumia muda mfupi. Mfano hapa ni mtandao wa irembo.

Hayo yote yanafanyika kwa kumtafutia maisha mema mwananchi na kumwezesha kujijengea tabia ya desturi ya kujitegemea na kujiendeleza binafsi na jamii kwa ujumla. Asanteni sana kunisikiliza.

**Kiongozi:** Ninamshukuru mama huyu mshiriki kwa hoja zake. Anaeleza kwamba teknolojia ni jambo muhimu sana ulimwenguni kote na kila shughuli nyingi huhitaji teknolojia ili itimizwe ifaavyo. Haya! Tusikilize bwana yule.

**Mshiriki wa 4:** Kwanza ninamshukuru sana kiongozi pamoja na washiriki wenzangu walionitangulia kwa maoni yao. Kuna sekta muhimu sana inayohitajika kwa kuimarisha desturi za kujitegemea katika jamii. Sekta hiyo isipopatikana hatuwezi kuwa na maendeleo endelevu. Hiyo ni ile ya viwanda ambavyo ni muhimu sana kwa maisha ya wanajamii kwa kuwapa kazi, bidhaa za kutumia katika maisha ya kila siku. Kuna viwanda vya namna na ukubwa tofauti kulingana na kazi vinavyokusudiwa kufanya. Kuhusu viwanda vidogo, kuna viwanda vya utengenezaji wa viatu, mikoba na mikanda kwa kutumia ngozi za wanyama wa mifugo kama malighafi inayopatikana kwetu. Kuna viwanda vidogo vya ususi wa sweta kwa kutumia nyuzi za aina tofauti.

Kuna aina nyingine ya viwanda vidogo vidogo vinavyotengeneza vinywaji na vyakula kutoka mavuno ya kilimo na ufugaji na hata kuhifadhiwa kwa muda mrefu. Utengenezaji huo hufanyika kwa usafi kuliko ule unaofanyika kwa namna ya kienyeji. Kuna viwanda vidogo vinavyotengeneza mafuta ya kujipaka mwilini, sabuni za kufulia na kuogea zinazosaidia watu kujisafisha. Viwanda vidogo hutengeneza pia kahawa inayouzwa nje ya nchi na kutupa pesa za kigeni na kunufaisha wakulima na nchi kwa ujumla.

Kuhusu viwanda vikubwa, bidhaa hutengenezwa kwa kiwango kikubwa kwa lengo la kutosheleza masoko ya ndani na ya nje. Baadhi ya bidhaa zinazotengenezewa humo ni vyuma vya kujengea nyumba tofauti, viwanda vya kutengenezewa vinywaji kwa kiwango kikubwa, sabuni na mafuta ya aina mbalimbali, viatu, mikoba na mikanda, kiwanda cha sukari, kiwanda cha saruji, kiwanda cha unga n.k. Viwanda vinavyotengeneza nguo ni muhimu sana kwa kutoa mchango wake kwa kujitengenezea nguo mpya na kupiga marufuku nguo zilizotumiwa kutoka nje baada ya kuvaliwa na wengine. Mambo haya yote yanamwezesha mwananchi wa kila rika kujenga tabia ya kujitegemea na kujitafutia ajira ili aboreshe maisha yake na ya nchi kwa ujumla. Asanteni sana kwa kunisikiliza.

**Kiongozi:** Ninamshukuru sana bwana huyu mshiriki kwa hoja zake. Anaeleza kwamba viwanda vina mchango mkubwa katika kujitegemea kwa nchi. Vinatusaidia kupata nguo na vyakula safi bila kusahau bidhaa tofauti. Ebu tusikilize bwana yule atoe hoja zake.

**Mshiriki wa 5:** Shukrani sana kiongozi pamoja na nyinyi nyote mlioshiriki katika mjadala huu. Kwa maoni yangu, kujitegemea kwa jamii kwahitaji usawa wa kijinsia ndani ya familia zetu. Familia ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi na jamii yoyote. Kwa hiyo, ni lazima wanawake na wanaume wawe na uwezo pamoja na ujuzi wa kujiendeleza katika familia zao. Kujitegemea kwa jamii yetu kwahitaji kuanzia ndani ya familia. Mwanamke ashirikiane na mumewe kuwalea watoto wao vilivyo kwani ndio ambao watasaidia jamii ya kesho kuyafikia maendeleo thabiti.

Mwanamume akishirikiana na mkewe huweza kutenda kazi zenye ufanisi kwa kupata mali nyingi. Ni lazima wawe na mwelekeo mmoja na wajiepushe na utengano wowote ili wayafikie malengo yao. Ushirikiano wa mume na mke ndio chanzo cha kuendeleza familia yao kwani kila familia ikifanikiwa ni nchi nzima inayofanikiwa. Tuimarishe usawa wa kijinsia ili tuweze kuyafikia maendeleo ya kudumu yatakayotuwezesha kujitegemea sisi wenyewe. Asanteni nyote kunisikiliza, hayo ndiyo maoni yangu.

***Kiongozi***: Asante sana mshiriki kwa hoja zako nzuri. Ni kweli familia ndiyo msingi wa maendeleo kwa nchi yote. Ni lazima familia ihakikishe usawa wa kijinsia na iweze kujitegemea ili jamii nzima ifikie maendeleo ya kudumu. Ebu tuufikie mwisho wa mjadala wetu.

Sasa inaonekana kwamba mjadala wetu unafikia mwisho. Lakini kabla ya kuufunga, ningependa kuwapongeza ninyi nyote kwa hoja zenu mlizozitoa katika mazungumzo haya. Asanteni sana! Niwakumbushe

kichwa cha mjadala wa leo kilikuwa “Mambo muhimu yanayohitajika ili kuimarisha desturi ya kujitegemea kwa jamii ya Rwanda. Miongoni mwa hoja mlizozitoa ni kuhusu sekta ya kilimo na ufugaji, elimu, viwanda, teknolojia na usawa wa kijinsia. Haya ni mambo muhimu sana yanayoungana mkono kwa kuimarisha desturi ya kujitegemea kwa jamii ya Rwanda, kupiga vita uhaba wa kazi, na kuboresha maisha ya wanajamii sote. Ninawaalikia kujiunga nasi kwa wingi wakati mwingine kwa mada itakayotolewa. Asanteni sana. Kwaherini! Ninawatakia heri na fanaka.

***Maswali ya Ufahamu***

1. Ni nani ambaye anaongoza mjadala na kuwaruhusu wanaotoa hoja zao?
2. Tabia ya desturi ya kujitegemea inaanzia wapi?
3. Eleza tofauti baina ya viwanda vidogo na viwanda vikubwa.
4. Eleza malighafi zilizotajwa katika mjadala uliousoma.
5. Taifa lilisaidia nini kwa kurahisisha mikakati ya desturi ya kujitegemea katika jamii?
6. Eleza methali hii”Mtegemea cha nduguye hufa maskini.”
7. Viwanda vya kutenezea nguo nchini vina manufaa gani kwa wananchi na nchi kwa ujumla?
8. Toa mfano wa malighafi inayoweza kutumiwa kwa kutengeneza mkoba na viatu, na mikanda.
9. ” Usawa wa jinsia ni kitu muhimu katika maendeleo ya jamii.” Jadili.
10. Ni maadili gani unayoyapata kutoka mjadala huu?

## 14.2. Msamiati kuhusu mjadala

***Zoezi la 2:Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. Jitegemea
2. Uchumi
3. Tajiri
4. Rahisisha
5. Karibisha
6. Malighafi
7. Kazi zenye ufanisi
8. Usawa wa jinsia
9. Bidhaa
10. Saidia

***Zoezi la 3: Ambatanisha maneno kutoka safu A na yale ya safu B kulingana na maana kamili.***

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| 1. Tegemezi | a. Kuwa mbele ya kikundi cha watu ili kukielekeza njia |
| 2. Uhondo | b. Tegemea mahitaji kutoka kwa mtu mwingine |
| 3. Desturi | c. Hali ya kufaidi vitu vitamu |
| 4. Ongoza | d. Jambo la kawaida linalotendwa kila siku. |
| 5. Mjadala | e. Kusudi ya kupata shabaha |
| 6. Ustadi | f. Hali ya kuwa stadi |
| 7. Lenga | g. Hali ya kufanikiwa kama vile kijamii au kiuchumi. |
| 8. Maendeleo | h. Mazungumzo ya jambo maalumu kwa kutoa hoja |
| 9. Mkakati | i. Hali ya kuwa na hamu/tamaa kubwa ya kufanya jambo fulani. |
| 10. Shauku | j. Mpango maalumu unaoandaliwa kwa ustadi mkubwa kwa kulenga jambo fulani. |

## 14.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno kuhusu Vivumishi na Vitenzi

***Zoezi la 4: Soma sentensi ifuatayo kisha ujadili neno linalopigiwa msitari na kuandikwa kwenye rangi iliyokoza kisha utunge sentensi sahihi kwa kuiga mfano uliotolewa.***

**Mfano:**

1. Safi ⟶ **Usafi** unahitajika nchini
2. **Refu**
3. **Bora**
4. **Sawa**
5. **Haba**
6. **Fundi**
7. **Tajiri**
8. **Kubwa**
9. **Dogo**

***Zoezi la 5: Soma maelezo muhimu kisha ujibu maswali husika hapo chini***

***Maelezo muhimu***

Katika uambishi, viambishi huweza kuwekwa mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa neno ili kuunda neno jipya lenye tabia mpya. Hali hii huliwezesha neno jipya kuchukua nafasi tofauti na neno la awali; yaani nafasi mpya katika tungo kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

***Vivumishi*** ⟶ ***Nomino***

Kivumishi ni kipashio ambacho hutoa maelezo zaidi juu ya nomino. Kivumishi huelezea nomino hiyo kwa kubainisha jinsi inavyoonekana, inavyofikiriwa ama kuonyesha tabia, idadi, n.k.

Tunaweza kuunda majina kutoka kwa vivumishi:

**Mfano:**

| **Vivumishi** | **Nomino** |
|---|---|
| **Zuri** | **Uzuri** |

Sentensi : 1. Mtoto **mzuri** huwafurahisha wazazi.

2. **Uzuri** wa mtoto hufurahisha wazazi.

**Safi Usafi**

Sentensi : 1. Kila mtu anapaswa kunywa maji **safi** kwa kujilinda magonjwa mbalimbali.

2. **Usafi** wa maji huimarisha afya nzuri ya mwanadamu.

**Mbili Upili**

Sentensi : 1. Kila mwanafunzi hapa atatunga sentensi mbili.

2. Shule za upili ni nyingi nchini kutokana na elimu kwa wote.

**Pya Upya**

Sentensi : 1. Baba yake alimnunulia nguo mpya jana.

2. Baada ya mvua iliyoharibu nyumba za watu, wote watazijenga upya nyumba hizo.

**Tajiri Utajiri**

Sentensi : 1. Watu tajiri hupenda kuwapa kazi watu wengi.

2. Utajiri wangu hautazuia kuheshimu kila mtu.

***B.Vitenzi → Nomino***

Kitenzi ni neno linalotoa taarifa juu ya tendo linalotendeka au linalotendwa na mtu au kitu fulani. Uambishaji wa vitenzi ni utaratibu wa uundaji wa vitenzi vipya katika lugha kwa kuongeza viambishi nyambulishi kwenye mzizi wa kitenzi. Kutokana na vitenzi, tunaweza kuunda majina kwa kufuatilia utaratibu wa kisarufi. Tunaweza kuunda majina mbalimbali kutoka vitenzi:

**Mfano:**

**Vitenzi** **Nomino**

**Kutegemea** **Utegemezi**

Sentensi : 1. Kila mtu ajenge tabia ya kujiepusha na utegemezi.

2 Utegemezi kwa wengine siyo desturi inayofaa utu.

**Kushirikiana** **Ushirikiano**

Sentensi : 1.Ushirikiano ni lazima katika kazi za Umuganda.

2. Ushirikiano wa mke na mume unahitajika katika malezi ya watoto

**Kurahishisha** **Urahisi**

Sentensi : 1. Kutokana na teknolojia kazi hufanyika kwa urahisi.

2. Urahisi wa kazi hutokana na tajiriba katika kazi hiyo.

**Kufunda** **Ufundi**

Sentensi : 1. Ufundi ni kazi inayohitaji ustadi.

2. Shule hii ni ya ufundi wa kujenga nyumba.

**Kuchuma** **Uchumi**

Sentensi : 1. Uchumi wa nchi utaimarishwa na kuongeza idadi ya viwanda.

2. Fulani alijifunza mambo ya uchumi katika chuo kikuu.

***Zoezi la 6: Tunga sentensi zenye nomino zilizoundwa kutokana na vitenzi ulivyopewa***

**Mfano:** Kushirikiana

**Jibu : Ushirikiano** wa kijinsia ni jambo muhimu katika maendeleo ya jamii.

1. Kurahisisha
2. Kuendelea
3. Kusawazisha
4. kuimarisha
5. Kulima
6. Kufuga
7. Kukuza
8. kutengeneza

## 14.4. Matumizi ya Lugha: Sifa za Mjadala

***Zoezi la 7: Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali hapo chini.***

### Maana ya mjadala

Mjadala ni mazungumzo yanayohusu mada mahususi ambayo hufanywa kwa kujenga hoja na kuongozwa na mtu mmoja au watu wawili.

- **Sifa za mjadala**

1. **Suala lililo wazi la mjadala:** Jambo au mada inayojadiliwa ni lazima iwe wazi na yenye kuvutia.
2. **Mpangilio na muungano wa hoja:** Kwa kutoa hoja, inalazimu kuzipanga ifaavyo. Kila hoja ikiwa katika maelezo yake bila ya kuchanganya changanya hoja.
3. **Msimamo dhahiri:** Mwandishi hutoa hoja kwanza au kudokeza msimamo mwanzo kisha mwandishi akatoa sababu za kuchukua msimamo fulani.
4. **Mjadala unaosadikika:** Mwandishi wa mjadala amsadikishe msomaji kwa kutumia mbinu alizochagua ifaavyo, zile zenye ithibati ambazo humwezesha msomaji kuhakikisha ukweli wa jambo alilosoma. Matumizi ya takwimu yanahitajika kwa kutilia mkazo na kuonyesha kinyume cha upande mwingine.
5. **Sauti inayokubalika:** Maandalizi ya mjadala yanamlazimu kuteua na kuyatumia maneno ya kumvutia watakaousoma ili yawatie kukubaliana kuhusu mada iliyozungumziwa au kuandikiwa. Inamlazimu tena matumizi ya lugha yenye heshima hata ikiwa kuna upinzani wa mada lugha yenye matusi na kudharau isitumiwe.
6. **Ufarisi wa lugha na mbinu zake:** Mwandishi atumie lugha teule na mbinu zake kwa kuwalenga wasomaji kama lugha ni muhimu sana katika kila kazi yoyote ya uandishi.

**Umuhimu wa mjadala**

1. Hukuza uwezo wa kitaaluma, fikra na hali ya udadisi pamoja na kushawishi hadhara.
2. Huwezesha mtu kujitambua binafsi kipaji chake cha kuchangia hoja na wengine.
3. Hutufanya tuzoee kuheshimu hoja za wengine, kuwasikiliza na kuachiria nafasi ya kutoa maoni yao.
4. Hutufanya kuheshemu na kutumia muda ifaavyo katika mazungumzo.
5. Husaidia mtu kukuza uwezo wa kupanga mawazo katika mazungumzo.
6. Anayehudhuria hukuza uwezo wa kuyachagua mawazo, kuiunga mada na pia kupinga kauli fulani.

***Maswali***

1. Tofautisha mdahalo na mjadala.
2. Eleza umuhimu wa mjadala kwa mwanafunzi.
3. Jadili kazi ya kiongozi wa mjadala.
4. Kwa nini umilisi wa lugha na mbinu zake ni kitu muhimu sana katika uandishi wowote?
5. "Mjadala unapaswa kuwa unaosadikika." Jadili.

***Zoezi la 8: Jaza mapengo kwa kutumia maneno yanayofaa kutoka parandesi.***

1. Kula uhondo kwataka ……….asiye na matendo hula uvundo. (Uvundo, tenda, matendo)
2. Ukiviona vinaelea…………(vimeundwa, ninaeleza, vitaelea)
3. Kila mwananchi inamlazimu kufuata…………ya kujitegemea (desturi, dazeni, daftari )
4. Tusipende vitu vya…………(bure, kuka, busara)
5. Mwanamke huyu ......................sana (ametajiri, amejitajirisha,amejitajirishwa )
6. Katika jamii nzima………wa kijinsia ni msingi wa maendeleo (usawa,sawa,sawa sawa)
7. Mali bila daftari hupotea bila………… (hatari, habari, hatia)
8. Utamu wa kazi ni…………….. (pesa, poso, pete)
9. Desturi ya kujitegemea hulazimu wanajamii………..bidii.(kufanya, piga ubwana, omba sana)
10. Kazi zenye…………………huleta matunda sana.(ufanisi,urahisi, uratibu)

## 14.5 Kusikiliza na Kuzungumza : Majadiliano

***Zoezi la 9: Andaa mjadala kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:***

1. Usawa wa kijinsia ndio msingi wa maendeleo ya kijamii.
2. Teknolojia ni mojawapo ya njia rahisi za kuzalisha mali na kuboresha maisha ya jamii.
3. Elimu hulinganishwa na msingi madhubuti katika uimarishaji wa desturi ya kujitegemea maishani na kuendeleza jamii.
4. Ndege aamkaye mapema hula wadudu watamu.
5. Akili ni mali.

## 14. 6. Utungaji: Utungaji wa insha ya mjadala

***Zoezi la 10: Chagua mada moja kati ya hizi zifuatazo kisha utunge kifungu cha habari chenye aya zisizopungua tano.***

1. Wajibu wa mwanafunzi katika kujitegemea.
2. Mambo muhimu katika uimarishaji wa tabia na mienendo mizuri ya vijana

# SOMO LA 15: UHUSIANO NA TOFAUTI KATI YA MIDAHALO NA MIJADALA

***Zoezi la 1: Jibu maswali yafuatayo:***

1. Uliwahi kusikia maneno yafuatayo : Mdahalo na mjadala ?
2. Eleza ni kwa namna gani maneno haya yanatofautiana ?
3. Maneno haya yana faida gani kwa jamii?

## 15.1. Kusoma na Ufahamu: Midahalo na mijadala

*Soma kifungu cha habari kuhusu "Midahalo na Mijadala' kisha jibu maswali uliyopewa hapo chini.*

Mara nyingi wanafunzi wa Kiswahili wa shule za sekondari nchini Rwanda hujadiliana kuhusu mada za aina mbalimbali. Majadiliano yao hufanywa kwa kuzingatia taratibu za mazungumzo ya aina ya midahalo au mijadala. Madhumuni ya majadiliano hayo ni kukuza uwezo wa wanafunzi hao wa kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha. Licha ya umuhimu wa mazungumzo ya aina hii, wanafunzi wengi huendelea kuchanganya mjadala na mdahalo kwa kufikiria kwamba yote ni mazungumzo tu na kusahau kuwa utekelezaji wake hutofautiana.

Katika mdahalo, watu hujadiliana baada ya kujigawa katika makundi mawili yenye misimamo tofauti kulingana na mada iliyochaguliwa. Miongoni mwa mazungumzo mengi yanayofanywa, mdahalo ndio unapendwa na wanafunzi wengi. Wao husema kuwa katika mdahalo wazungumzaji hupata fursa ya kuonyesha fikra zao kuhusu mada iliyotolewa kiasi kwamba majadiliano yenyewe haya huwa ni mashindano ya hoja. Wasemaji waliopo katika mdahalo huwania kuupata ushindi dhidi ya wenzao wenye msimamo tofauti na wao kwa kushawishi hadhira ili iwaunge mkono.

Mazungumzo haya yanapofanywa, wasikilizaji hutega sikio na hufurahia kusikiliza hoja zinazotolewa na pande mbili katika mdahalo. Upande wa utetezi huitetea

mada iliyopo na hushikilia mawazo yenye kuunga mkono mada hiyo. Upande wa upinzani nao hulenga kutafuta hoja na mifano ya kuthibitisha maoni yao kwa kupinga mada na maoni ya watetezi ili kuwaridhisha wasikilizaji washiriki. Pande hizi hujadiliana kwa kuongozwa na mwenyekiti na kuheshimu nidhamu katika malumbano yao. Hivyo mazungumzo yenyewe huwa mashindano ya watetezi na wapinzani kimawazo.

Mwenyekiti ndiye huwajibika kufungua mdahalo na kuongoza wazungumzaji wote kwa kuwachagua wasemaji bila kuonyesha upendeleo wowote, akihakikisha kwamba kuna nidhamu wakati wa kutoa mawazo. Kila msemaji anatumia muda aliopangiwa na mwenyekiti. Mazungumzo yanapofikia kikomo, yeye humkaribisha katibu kumsaidia kuongoza zoezi la kupiga kura na kutoa muhtasari wa mambo yaliyozungumziwa. Baadaye mwenyekiti hufunga mdahalo. Hali kadhalika wajibu wa katibu katika mdahalo ni kuandika muhtasari wa hoja zinazotolewa na wasemaji wa pande zote zinazohusika, kuzisoma kwa hadhira na kutangaza matokeo ya kura zilizopigwa.

Aidha, mazungumzo mengine yanayochangia kukuza uwezo wa wanafunzi wa kutumia lugha ya Kiswahili huchukua utaratibu tofauti kidogo na ule wa mdahalo. Hapa mazungumzo hufanywa kuhusu suala fulani linalohitaji kujadiliwa na kutafutiwa ufumbuzi. Mazungumzo ya aina hii ndiyo hujulikana kwa jina la mijadala. Mazungumzo haya pia husifiwa kwa mchango wake katika kukuza kiwango cha kutafuta masuluhisho kwa masuala mbalimbali yanayoikabili jamii.

Katika mjadala, ni lazima pia kuwepo kwa mwenyekiti ambaye anaongoza majadiliano. Yeye hufungua mjadala, huchagua wazungumzaji wa kutoa michango yao kuhusu suala husika na kuhakikisha kwamba kila msemaji anatumia muda aliopangiwa. Mzungumzaji aliyechaguliwa kusema huweza kutoa hoja zake kulingana na anavyolifikiria suala bila kushikilia upande wowote. Mara nyingi, mjadala huweza kufanyika katika makundi madogo au makubwa na kiongozi hutoa mwongozo kuhakikisha kuna mwenendo mwema kati ya washiriki wa mjadala huo. Majadiliano yanapokaribia kufikia kikomo, mwenyekiti hukumbusha mambo muhimu yaliyozungumziwa na huwashukuru waliohusika katika mjadala huo.

Kwa hakika, mdahalo na mjadala yote ni mazungumzo, lakini taratibu zinazozingatiwa katika utekelezaji wa mazungumzo yenyewe hutofautiana. Mazungumzo hayo husaidia kila mwanafunzi kujizoeza kutumia lugha fasaha, kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri na pia kwa kujiegemeza katika mifano kamili kila anapotoa hoja zake. Mada za mdahalo na mjadala hutofautiana kwani lengo la mada za mijadala ni kutafuta suluhisho kwa jambo linaloikabili jamii fulani ilhali mdahalo huhitaji wapinzani na watetezi ambao huwania kuibuka na ushindi.

**Maswali ya Ufahamu**

1. Taja wahusika wanaoshiriki katika mdahalo kisha ueleze wajibu wao.
2. Mjadala hushirikisha watu gani? Eleza shughuli za kila mmoja wa washiriki hao.
3. Eleza uhusiano uliopo kati ya mdahalo na mjadala.
4. Bainisha mambo muhimu yanayotofautisha mdahalo na mjadala.
5. Eleza manufaa ya kufanya mazoezi mengi ya midahalo na mijadala kwa wanafunzi

## 15.2. Msamiati kuhusu Kifungu

***Zoezi la 2: Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo.***

1. Katibu
2. Mwenyekiti
3. Kikomo
4. Ufasaha
5. Nidhamu
6. Mdahalo
7. Maoni
8. Kutetea
9. Makundi
10. Ufasaha

***Zoezi la 3: Husisha neno katika sehemu A na maana yake katika sehemu B.***

| A Neno | | B Maana ya neno |
|---|---|---|
| 1. Matokeo | | a. Hali ya kuweza kufanya jambo |
| 2. Mtetezi | | b. Mambo yanayojadiliwa na kukatiwa |
| 3. Ushirikiano | | c. Mazungumzo ya watu wawili au zaidi wanaobadilishana mawazo kuhusu mada fulani |
| 4. Uwezo | | d. Mtu anayepigania haki au jambo la mtu mwingine ili asionewe |
| 5. Majadiliano | | e. Mtu asiyekubaliana na jambo au fikra za mtu au watu wengine |
| 6. Mpinzani | | f. Hali ya kuungana na kuwa na mwelekeo mmoja katika jambo |
| 7. Kushawishi | | g. Wahudhuriaji, wasikilizaji au watazamaji |
| 8. Katibu | | h. Kumpa mtu maelezo ili kutaka kumfanya akubali kufuata fikra au maelezo yako |
| 9. Hadhira | | i. Mtu anayefanya kazi za kuandika na kuhifadhi maandishi ya shirika |
| 10. Masuala | | j. Mambo yanayopatikana baada ya kitendo fulani |

***Zoezi la 4: Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia maneno yanayofaa kati ya haya: Kiwango, kuheshimu, kuelewa, kushiriki, anaandika, matamshi, mjadala, mdahalo, lugha, majadiliano.***

1. Mwanafunzi wa lugha anajizoeza kutumia ………… bora wakati wa mdahalo.
2. Katibu wa mdahalo …………… hoja zilizotolewa na wasemaji.
3. Mdahalo humpasa mshiriki kuwa na moyo wa ……… mawazo ya wengine.
4. Mjadala ni ………………. yanayohusisha watu wengi.
5. Washiriki wa ……………….. ni lazima watoe maoni yao bila kuegemea kwa upande wowote.
6. Midahalo na mijadala humsaidia mwanafunzi kutambua …………… chake katika lugha.
7. Katika ……………………. mwenyekiti ndiye ambaye anachagua atakayesema.
8. Kila mtu aliyealikwa anaombwa ……………… katika majadiliano.
9. Anayeshiriki katika mazungumzo anakuza utumiaji wa …………..
10. ..........................................mada ni chanzo cha kutoa maoni mazuri.

## 15.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno

***Zoezi la 5: Unda vielezi kutoka kwenye vivumishi ambavyo vimepigiwa mstari, kisha utunge sentensi kwa kutumia kielezi hicho***

***Mfano:*** Angalia watoto wale **wema.**

⟶ Wema: **vema**

- Wanafunzi wangu hufanya mtihani vema.

1. Chuki ni jambo **baya** la kuepuka.
2. Majira ya kiangazi ni wakati wa jua **kali** kabisa.
3. Watu **wazuri** mara nyingi hupenda kusaidia maskini.

- **Chunguza maelezo haya yafuatayo kuhusu uambishaji wa maneno**

Kama ilivyoelezwa katika masomo yaliyotangulia somo hili, maneno huweza kuundwa kutokana na maneno mengine kwa kutumia viambishi tofauti. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali ya kuunda maneno mengine kutokana na vielezi. Hali kadhalika, vielezi navyo huweza kuundwa kutokana na maneno mengine.

- **Uundaji wa maneno mengine kutokana na vielezi**

Kwa kutumia vielezi, maneno mapya huweza kuundwa. Katika hali hii, vielezi huambishwa viambishi vya aina mbalimbali kama tunavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo.

**Mfano:**

1. **Haraka:** harakisha, harakisho, uharakishaji.
2. **Tayari:** tayarisha, tayarisho, utayarishaji, mtayarishaji.
3. **Binafsi:** ubinafsi, ubinafsishaji, binafsisha.
4. **Karibu:** ukaribu, karibia, karibisha, ukaribishaji.

- **Uundaji wa vielezi kutokana na maneno mengine**

Huu ni uundaji wa vielezi kutoka kwa maneno mengine. Vielezi vinavyozaliwa kwa namna hii huwa ni vielezi vya namna. Kuna vielezi kutoka majina na vielezi kutoka vivumishi. Uundaji wa vielezi kutoka majina hufanyika kwa kuweka kiambishi awali ki- mbele ya shina la jina.

**Nomino** ⟶ **Kielezi**

**Mfano:**

- Mzungu: kizungu

**Sentensi:** Rafiki yake anaimba kizungu.

- Tajiri: kitajiri

**Sentensi:** Mugisha anatembea kitajiri.

- Mtoto: kitoto

**Sentensi :** Wachezaji hawa walicheza kitoto.

- Mke: kike

**Sentensi:** Mvulana yule amepenya kike.

**Kivumishi** ⟶ **Kielez**i

**Kwa mfano:**

- Zuri : vizuri

**Sentensi :** Kazi hii imefanyika vizuri

- Ema : vema (alifanya vema)

**Sentensi** : Mama yao alipewa ng'ombe kwani alimtendea vema mwaka jana.

- Kali : vikali (walipigana vikali)

**Sentensi:** Magari yaligongana vikali wakati wa ajali ile ile.

- Baya: vibaya

**Sentensi :** Alimwambia vibaya shangazi wakati wa harusi ya binamu yake.

## 15.4. Matumizi ya Lugha : Mdahalo na Mjadala

***Zoezi la 6: Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali hapo chini***

- **Uhusiano kati ya mdahalo na mjadala**

Mdahalo na mjadala huhusisha watu wengi wanaojadiliana kuhusu jambo fulani.

Mazungumzo katika mdahalo na mjadala huhusisha kiongozi wa kuanzisha na kusimania mambo mpaka mwisho. Mdahalo na mjadala huwa na malengo sawa ya kukuza utamaduni wa kuheshimiana, kukuza matumizi fasaha ya lugha na matamshi yake bora, kukuza uwezo wa kusema hadharani na kuwapa watu fursa ya kuelewana na wengine mbalimbali pamoja na kumwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika au kuelezea insha au habari.

- **Tofauti kati ya mdahalo na mjadala**

**Mdahalo** huhusisha pande mbili: upande wa utetezi na upande wa upinzani. Huwasaidia wanafunzi kushiriki katika utetezi au upinzani wa jambo fulani. Unaongozwa
na mwenyekiti pamoja na katibu. Katika mdahalo, wazungumzaji hushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo yao kuhusu jambo fulani. Mdahalo huzoeza watu kusikiliza, kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine.

Kwa upande mwingine, **mjadala** ni mazugumzo juu ya jambo husika katika makundi madogo au makubwa. Unaongozwa na mwenyekiti mmoja wa kuzusha mawazo, kuhakikisha kwamba kuna kuheshimiana kati ya washiriki na kutoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa mwishoni. Mjadala huhusika na mada ambazo zinahitaji ufafanuzi kutokana na mchango wa mawazo ya wengi. Anayetoa hoja yake, anaweza kukubali au kupinga maoni ya mwenzake kwa kutoa mchango wake wa kutatua tatizo linalojadiliwa.

***Maswali:***

1. Kwa nini wapinzani hutaka kushawishi hadhira katika mdahalo?
2. Je, katibu ana kazi yoyote katika mjadala? Ikiwa anayo kazi eleza, ikiwa hana sema sababu.
3. Linganisha majukumu ya mwenyekiti katika mjadala na yale mdahalo kwa kusisitizia yaliyopatikana ndani ya moja ya majadiliano hayo.
4. Nini umuhimu wa mdahalo kwa washiriki wake?
5. Mada za mjadala huwa na maumbile gani?

## 15.5. Kusikiliza na kuzungumza : Majadiliano

***Zoezi la 7:***

***1. Kwa kushirikiana na wenzako, toa hoja nne za kuonyesha kwamba mada ifuatayo ni kweli kisha uziwasilishe darasani.***

"Majadiliano huimarisha utamaduni wa amani.

***2. Toa hoja tatu za kutetea mada inayofuata na tatu ambazo zinaipinga na kuzielezea wanafunzi wenzako.***

"Ndoa za zamani nchini Rwanda zilikuwa nzuri kuliko ndoa za kisasa."

## 15.6. Kuandika: Utungaji wa mjadala

***Zoezi la 8: Unda mada inayohusiana na desturi ya kujitegemea. Tunga mjadala wa ukurasa mmoja kamili au zaidi kuhusu mada uliyoiunda.***

### TATHMINI YA MADA YA NNE

1. Toa sifa zinazotofautisha mdahalo kwa mjadala.
2. Wewe umechaguliwa kuongoza mdahalo. Eleza jinsi utakavyouongoza toka mwanzo mpaka mwisho.
3. Jadili nafasi ya mdahalo katika bunge la taifa la Rwanda.
4. Fanya maandalizi ya mdahalo usiozidi kurasa mbili kuhusu

   "Mahari hupotosha mila na desturi za jamii siku hizi."
5. Shiriki mjadala kuhusu mada ifuatayo:

   "Elimu ndio msingi madhubuti wa maendeleo endelevu"

## MAREJELEO:


MASEBO, N. C. (2002). Kiswahili Kidato cha Tatu na Nne Maendeleo ya Kiswahili, Fasihi, Sarufi, Matumizi, Utungaji na Ufahamu. Dar es Salaam: NYAMBARI NYANGWINE PUBLISHERS

Massamba D.P.B., Kihore, Y. K., Hokororo, J.I. (2009). Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mlaga. W. K. (2017). Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21. Heko Publishers Ltd. Dar es salaam.

Ndalu, A., S. M. (2013). Johari ya Kiswahili Rwanda Kidato cha Nne Kitabu cha mwanafunzi. Kigali: East African Publishers Rwanda Ltd.

NIYOMUGABO, C. (2013). Mafunzo ya kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi. Kigali: Fountain Publishers Rwanda Ltd.

NIYIRORA E., NDAYAMBAJE L. (2012). Kiswahili Sanifu kwa Shule za Sekondari. New Delhi: Tan Prints (India) Pvt.Ltd.

NIYOMUGABO, C. (2013). Mafunzo ya Kiswahili kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha 6.Kigali: Fountain Publishers Rwanda Ltd.

Nkwera, F.V.M. (1979). Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

NTAWIYANGA, S., Muhamud A, Kinya J na Sanja L, (2018), Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Mchepuo wa Lugha, Kidato cha Sita. Nairobi, Longhorn Publishers.

TUKI. (2006). English Swahili Dictionary 3rd Edition. Dar es Salaam: Book Printing Services Ltd.

TUKI. (2004). Kamusi ya Kiswahili Sanifu.Nairobi: Oxford University Press.

Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari (1987). Kitabu cha Kiswahili III B. Kigali: Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari.

Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari (1987). Kitabu cha Kiswahili IV-V B. Kigali: Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari.